ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1. Mhe. Ali Abdalla Ali	Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini.
2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni.
3. Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake.
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais.
5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani.
6. Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais.
7. Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Tumbatu.
8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais.
9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais.
10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
11. Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/ Waziri wa Afya/ /Jimbo la Ziwani.
12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais.
13.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Kuteuliwa na Rais.
14.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais.
15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni.
16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge.
17.Mhe Dr. Sira Ubwa Mamboya	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Kuteuliwa na Rais.
18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara,Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni.
19.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.
20.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi.
21.Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni.
22.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.

23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole.
24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.
25. Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake.
26.Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake.
28.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi.
29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni.
30.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae.
31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake.
32.Mhe. Said Hassan Said	Mwanasheria Mkuu.
33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
35.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
36.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
37.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
40.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
44.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
45.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
46.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
47.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
48.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
49.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni

53.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Jimbo la Bumbwini
58.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi	Jimbo la Chambani
61.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
65.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
66.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
67.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
68.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
70.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
71.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
72.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
74.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
75.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	Jimbo la Jang'ombe
79.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Saba – Tarehe 29 Januari, 2015

(Kikao Kilianza saa 3:00 asubuhi)

Dua

Mhe. Mwenyekiti: (Mhe. Mgeni Hassan Juma) Alisoma Dua.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 55

Hifadhi ya Maeneo ya Historia

Mhe. Saleh Nassor Juma -(Kny: Mhe. Nassor Salim Ali) Aliuliza:

Kwa kuwa Zanzibar ina maeneo mengi ya historia ambayo kama yatatunzwa, kuhifadhiwa pamoja na kutangazwa nje ya nchi yanaweza kuwa kivutio kikubwa cha watalii na hatimaye kuweza kuinua pato la Taifa. Mfano wa maeneo hayo kwa Pemba ni kama vile magofu ya Mkamandume Pujini, Pango la Watoro iliyoko – Kaskazini Pemba, Mvumo Panda ulioko Kisiwa Panza pamoja na gofu la nyumba ya mapumziko ya Mfalme iliyoko Makaani Vitongoji.

(a) Je, ni kwa kiasi gani maeneo hayo yamehifadhiwa na kuchangia mapato katika uchumi wa nchi.

(b) Kwa kuwa kuna maeneo mengi ya kihistoria kama vile Rasi Mkumbuu, Chwaka, Tumbe na Jambangome hayako katika uhifadhi mzuri, je, ni lini maeneo haya yatahifadhiwa na kuwekwa vizuri ili yawe kivutio cha watalii na kuchangia mapato ya nchi yetu.

(c) Je, maeneo mangapi tayari yamehifadhiwa na kuwekewa walinzi na wahudumu kwa ajili ya wageni.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo - Alijibu**:**

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 55 lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kwanza napenda kufahamisha kwamba Zanzibar ina maeneo ya kihistoria yapatayo 85 Unguja na Pemba. Maeneo haya ni kweli yakitunzwa, yakahifadhiwa na kutangazwa nje ya nchi yataweza kuwa kivutio kikubwa cha watalii na hatimaye kuinua pato la Taifa. Ili kuweza kuyatunza, kuyahifadhi, kuyajenga upya na kuyatangaza maeneo hayo 85 hadi kuwa kivutio cha watalii inahitajika bajeti kubwa. Kwa mfano moja tu utafiti tulioufanya ili kulitunza na kulirejesha upya katika hadhi yake jengo la Beit- Al Ajaib linahitaji karibu shilingi bilioni tano.

(a) Maeneo hayo yanahifadhiwa kulingana na kiwango cha fedha kinachopatikana kila mwaka.

(b) Maeneo ya Ras Mkumbuu, Chwaka, Tumbe na Jambangome ambayo hayako katika uhifadhi mzuri yameandaliwa mpango maalum wa kuyashughulikia. Kwa kuwa kuna maeneo mengi ya kihistoria yanayohitajika kuhifadhiwa, mkazo uliowekwa ni kushughulikia eneo moja moja kulingana na uwezo tulionao. Kwa mujibu wa mpango wa maabara ya Utalii, Ras Mkumbuu imewekwa katika mwaka ujao wa fedha kujengwa ukuta wa kuzuia maji ya bahari yasiingie katika eneo hilo.

(c) Yako maeneo mengine tuliyoyatengeneza katika katika kipindi cha hivi karibuni. Miongoni mwa maeneo hayo ni pamoja na Kijichi, Kwa Bi Khole, maeneo ya mahandaki yaliyotumika katika vita vya pili vya dunia, eneo la pango la watumwa na mnara vyote vilivyoko Mangapwani. Aidha, ujenzi wa makumbusho kwenye pango la Kumbi umemalizika.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Mwenyekiti, mbali na majibu ya Mhe. Waziri katika majibu yake amesema kwamba yako maeneo mengi ambayo yamehifadhiwa katika kipindi cha hivi karibuni. Swali langu ni kwamba maeneo haya yaliyohifadhiwa yakiwemo maeneo ya Kidichi, Bi Khole, Mangapwani kwa upande wa Unguja.

Je, kwa upande wa Pemba ni maeneo mangapi ambayo yamehifadhiwa ili kuweza kuitangaza Zanzibar katika kisiwa cha Pemba.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, uhifadhi wa maeneo ya kihistoria ni shughuli inayoendelea katika Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. Katika kufanya shughuli hizi huwa tunatafuta kila aina ya uwezo wa kufanya kazi hizi.

Katika kipindi kilichopita tulishirikiana na mradi wa *MACEMP* tukajaribu kuyahifadhi maeneo mengi yakiwemo ya Chwaka tulijaribu kuhifadhi pale na zikaingizwa fedha nyingi ambazo pia tulianzisha Kamati ya Wenyeji ya kuona kwamba tunashughulikia pamoja. Chwaka tumefanya kazi hiyo eneo la Pujini pia tumefanya kazi hiyo tumejenga jengo pale na pia tulianza kazi kule Ras Mkumbuu lakini haikumalizika na ndio maana hivi sasa tumeingiza katika Utalii ili kuona kwamba kazi ile inafanyika kwa ufanisi eneo ambalo linahitaji kufanya kazi kwa kiwango kikubwa sana.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Mhe. Mwenyekiti, kuna maeneo hata yale mabango yake hayapo na yamechakaa hasa katika kijiji cha Tumbe huko anakozungumzia kuwa wamo ndani ya kukarabati.

Je, Mhe. Waziri kuendelea kubakia katika maeneo yale hata mabango hayasomeki huko ni kuendeleza hayo maeneo ya kihistoria au ni kuyadhalilisha. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kama nilivyosema kwamba kazi ya kuyarudisha katika hali yake maeneo haya 85 yanahitaji fedha nyingi sana na ndio maana katika kuyahifadhi serikali kwa makusudi ikakubaliana kwamba ishirikiane na wanavijiji wenyewe yaani Kamati za Vijiji kuona kwamba kazi ya kuyahifadhi tunaenda nayo pamoja. Kuna mambo makubwa ambayo wizara na serikali tunaendelea kuyashughulikia, lakini mambo madogo madogo tumekubaliana kamati wenyewe washughulikie.

Mhe. Mwenyekiti, basi hata kuandika Bango iwe atokee waziri na wizara ambapo kamati ipo. Basi kama hivi sawa kama kamati zinashindwa kuandika Bango la kuyashughulikia maeneo yenyewe tutafanya hivi Mheshimiwa kazi. Lakini tumekubaliana kwamba maeneo hayo ya kihistoria ni maeneo yetu pamoja katika nchi yetu sisi na wananchi wenyewe tunashirikiana katika kuyahifadhi na kuyatunza kwa maslahi ya vizazi viliopo na vizazi vijavyo.

Kwa hivyo, si vibaya kamati zenyewe mambo madogo madogo ukiona mabango yale yamechakaa au maandishi yametoka kamati zikafanya kazi hizo ndogo ndogo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Mvumo kwa kawaida huwa hautoi Mapanda na ni miongoni mwa miti muhimu kupatikana katika Jangwa la Sahara, ni miongoni mwa miti muhimu sana na kwa kuwa Kisiwa Panza kuna Mvumo umetoa mapanda manne unaitwa Mvumo Panda. Kwa kuwa Mvumo huu huwa wanapenda sana watalii kutoka sehemu kadhaa hasa kutoka katika nchi hizi za *Gulf* wanapenda sana kuja kuuangalia ule Mvumo wenye mapanda manne.

(a) Je, ni sababu gani za msingi zilizoifanya SMZ hadi leo hii kwamba hawajauhifadhi ule mvumo na hawajaunadi katika Soko la Kimataifa.

(b) Kwa kuendelea kuacha Watalii kuja kuja tu hivi kienyeji pale wakiuangalia, huoni kwamba Mhe. Waziri ni kuipotezea mapato Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, Mvumo Panda ulioko Kisiwa Panza katika jimbo la Mkanyageni sisi wizara tunaufahamu, tunauelewa na kwamba ni kweli ni eneo ambalo la maajabu na ule mti wenyewe ni wa maajabu maajabu na watu wengi wanakwenda kuuangalia. Sasa ule ni mti, na mti ni kiumbe ambacho kina uhai unaweza ukasema leo unauhifadhi lakini kesho na keshokutwa ukifika ukaona umeshakufa.

Kwa hivyo, yako mambo Mhe. Mwenyekiti, serikali kabla haijachukua hatua kubwa za kuhifadhi na kuitangaza lazima tufanye utafiti wa kina kuona kwamba tusije tukahifadhi jambo la gharama kubwa tukatia katika magazeti, Gazeti la Serikali tukaitangaza halafu ni kiumbe ambacho keshokutwa tukaona Mvumo umeanza kuyayuka umeanza kukatika mapande watu wanakuja kutoka nje kuangalia Mvumo uko chini.

Sasa hayo Mhe. Mwenyekiti, ni mambo ambayo yanahitaji utafiti mpana, hilo ndilo jambo ambalo wizara yangu kwanza inafanya kabla ya kuchukua hatua hizo za kuutangaza na katika Magazeti ya Serikali kwamba ni jambo ambalo linahifadhiwa.

Kuhusu suala la kusema kwamba wageni wanakwenda, ni kweli kuna baadhi ya wenye *Tour Operator* wanajaribu kupeleka peleka wageni. Hili ni jambo zuri kuweka katika nchi yetu kuona kwamba kuna kianzio cha Kitalii ambacho wageni wanapelekwa tunawashukuru, na sio eneo hili tu kuna baadhi ya minazi imepinda pinda imefanya kama *cross* pia watu wanapeleka ni katika kujaribu kuangalia vianzo vyengine vya utalii vya nchi yetu.

Kwa hivyo, tunawaomba *Tour Operators* popote pale walipo wakiona kuna eneo ambalo ni zuri basi washirikiane na Kamisheni ya Utalii ili kuona kwamba ni eneo ambalo wageni wetu wanaweza kwenda.

Nam. 58

Sensa kwa Filamu ziendazo Kinyume na Maadili

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza**:**

Kazi zote za sanaa hutakiwa zitoe mafunzo pamoja na kuelimisha jamii. Kwa kuwa wasanii pamoja na vikundi vingi vya sanaa za maonesho zikiwemo zile za filamu za Kitanzania kazi zao za sanaa haziendani na mila, silka pamoja na utamaduni wa Kizanzibari pale wanaposhindwa kuvaa mavazi ya stara.

Je, ni lini Serikali itafanya uhakiki makini wa kazi hizi na kuzizuia kuingia nchini kazi zote za sanaa zinazokwenda kinyume na maadili ya Zanzibar yakiwemo mavazi yasiyokuwa na staha.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo - Alijibu**:**

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 58 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kazi zote za sanaa zikiwemo za filamu hutakiwa kutoa mafunzo pamoja na kuelimisha jamii. Kwa kuelewa umuhimu huo, Serikali imekuwa ikichukua tahadhari kubwa kuona kazi hizo za sanaa haziendi kinyume na mila, silka na utamaduni wetu.

Katika kuhakikisha hayo, Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo inazingatia utekelezwaji wa Sheria Nam. 1 ya 2009 ya Bodi ya Sensa. Sheria hii iliundwa kwa lengo la kuhakikisha kazi zote za sanaa na utamaduni zinahakikiwa ili kuhakikisha mafunzo yanayopatikana katika sanaa hizo yanaenziwa, kulindwa, kukuzwa na kuendeleza mila, silka na utamaduni wetu.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa lengo la SMZ katika masuala ya kupambana na Ukimwi ni kufikisha 000, kwa maana Maambuzi mapya 0 Ukimwi 0, HIV 0, na kwa kuwa inaonekana kwa kiasi kikubwa sana kazi hizi za sanaa zinachangia sana katika suala zima la kuhamasisha Ngono zembe, na kwa kuwa miaka ya nyuma tulikuwa tukipata burudani na tulikuwa tunaburudika sana na tulikuwa tunaburudika na kazi za sanaa walizokuwa wakiendesha akina mama Siti binti Saadi, Marehemu Kidude binti Baraka wao walikuwa wanaimba huku wanajifunika nyuso zao, lakini sauti yao ilikuwa inatuburudisha.

Je, ni lini sasa mtatunga sheria ya mavazi hasa ya wana sanaa kusudi baada ya kuhamasishwa katika mambo maovu tukawa zaidi tunapata burudani kulikoni kupelekea mambo hayo machafu ambayo hayana maadili. Ni lini mtawatungia sheria hasa hawa wasanii, achilia mbali kazi zao lakini hapa wanaponengua katika majukwaa huwa wanacheza nusu uchi. Sasa ni lini mtatunga sheria za kuzuia mambo haya ya kucheza nusu uchi.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, mapungufu hayo katika sheria tumeyaona na tukijaaliwa mwisho wa kikao hichi tutasoma kwa mara ya kwanza marekebisho ya Sheria ya Bodi ya Sensa na Baraza la Sanaa la Zanzibar. Kwa hiyo, hiyo ndiyo jitihada ya serikali ambayo wanaifanya

Nam. 63

Msongamano wa Gari Barabara ya Mwanakwerekwe- Tunguu

Mhe. Subeit Khamis Faki (Kny: Mhe. Ali Salum Haji) - Aliuliza**:**

Kutokana na ukuaji wa mji kutoka Mwanakwerekwe hadi Tunguu kumepelekea kuongezeka kwa matumizi ya barabara na kupelekea baadhi ya wakati msongamano wa magari na kuhatarisha usalama wa watu wanaotumia barabara hiyo.

Je, Wizara ina mpango gani katika kupata ufumbuzi wa haraka wa ujenzi wa barabara hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu**:**

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Namba 63 kama ifuatavyo;-

Mhe. Mwenyekiti, serikali imeshakamilisha upembuzi yakinifu na kuandaa makabrasha ya zabuni (*Tender documents)* kwa ajili ya kazi za upanuzi wa barabara mbalimbali zinazoingia kwenye mji wa Zanzibar (*Zanzibar town entry roads)* zenye jumla ya kilomita 78. Serikali inatafuta fedha za ujenzi wa barabara hizo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo mbalimbali. Barabara ya Mwanakwerekwe – Tunguu ni miongoni mwa barabara hizo ambayo itapanuliwa kuwa barabara mbili *dual carriage way*.

Mhe. Mwenyekiti, hata hivyo wakati Serikali ikiendelea kutafuta fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, Wizara yangu kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara kwenye mwaka wa Fedha 2014/2015 ilitenga fedha kwa ajili ya kuanza matengenezo ya barabara kutoka Mwanakwerekwe makaburini mpaka Fuoni njia ya Kwarara (1.78km) kwa kuanzia, na kwenye mwaka wa Fedha 2015/16 Wizara itatenga tena fedha za kuendelea na matengenezo ya barabara hiyo kama Serikali haitafanikiwa kupata fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

Wizara inakamilisha taratibu za kuandaa zabuni kulingana na ukubwa wa kazi zilizopangwa kwa ajili ya kutangaza na kazi zitaanza baada ya kumpata Mkandarasi atakayeshinda zabuni hiyo.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri nataka nimuulize swali dogo tu la nyongeza.

Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akijibu swali mama ameelezea namna ya Serikali inavyojitahidi na kuonesha nia njema ya kutengeneza barabara kuu za mji wetu wa Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, pamoja na jitihada na nia njema ya kutengeneza barabara hizo kuu, lakini nataka niipongeze Serikali kwa kuanza kuonesha nia njema ya kuzitengeneza barabara za ndani *(feeder roads)* katika mji wa Zanzibar lakini hususan katika maeneo ya Mji Mkongwe na maeneo ya Fuoni kwenye njia mbali mbali.

Lakini ninataka nimuulize ni lini wataboresha barabara za ndani katika maeneo ya Ng'ambu badala ya Mji Mkongwe na maeneo ya magharibi. Kwa mfano, barabara ya Daraja Bovu/Saateni, Amani-fresh/Mboriborini, Magomeni kwa wazee na Mwembeladu Miti Ulaya.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, barabara takriban zote zipo katika mamlaka ya kujengwa na Manispaa ama Halmashauri, lakini kwa kutambua uwezo wa Halmashauri na Manispaa yetu, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa kushirikiana na Mfuko wa Barabara tumekuwa na kawaida ya kusaidiana katika ujenzi kwa maeneo hayo. Barabara alizozitaja zimo barabara mbili ambazo sisi kama Wizara kwa kushirikiana na wenzetu wa Mfuko wa Barabara tumeanza ukarabati. Barabara kutoka kwa Abass Hussein mpaka Shaurimoyo-Darajabovu.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia madhumuni makubwa ni kuona kwamba barabara hizi tutaziimarisha ili kuweka mandhari nzuri kwa ajili ya mji wetu. Kwa hivyo nimuombe tu Mhe. Mwakilishi kwamba atupe ushirikiano, sisi kwa kushirikiana na wenzetu wa Mfuko wa Barabara tutafanya matengenezo barabara hizi zote na tukimaliza tutaanza kuona barabara za ndani za mitaani nazo namna gani zinaweza kuimarishwa kwa kushirikiana na wenzetu wa Mfuko wa Barabara, Halmashauri pamoja na Manispaa.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi napenda kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza.

Katika swali lake mama Mhe.Naibu Waziri alisema kwamba kumetengwa kiasi cha fedha cha kujengea barabara hizo. Je, ni kiasi gani cha fedha ambacho kimetengwa katika ujenzi wa barabara hizo.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, katika majibu ya msingi tulieleza kwamba kulikuwa kuna mambo mawili. La kwanza ilikuwa ni mradi mkubwa wa *Town Entry Road* ambao una kilomita 78 ambapo makisio yameshafanywa, bado fedha hazijapatikana tunaendelea kuwaomba wahisani na wafadhili waweze kutusaidia.

Tulichokisema kwamba fedha ambazo tumezipanga katika Mfuko wa Barabara ni kutoka pale Makaburini mpaka Fuoni Msikitini kwa kuongeza njia mbili. Kwa hivyo kuna takriban kuna shilingi milioni mia moja na hamsini zitakazoanzia kazi hiyo na utaratibu wa kutoa zabuni tayari tumeshauanza kukamilisha zabuni, tutatoa kazi hii ianze kufanywa ili kuona eneo lile nalo tunaondoa usumbufu ambao umejitokeza.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa fursa nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza.

Kwa kuwa barabara hii anayoitaja Mheshimiwa aliyeuliza Mhe. Ali Salum Haji, barabara ya Mwanakwerekwe ambayo inakuwa na msongamano wa magari, na kwa kuwa barabara hii ilipanuliwa lakini ikawa na barabara mbili. Lakini hata hivyo Mwanakwerekwe kwa sababu kuna soko, na soko lenyewe lipo karibu na barabara kunakuwa na msongamano wa magari hasa kipindi cha asubuhi na jioni kwa sababu gari za barabara hii ni nyingi sana.

Mhe. Mwenyekiti, sasa Mhe. Naibu Waziri kwa kuwa wenzetu kule Dar es Salaam kama maeneo ya Manzese kumejengwa barabara ya juu ya kukatisha watu kuingia upande wa pili tu, ni daraja la kutoka barabara hii ukaingia upande wa pili kwa ajili ya waenda kwa miguu. Na kwa kuwa waenda kwa miguu Mwanakwerekwe wanasababisha gari kuwa na msongamano zaidi.

Je, haoni Mhe. Naibu Waziri kuna haja ya kujenga daraja la wapita miguu wakakatisha ili kuzipisha gari ukapunguka ule msongamano wa magari. Na je, kwa kuwa soko lipo karibu na ile *junction* ya kugeuza magari pale haikuwekwa vizuri, ni lini Serikali itaona utaratibu wa kupanua vizuri pale ili magari yapate kugeuka isisababishe msongamano wa magari.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi maswali yake ya nyongeza kwa pamoja kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, ametoa mfano wa Manzese lakini naamini kwamba daraja la Manzese halikujengwa kwa sababu ya msongamano, limejengwa kwa ajili ya usalama wa watu wanaokiuka kutoka ng'ambu moja kwenda ng'ambu ya pili. Msongamano uliopo Mwanakwerekwe sokoni hausababishwi na watu wanaokata au wanaokatisha barabara kwa miguu.

Mhe. Mwenyekiti, msongamano wa Mwanakwerekwe unasababishwa na magari. Kwa hivyo sisi rai yetu ni kuwaomba tu wenzetu wa Jeshi la Polisi wanaosimamia usalama wa barabarani wawe makini katika kusimamia watu wageuze magari eneo husika. Dhana ya kujenga daraja nadhani wakati ukifika Serikali hatutalikataa. Kwa hivi sasa hatujaona ulazima wala haja ya kulazimisha jambo hilo.

Na. 66

Marekebisho ya Alama Barabarani Zinapofutika

Mhe. Ali Salum Haji - Aliuliza:

Kwa kuwa kuna utaratibu wa kuweka alama za barabarani kwa lengo la kusaidia madereva na waenda kwa miguu, lakini inaonekana mara nyingi hizo hufutika na kuchukua muda mrefu wa matengenezo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Na. 66 kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kumjibu naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo.

Mhe. Mwenyekiti, wakati barabara inapokamilika kujengwa huwekewa alama mbali mbali kwa ajili ya kuwasaidia watumia barabara husika kuepusha ajali. Kwa bahati mbaya sana baadhi ya wananchi kwa makusudi huziondoa alama hizo na wengine huzifuta maandishi hayo na alama, na hivyo kupelekea kutokuwepo kwa alama husika au kutoweka maandishi yaliyokusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kuwa barabara nyingi alama zimeondoshwa na kuchunwa herufi au nembo za alama hizo kwa makusudi. Kwa mfano, Mkoa wa Kaskazini Unguja ndiyo unaoongoza kwa kuhujumu alama za barabarani. Ajali nyingi zinazotokea barabarani husababishwa na mwendo wa kasi kwa waendeshaji wa vyombo vya moto. Madereva walio wengi huwa hawafuati maelekezo ya alama zilizowekwa barabarani kwa barabara zenye alama hizo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo sasa naomba nimjibu Mhe. Mjumbe swali lake kama ifuatavyo.

Kwa mujibu wa Sheria za Usalama Barabarani mtu aliyesababisha ajali ikibainika huwa yeye ndiye hupaswa kutiwa hatiani. Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano inatoa wito kwa watumiaji wa barabara hasa kwa madereva na wapanda vyombo vya moto kutoendesha kwa mwendo wa kasi vyombo vyao na kuzingatia alama za usalama barabarani zilizowekwa.

Aidha, Wizara inawaomba wananchi kuwa walinzi wa alama zilizowekwa barabarani na wakimbaini mtu anahujumu alama hizo wasisite kupeleka taarifa kituo chochote cha Polisi au Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara na zawadi itatolewa kwa mtu atakayepelekea kukamatwa kwa muhusika aliyehujumu miundombinu na alama zilizowekwa.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, ahsante pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, mimi nilitaka kumuuliza swali dogo tu la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, swali langu lipo katika suala zima la chaki na hususan katika masuala ya *zebra cross* au alama ya *stop* kama iliyowekwa pale Mwembeladu unaposhuka kilima inamuonesha dereva anayetoka Michenzani kwenda Magomeni anatakiwa asimame ili anayetokea maeneo ya Kariakoo huku Miembeni ndiye yeye apite. Sasa mara nyingi ndiyo zinakuwa zinafutika. Sasa mimi nataka kujua tatizo kufutika mpaka kufika pahala alama zile zikawa hazipo, tatizo ni nini. Tatizo ni ubora wa chaki au rangi inayotiwa au tatizo ni mpangilio wa kuwekwa kila baada ya muda.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kuna namna mbili ambazo zinapelekea alama hizi kufutika. Zipo baadhi ya alama ambazo rangi au *material* iliyotumika haipo katika kiwango stahiki, lakini unapoweka ile alama ya mkando wa moto, ukichoma vizuri kwenye barabara inachukua muda lakini pia lipo tatizo la kutumika muda mrefu bila ya kufanyiwa *repair*.

Sasa sisi kama Wizara tutalichukua hili la kutumika muda mrefu kwa kushirikiana na wenzetu wa Manispaa ili kuona maeneo haya ya mjini, alama hizi zinawekwa kila kipindi bila ya kupita kipindi kirefu ili kuwezesha alama zile ziweze kuonekana kwa ajili ya kuelekeza na kuongoza vizuri matumizi ya barabara zetu.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri napenda na mimi nimuulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa alama za barabarani ni muhimu sana, na kwa kuwa kuna matuta yamejengwa bila ya kutiwa alama hizo hali ambayo inaweza kusababisha ajali baada ya nia nzuri ya kuwekwa matuta hayo kwa ajili ya kupunguza ajali.

Je, Mhe. Naibu Waziri ni lini Serikali itazingatia kuyaweka alama yale matuta ambayo hayajawekewa alama na yale ambayo yamejengwa chini ya kiwango ili yakaweza kupunguza kutokea kwa ajali.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Panya Ali Abdalla kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, utaratibu wa uwekaji wa matuta yale ambayo yamesimamiwa na Wizara yetu, tunahakikisha tunapoweka matuta yanaambatanishwa na alama za barabarani zinazoashiria kwamba umbali usiozidi mita 20 ama mita 50 kuna matuta mbele. Kama matuta ambayo hayakuwekwa na alama, hayo ni makosa na sisi Wizara tutahakikisha kwamba tuna-*rectify* makosa hayo. Lakini kuna watu ambao wameweka matuta kiholela, matuta hayo tutayaondoa na kama kuna matuta ambayo yamewekwa kinyume na taratibu au chini ya viwango, matuta hayo tutayaondoa au tutayarekebisha ili kuona kwamba uwekaji wa matuta iwe ni hatua ya mwisho katika usalama wa barabarani kwa kulazimisha watu kupunguza mwendo, isiwe uwekaji wa matuta kwamba chanzo na kuchochea ajali.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na kwa ruhusa yako naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa miongoni mwa alama muhimu sana ya barabarani ni yale maeneo yaliyowekwa *zebra cross,* na kwa kuwa madereva wengi hawaziheshimu zile alama mpaka sasa hivi wananchi hawajiamini kupita pale barabarani.

Je, Wizara yake ina mpango gani wa kunasihi au kuwaelimisha hawa madereva ili wawe wanaziheshimu zile alama za barabarani ili kuwaondolea wananchi usumbufu na ile hofu waliyonayo ikiwa wakikata barabara dereva yule atakuja tu bila ya kusimama.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kutokuheshimu sheria za usalama barabarani, likiwemo suala la kuvuka kwenye alama za *zebra cross,* sisi Wizara hatupaswi kumbembeleza wala kumuelimisha. Utaratibu uliopo wazi kwamba dereva ambaye amehitamu anapaswa azijue sheria hizo. Kwa hivyo kama kutakuwa kuna dereva ambaye haheshimu alama za barabarani, wenzetu wa Jeshi la Polisi wanapaswa kumkamata na kumfikisha katika vyombo vya sheria ili haki iweze kutendeka, hatutovumilia kwa kumuona dereva mzembe anayesababisha majanga ama maafa kwa wananchi wetu kwa upambavu au uzembe wake binafsi. Tunaomba sana wenzetu wa Jeshi la Polisi wasimamie jambo hili ili kuepusha ajali zinazoweza kuepukika.

Na.91

Utaratibu wa kuingia Hospitali ya Mnazi Mmoja

Mhe. Ali Salum Haji - Aliuliza:

Kutokana na tatizo la kuingia Hospitali bila ya kufuata utaratibu wa wakati maalum wa kutazama wagonjwa na kupelekea usumbufu baina ya walinzi na raia, wenzetu Muhimbili wameamua kuweka milango inayotumia kadi maalum za milango na wahusika tu ndiyo wanaotumia wakati wote wa kutoa huduma.

Je, ni lini Hospitali ya Mnazi Mmoja watawaweka utaratibu huo ili kuwaweka wagonjwa katika hali ya utulivu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, ahsante. Kwanza naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia sote tukiwa wazima wa afya na tukiwa tumejumuika kwenye masuala yetu ya kawaida ya Baraza la Wawakilishi kama wajibu wetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Na. 91 kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba kutoa maelezo juu ya suala hili na kuhusiana na utaratibu mzima wa kuingia kwa wananchi katika Hospitali Kuu ya Rufaa ya Mnazi Mmoja wakati wa kuangalia au kuwatizama wagonjwa kwa nyakati zilizopangwa. Wakati huo wa kutumia kadi maalum kwa kuangalia wagonjwa Mhe. Mwenyekiti, ulipokuwepo hapo awali ambapo kila mgonjwa mmoja aliwekewa kadi tatu ambazo ziliruhusu jamaa wasiozidi watatu kuingia wodini kwa wakati mmoja kumtazama mgonjwa wao.

Kwa masikitiko makubwa sana Mhe. Mwenyekiti, utaratibu huo ulisita kutokana na kukosa mashirikiano ya moja kwa moja kutoka jamii na kuleta taharuki hapo hospitali. Hata hivyo Mhe. Mwenyekiti, kadi hizo bado zipo katika wodi mbali mbali na hivi karibuni baada ya kutoa elimu ya kutosha kwa wale wanaokuja kuwatazama wagonjwa ili kuepukana na mtafaruku unaoweza kutokea, basi tutaanza tena kuzitumia kadi hizo hivi karibuni.

Tunawaomba Mhe. Mwenyekiti, kupitia kiti chako na Baraza hili Tukufu, tunawaomba wananchi wote kutoa mashirikiano yao na kuzingatia taratibu zitakazopangwa kwa kutumia kadi hizo ili kuondoa msongamano wa wagonjwa pamoja na familia zao ndani ya wodi, pamoja na msongamano baina ya wale wanaokuja kuwatazama wagonjwa na wafanyakazi wa Wizara ya Afya, ili kuepusha msongamano huo nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi nao watusaidie katika hili kwenye kutoa ujumbe kwa wananchi wao kwamba utaratibu huu utapangwa kisheria na waweze kutupa mashirikiano ya kufuata utaratibu huu kwa kuwaelimisha.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri nataka kumuuliza swali dogo tu la nyongeza.

Kwa kuwa utaratibu huu umeanza kuleta matumaini na wananchi wameanza kufuata utaratibu wa Wizara uliowekwa, lakini tunafahamu kwamba wale watu ambao wenye wagonjwa ambao hali zao siyo nzuri huwa karibu ili kusubiri ushirikiano wa madaktari pale panapohitajika vifaa vya wale wagonjwa vinavyohitajika.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, kwamba hivi sasa bado wanaokwenda kuwatazama wagonjwa wamekuwa wanakaa nje ya hospitali na kugaragara katika mavumbi na sehemu ambazo zisizoridhisha kusubiri muda kwenda kuangalia wagonjwa wao.

Mhe. Mwenyekiti, nataka kumuuliza Mhe. Naibu Waziri ni lini lile banda ambalo lilitolewa ahadi na Mhe. Waziri aliyepita ambaye sasa hivi ni Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, na baada ya kipindi kirefu kuwa na mgongano na Mamlaka ya Mji Mkongwe, ni lini banda lile litaanza kujengwa ili kuwaondoshea usumbufu wananchi wetu kugaragara katika maeneo yasiyostahiki kwa kusubiri muda wa kwenda kuangalia wagonjwa wao.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Ali Salum Haji swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Naomba nikiri kwamba kweli hilo tatizo lipo linatukabili hivi sasa, wananchi wanakaa kuanzia pale kwenye *garden* mpaka siku hizi kule Wizara ya Afya kwenye maeneo ya *parking*. Kwa hivyo hivi sasa tunaendelea na utaratibu wa kufanya mawasiliano na wenzetu wa Mji Mkongwe ni *structure* gani ambayo itakubalika kujengwa pale. Bahati nzuri ile ramani imeshafikishwa na nakumbuka iliwasilishwa hapa Barazani na Waziri aliyepita, ramani ile tayari imeshakubalika, sasa hivi utaratibu wa kutafuta fedha ili kujenga siyo banda, sitoita banda lakini ni eneo zuri kama pale wenzetu Hospitali ya Muhimbili walivyoweza kujenga kwa kushirikiana pia na sekta binafsi kama Azam na

wengine ambao wanaoweza maduka yao na kufanya biashara zao pia kwa kuwahudumia wale wanaokuja kuwatazama wagonjwa.

Kwa hivyo, utaratibu huo hivi sasa unaendelea na mara tu tutakapopata hizo fedha basi kazi itaanza mara moja.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

Mhe. Farida Amour Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza, pamoja na majibu mazuri sana ya ufasaha ya Mhe. Naibu Spika, naomba nimuulize swali dogo tu la nyongeza.

Mhe. Naibu Waziri ulikiri kwamba utumiaji wa kadi katika kuangalia wagonjwa unategemea hivi karibuni tu utaendelea tena, na kwa kuwa sehemu moja ya kuwafariji wagonjwa ni kwenda kuwaona pale katika vitanda vyao au maeneo yao waliowekwa, na kwa kuwa msongamano ukiwa mkubwa pia unawaletea usumbufu wale wagonjwa waliopo pale, haipendezi.

Je, ni lini wizara yako itaweka mpango maalum wa ile kadi inayotolewa, wale wanaokwenda pale kupewa muda maalum wa kukaa ili wakirudi wakawapa na wenzao nafasi ya kwenda kumuona mgonjwa huyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Kwanza namshukuru kwa swali lake zuri sana, maana swali hili linagusa hospitali ya rufaa ya Mnazi Mmoja tu, hatuna tatizo hili katika hospitali yoyote nyengine. Nimekwenda Chake Chake, nimekwenda Wete kule, Mkoani na Abdalla Mzee hakuna tatizo kama hili, tatizo hili liko hospitali ya Mnazi Mmoja. Tulichunguza kwa nini tatizo hili lipo Mnazi Mmoja.

Mhe. Mwenyekiti, wakati hospitali ya Mnazi Mmoja inajengwa, ilijengwa kwa kuwahudumia watu 360,000 ndio walikuwa wakaazi wakati huo wa Zanzibar nzima. Hivi sasa Zanzibar ina watu milioni 1.3 na wengi wao wanahudumiwa na hospitali ile ya rufaa ya Mnazi Mmoja. Kwa hivyo, moja kwa moja ule msongamano utatokezea tu.

Sasa jambo ambalo tunatarajia kufanya, kwa kila mgonjwa tutatoa kadi tatu, wale watatu wasipoondoka kwa yule mgonjwa, familia yake nyengine hawatoweza kuingia. Kwa hivyo, ule muda wataweza kujipangia wao wenyewe, kama wale watatu wataganda pale pale watakaa, basi hawa wengine watazuia nafasi zao za kuingia. Lakini watakapotoka wale watatu basi zile kadi watapokezana wanawapa watatu wengine, kwa sababu kwa kila mgonjwa wataruhusiwa watu watatu tu kwa wakati mmoja kuona na wale watakapochelewa kutoka, na muda wa kuwaona wagonjwa umekwisha ama ile kengele imepigwa basi watakuwa wamewakosesha wenzao.

Kwa hivyo, tunatarajia wagonjwa wenyewe pamoja na wale wanaokuja kuwaangalia wagonjwa watapangiana utaratibu huo kifamilia, badala ya sisi pale walinzi wetu kwenda kuwatoa. Sisi walinzi wetu watahusika pale muda unapokwisha wa kuwatazama wagonjwa. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Asaa Othman Hamad: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia fursa hii ya kuuliza swali moja la mwisho dogo la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri amekiri kwamba hospitali ile ya Mnazi Mmoja ilipojengwa ilikuwa inawahudumia watu 360,000 na sasa hivi inawahudumia watu milioni 1.3.

Swali langu ni kwamba hivi kutoa kadi kwa kuwaona wagonjwa ama kuwafariji, hili ni suluhisho sahihi ama bado tutaongeza tatizo la wananchi hawa kuwaona wagonjwa wao.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, kwa hivi sasa hili ndio suluhisho lililokuwepo. Kwa sababu Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja ipo katika programu ya kuongezewa maeneo mengine mbali mbali.

Kwa mfano, sasa hivi *Neurosurgical Unit* imeshaongezwa kuna jengo jipya, hospitali ya Mapinduzi Mpya nayo itafanyiwa ukarabati. Kwa hivyo, kutakuwa kuna *facility* ambazo zitatolewa pale. Kama mtakuwa mnapita eneo la Kiwanda cha Madawa mtaona limezungushiwa mabati, pale panajengwa hospitali naweza kusema ni mpya ya kisasa ambayo itakuwa inatoa huduma kwa watoto na wale wagonjwa wenye matatizo ya figo.

Kwa hivyo, kwa kuongeza maeneo hayo *automatic* ule msongamano utapungua, la kwanza. Lakini njia pekee sasa hivi hata wenzetu India, kwa wale Wawakilishi waliokwenda nchini India kwenda aidha kufanyiwa matibabu au kupata huduma nyengine za kiafya, basi watakuwa wamegundua kwamba wakiingia India kule hospitalini unapewa kadi mbili, wanaita *attendant card*, kule unapewa mbili kwa sababu msongamano wao ni mkubwa zaidi, wao wako bilioni 1.2. Wanatoa kadi mbili ambazo anapewa yule mwenye kutazama mgonjwa au aliyefuatana na mgonjwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwetu sisi hapa kwa sababu ya mila, silka na utamaduni wetu, familia nzima huwa inataka kwenda kumtazama mgonjwa wao na kwenda kumuona kwa pamoja, basi nadhani utaratibu huu ndio pekee uliokuwepo sasa hivi wa kutoa kadi tatu kwa mgonjwa, kwa sababu familia zetu sisi kwa hapa Zanzibar wastani ni watu wanne, kwa hivyo wataweza kupokezana pamoja na zile *extended family*, yaani ndugu wa ndugu ili waweze kumuona mgonjwa wao kwa muda uliopangwa. Utaratibu huu ndio pekee tulionao, kwa sababu tukifanya utaratibu mwengine wowote, aidha utambughudhi mgonjwa ama utawabughudhi familia wanaokuja kumuangalia mgonjwa, au utawaletea matatizo wafanyakazi wetu katika ule muda uliopangwa wa kuwatazama wagonjwa. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Nam. 106

Kuongezeka Kwa Vifo Vya Kinamama

Mhe. Panya Ali Abdalla - Aliuliza:-

Tunaipongeza Serikali kwa juhudi mbali mbali za kuwapatia matibabu wananchi wake na huduma nzuri za mama na mtoto. Kuna taarifa kuwa vifo vya kina mama vimeongezeka. Je, Mhe. Waziri taarifa hii ni sahihi.

(a) Kama ni sahihi ni sababu zipi zilizochangia kuongezeka vifo hivyo.
(b) Kuna mikakati gani iliyopangwa ili kunusuru vifo vya kinamama.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 106 lenye sehemu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

Kwanza Mhe. Mwenyekiti, naomba nikubaliane na Mhe. Bi Panya Ali Abdalla, kwamba vifo vya mama huwa vinapanda vikishuka na nitaeleza sababu. Vifo hivyo huwa vinapanda kutokana na wale kinamama waliokuwa na matatizo ya ujauzito.

Aidha, damu yake kuwa chini yaani HB, ama kuwa na tatizo la kuwa na *pressure* ya juu ya *pressure* ya chini, lakini la tatu kutumia huduma za wale wakunga wa jadi, yaani *TBA, Tradition Back Attendance*. Sasa hapa sisi tunasisitiza sana tuweze kushirikiana na zile imani za kina mama ambao wanawaamini wale wakunga wa jadi. Panapokuwa na tatizo huwa tunasema kwamba kinamama hawa wakunga wa jadi wawe wanashirikiana kwa karibu zaidi na Wizara ya Afya.

Mhe. Mwenyekiti, mwanamke mjamzito anapokuwa na tatizo la kifafa cha mimba ama *pressure*, ama HB kuwa ndogo, anapokwenda kule kwa mkunga wa jadi na pakatokea *complication* yoyote, basi mara nyingi sisi huletewa aidha nusu maiti au maiti kamili na bahati mbaya usajili ule wa nusu maiti au maiti unafanyika ndani ya takwimu zetu za Wizara ya Afya na ndio maana inaonekana ongezeko na punguzo la vifo.

Mhe. Mwenyekiti, nitatoa mfano, hivi karibuni nilibahatika kutembelea Kituo cha Kijini, wanasema ni kituo ambacho ndio *the remote*, kituo kilichokuwa mbali kabisa kwa hapa Zanzibar na kiko chengine cha Micheweni kule Pemba. Sasa Kituo hiki cha Kijini kiko Matemwe, pale pana *orderly* dada mmoja ambaye anaaminiwa sana na jamii ya pale, anaitwa Jamhuri na huyo Jamhuri naweza kusema katika miaka 20 iliyopita hii, alimzalisha kila mtoto pale Matemwe amepita mikononi mwake. Lakini ni *orderly* ambaye alipata *training* ya Wizara ya Afya kuweza kuzalisha vizuri kwa kushirikiana na kituo chake. Kwa sababu sasa hivi tayari ameshaajiriwa ni mfanyakazi wa Wizara ya Afya na anafanya vizuri tu, anafanya sawa sawa na daktari.

Mhe. Mwenyekiti, tuna utaratibu tunaandaa tunafikiria kumzawadia, kwa sababu kazi aliyokuwa anaifanya ni ya kupigiwa mfano wa aina yake, haijapata kutokezea kwa Zanzibar nzima. Sasa hili ni tatizo ambalo linaweza kutatuliwa na sisi wenyewe.

Naomba nimjulishe Mhe. Bi Panya Ali Abdalla kwamba katika mkoa unaoongoza kwa vifo vya kinamama ni Mkoa wa Kaskazini, kwa sababu katika mkoa unaoongoza kwa kuwatumia wakunga wa jadi kwa kuzaa au kuzalisha basi ni Mkoa wa Kaskazini. Ukienda vituo vyote wanakwambia kinamama bado wana imani, aidha Mama mkwe au Mama mzazi wa yule mtoto, anamwambia aah! huyu ndiye aliyemzalisha fulani, huyu ndiye aliyemzalisha fulani na wewe utakwenda huko huko.

Mhe. Mwenyekiti, sasa panapokuwa na *complication* ndogo tu, basi tunaletewa sisi mwanamke ambaye ameshapoteza damu nyingi na bado *bleeding* inaendelea, kama amechanika kiasi kikubwa na fuko la uzazi ambalo bado linaendelea kuvuja damu halijafunga. Kwa hivyo, tunapoletewa sisi inakuwa tuna- *treat* kama *emergence*, hatufanyi tena kama ule utaratibu wa mtu wa kawaida wa kumzalisha na hapo ndipo tatizo linapoanza na ongezeko la takwimu hizo za vifo linakuja.

Sasa naomba Mhe. Mwenyekiti, nitoe hizi takwimu kidogo kwa sababu Mheshimiwa ameuliza swali. Vifo vya uzazi vinaonekana kupanda na kushuka kutokana na misimu ya kuzaa. Katika kila mwaka takwimu hizo zimekuwa kama ifuatavyo.

Mwaka 2011 vifo vya mama 77, vikashuka katika mwaka 2012 vikawa 62, na baadae vikapanda tena mwaka 2013 kufikia vifo 103 na kushuka tena mwaka 2014 kufikia vifo 80. Tunachofanya sisi Wizara ya Afya na tunawaombeni nyinyi Waheshimiwa Wajumbe pia, tujaribu kuwashajihisha wakunga wa jadi waje kwetu tuwape mafunzo, na wanapoona kuna *complications* kwa mwanamke mjamzito, basi mwanamke yule wasimzalishe wao wamrifae. Au kama mama mkwe au mama mzazi atakuwa anataka mtoto wake lazima azalishwe basi waje tunawaruhusu, waje pale vituoni kwenye Vituo vya Afya ambavyo vinazalisha, wafanye kazi pamoja na *staff* wetu katika kumuhudumia yule mzazi. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini hata hivyo naomba nimuulize swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b). Kwa kuwa huduma hii kutokana na umuhimu wake wa kunusuru vifo vya kinamama na watoto. Mhe. Rais Dk. Ali Mohammed Shein alitoa ofa maalum kwa kinamama wajawazito kusamehewa fedha zote zile ambazo zitahusu vifaa vya kujifungulia, ili kinamama waweze kujifungua katika hali ya usalama.

(a) Je, Mhe. Waziri utakubaliana na mimi kwamba tufanye ziara ya makusudi kupita katika hivi vituo vya afya ambavyo kinamama wanajifungulia, ili kwanza kwenda kulihakikisha hilo kama bado ahadi ya Mhe. Rais aliyoitoa inatekelezwa kama alivyoagiza. Lakini (b),

(b) Kwa kuwa mwenyewe umekiri kwamba katika vituo vyetu vya kijijini wapo ma-*orderly* wengine wanafanya kazi vizuri, na hata hawa wakunga wa kienyeji wapo wengine wanafanya kazi vizuri. Je, ni lini Mhe. Naibu Waziri kinamama hawa mtaweza kuwapatia elimu, ili waweze kuwazalisha kinamama katika hali ya usalama.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema juzi na ninaendelea kusisitiza tena na kurudia tena kauli ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohammed Shein aliyosema kwamba huduma za mzazi zote zinatakiwa kutolewa bila ya malipo yoyote. Hilo tunalisimamia, naomba nimuhakikishie kuwa tunalisimamia.

Hivi juzi tu nilifanya ziara tena ya *Maternity* Kuu pale Mnazi Mmoja ambayo ndio inayozalisha watoto wengi kuliko kituo chochote chengine cha hapa Zanzibar, nilikutana na *Chief Maternity Matron*, anaitwa Bi Sanura na yeye alinihakikishia kwamba vifaa vyote na kwa kuona. Alinihakikishia kwa kuona sio kwa maneno, ile mipira wanayoambiwa wapeleke ipo maroli kwa maroli. Huwa inatokezea wakati mwengine inatokea mapungufu kwa kuwa havijafika vile vifaa kwa wakati, huwa inatokezea, lakini panapotokezea mapungufu hayo basi huwa yule mgonjwa aidha anaombwa akatafute mwenyewe, lakini kama hana kunakuwa na *stock* ambayo sisi tunaiweka akiba ya kuwasaidia wale pia waliokuwa hawana uwezo.

Kwa hivyo, bado hawachukui fedha taslimu. Hata hivyo *jik* inayozungumziwa mara nyingi kama *disinfectant*, kuleta *jik*. Zikiwa zimekwisha pale basi wale hawachukui fedha wala hawapokei fedha, huambiwa kinamama waje na *jik* yao wenyewe. Lakini kwa sasa *stock* ipo na wanaendelea kupatiwa vifaa vyote hivyo, na hilo nimethibitishiwa.

Lakini la pili Mhe. Mwenyekiti, mimi nashukuru kwa wazo lake Mhe. Mjumbe, na niko tayari sana, nimefurahi na nampongeza tushirikiane naye. Wazo kama hilo Mhe. Mwenyekiti, wewe pia umekuja nalo, kama Mwenyekiti wa Kamati ya Ustwi wa Jamii, kwamba tufanye ziara kwa pamoja na watendaji wa Wizara ya Afya, ili yale yote yanayozungumzwa humu tuweze sisi wenyewe kujithibitishia. Pale panapokuwa na tatizo tutaweza kuligundua pale pale, na kauli ya Rais inapokuwa haitekelezwi pia tutaliona pale pale. Kwa sababu sisi tunapokwenda yote tunayaona yanakuwa sawa.

Lakini wakati mwengine wananchi wanapokuja kwenu, huwa wengine wanataka na wao muwasaidie, nadhani nimeshaeleweka. Sasa wanapokuja huko kwenu, wanakwambia hiki hakuna mheshimiwa na hiki, na wewe unakuja moja kwa moja unakuja kulileta Barazani. Kumbe yule alikuwa anataka umsaidie jambo jengine pale.

Kwa hivyo, mimi ninachoomba tufanye hii ziara kwa pamoja, tutaandaa utaratibu mzuri, na bahati nzuri Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii ndiye Mwenyekiti wetu wa Baraza pia na leo ndiye aliyekalia kiti, basi tutaandaa utaratibu mzuri wa kwenda hii ziara.

La mwisho kabisa ni elimu kwa hawa wakunga wa jadi. Sisi hatuwadharau na kuna utaratibu maalum wa kitu kama leseni, kwamba huyu mkunga wa jadi anatambuliwa na Wizara ya Afya kupitia sheria. Utaratibu huo upo, mafunzo yanatolewa, kama tunavyofanya kwa watu wa dawa asili, waganga wa kienyeji.

Mhe. Mwenyekiti, hivi karibuni muliona walifungiwa wengi na walitoka kwenye TV wengine wakalalamika sana na wakapiga kelele sana. Lakini kuna bodi pale ya tiba asilia na waganga wa kienyeji wote, hata wale wachuaji wa hii mishipa pia wana vibali vyao ambavyo wanapewa baada ya sisi kuwathibitisha kwamba huyu hatokwanyua mshipa wa mtu. Maana wakati mwengine unaweza kwenda wewe kuchuliwa, kumbe ukaongezewa ulemavu ama ukawa mlemavu kabisa. Kwa hivyo, kwa yale sisi tuna vibali maalum ambavyo tunavitoa na vibali hivyo hupati mpaka kuna mafunzo unapitia. Kwa hivyo, vile vibali na kama leseni zao za kufanyia kazi. Kwa hivyo, hiyo programu ya kinamama hasa hawa wakunga wa jadi inaendelea. Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri yenye ufafanuzi wa kina, naomba niulize swali moja dogo sana la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa idadi ya vifo vya mama na mtoto vinaongezeka pale ambapo akinamama wengi wajawazito kushindwa kujifungulia katika vituo vya afya. Kwa kuwa katika maeneo ya Zanzibar bado kuna *out reach areas*, ambazo akinamama hulazimika kufanya kazi ya kujifungua kwa hao aliowataja Mhe. Naibu Waziri wakunga wa kienyeji, ambapo hata sisi ndiko wazazi wetu walipojifungulia huko.

(a) Mhe. Mwenyekiti, katika hili naomba niulize swali dogo sana la nyongeza. Je, ni lini SMZ itatoa *out reach service* kwa mama wajawazito kwa kuwapelekea *mobile maternity ward* katika maeneo kama yale ya Vitongoji Umangani, sehemu za Kizambarauni Makoongwe, sehemu za Kidundo na sehemu za Mtambwe. Je, ni lini watapeleka *mobile maternity ward. That* is (a).

(b) Kwa kuwa idadi ya madaktari pamoja na ma-*nurse*, uchache wa madaktari pamoja na ma-*nurse*, hupelekea sana akinamama wajawazito kukosa huduma ya afya na hatimaye kupoteza maisha pamoja na watoto wao. Sijui Mhe. Waziri ni madaktari wangapi wanaotakiwa pamoja na ma-*nurse* wangapi kutoa huduma kwa akinamama wajawazito wangapi. Nataka nijue tu kwamba ikiwa tutapata ma-*nurse* kadhaa na madaktari kadhaa, hii idadi ya vifo vya watoto na kinamama itapungua. Ni madaktari wangapi na ma-*nurse* wangapi wanahitajika ili tuweze kupunguza vifo vya mama na watoto, ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, naomba nirekebishe kidogo. Nilisema hivi vifo vya kinamama huwa vinapanda na kushuka kutokana na *season* ya kuzaa, pamoja na huduma zinazotumiwa za wakunga wa jadi panapokuwa na *complicated cases*, lakini vifo vile kwa bahati mbaya sana vinakuwa vinaanzia huko mitaani lakini vinasajiliwa ndani ya Wizara ya Afya baada ya yule mgonjwa kuletwa pale au mzazi kuletwa pale kuwa mahututi, hapo tu naomba nirekebishe. Kwa hivyo sio kwamba vinaongezeka lakini

huwa vinapanda na kushuka kwa takwimu za mwaka huu uliopita 2014 zimeshuka, lakini mwaka 2013 vilipanda, hapo naomba nirekebishe.

La pili Mhe. Mwenyekiti, sisi tayari tuna *home based take care* na *home based visit* manesi wote yaani wale *COs* , *Orderly* pamoja na manesi walokuwa katika vituo vyote vinavyozalisha tayari wanafanya *home based care* wanakwenda nyumbani kuwatembelea wakati wa *clinic* kabla ya *pre natal* na huwa wanaendelea kwenda hata *post natal* kumuangalia mtoto na mama pamoja na afya zao. Hili tayari linafanyika, kwa upande wetu sisi hatukuona bado kuwa na haja ya *mobile units* za kuzalisha na nitaeleza kwa nini.

Hivi sasa Zanzibar ina vituo 142 vyote vya afya kituo chengine kilichokuwa mbali kabisa ni kituo cha pahali panaitwa Kiongwe kule Bubwini mbele mtanisahihisha kama kumbukumbu zangu zitakuwa sio sahihi kwa sababu nilikitembelea kituo hicho, kituo cha Kiongwe kina uwezo wa kuzalisha sasa hivi na tayari sisi Zanzibar tumeshapita hata takwimu za *World Health Ogranization* (*WHO)*. Kwa sababu *WHO* wanasema katika takwimu zao panatakiwa pawe na kituo cha afya chenye uwezo wa kuzalisha si chini ya kilomita tano, sisi tumepita takwimu naweza kusema katika nchi inayoongoza Afrika nzima ni sisi Zanzibar, kwa sababu sisi takwimu zetu kituo kilicho mbali kabisa ndio hicho Kiongwe ambacho kiko kilomita 3.5 kutokana na kituo chengine ambacho kinazalisha au kinatoa huduma za afya ya mama na mtoto.

Kwa hivyo bado haijafikia ile *demand,* kuhitajika kutoa *mobile clinic services,* tayari wafanyakazi wetu wanatoa *home based* wanaita *HBC Home based care* na *HBV home based visits* ambazo zinaendelea kufanywa.

Lakini la mwisho kabisa ninachotaka kusema *PHC* zilizopo zote zina uwezo wa kuzalisha watoto ishirini kwa siku na mpaka sasa hivi wastani wa watoto wanaozalishwa kwa siku ni watoto watatu hadi watano, watu wa Kaskazini au Mkoa wa Kaskazini ndio unaoongoza kwa kuzalisha na kuzaa Zanzibar, naomba niwapongeze kwa kazi hiyo nzuri vituo vyote vya Kaskazini nafikiri na ule ukanda wa bahari na samaki wazuri waliokuweko. Vituo vyote vilivyokuwepo katika Mkoa wa Kaskazini kwa kweli vinatoa huduma na havijawahi kuzidiwa sisi tunaona bado vina upungufu wakati mwengine kwa sababu hukaa wiki nzima wakati mwengine hawajapata hata mtoto mmoja wa kuzalisha.

Nitatoa mfano kituo cha Mahonda kuna kituo cha Donge vyote hivyo vinatoa huduma hizo, sasa bado uwezo waliokuwa nao watoto 20 kwa siku haujafikiwa, hivi sasa *average* ni baina ya watatu mpaka watano. Nashukuru Mwenyekiti.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri amekiri kama tamko hili la Rais la kusamehewa waja wazito vifaa vyote vya kuzalia, na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kuwa amekiri kama inatokea muda ikawa vifaa havipo wakawaambia wenye mgonjwa au wenye mzazi aende akachukue vile vifaa ili waje watumie.

Je, Mhe. Waziri haoni kama kuwaambia hivyo wakanunue vifaa ili vije visaidie itabidi kama lipo pale pale suala la kuwa wanachangia. Je, kwa sababu kama hivyo ndivyo haoni kama kuna haja ya Wizara yake kuweka duka *special* ambalo kuwa watakuwa wanakwenda kulipa bili lakini yule mgonjwa au mzazi akachukuliwa vile vifaa bila ya kulipishwa, maana wakimwambia akanunue itakuwa ni suala lile lile la kuwa wanajihudumia wenyewe, haoni kama ni bora kuweko na taratibu wa kuweka duka, Wizara ikaenda ikalipa bili lakini wakapata vifaa vya mzazi bila ya kulipa chochote.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Kwanza naomba radhi kidogo swali la pili la Mheshimiwa Saleh Nassor Juma nilikuwa sijalijibu, nitaeleza tu kwa ufupi aliuliza madaktari wapo wangapi na manesi wapo wangapi, hivi sasa

Madaktari wote ni jumla yake ni 110 pamoja na wale walioko masomoni, lakini manesi tuna tuko kwenye 440 hapa tuna *surplus* lakini nitakwenda moja kwa moja kwenye vituo vya Afya, kila kituo kinachotoa huduma za mama na mtoto pamoja na kuzalisha kina wastani wa *CO/Nurse* na *Orderly* aidha watatu au wanne wenye uwezo wa kuzalisha watoto 20 kwa siku. Kwa hiyo *average* ni *staff* mmoja kwa watu watano.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti nilikuwa nataka tu Mhe. Naibu Waziri anifahamishe ametaja madaktari 110 hawa ni wale madaktari hasa au mpaka *clinical officers* wamo, nataka wale MD angalau wenye *First MD Degree in medicine* na kuendelea.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Hawa ni madaktari hasa wenye *MD Degree* lakini sio lazima wawe katika Wizara ya afya wana *practice* hao ni pamoja na kina Dkt. Jidawi, Dkt. Jamala ambao wako kwenye *administration* nimetoa takwimu ya jumla ya Madaktari wenye *MD Degree* yaani Degree ya kwanza ya udaktari, si lazima awe anafanya kazi kituoni au hospitalini wengine wako kwenye *administration* na ni wengi hao waliokuweko kwenye *administration* katika kada mbali mbali, kuanzia *zone*, *district* huko ambao wanafanya kazi ya *administration* zaidi kuliko matibabu.

Naomba kuendelea Mhe. Mwenyekiti, kumjibu Mheshimiwa Subeit swali lake hili la nyongeza kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukianza kuweka duka kwa sababu sio kazi yetu kuu kufanya biashara, kazi yetu kuu ni kutoa huduma ya afya, tukianza kuweka maduka haya ya madawa ambayo wale wagonjwa wasipopata kule wakaenda kwenye duka lile itakuwa tunakwenda kinyume na ile sera ya Afro Shirazi *Party* ya kutoa matibabu bila ya malipo, tutakuwa tunakwenda kinyume pia na sera inasimamia Serikali hii ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Sasa naomba nimalize Mhe. Mwenyekiti.

UTARATIBU

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, sikusudii kama Serikali iweke duka lake, nakusudia kwamba kuwe na duka lenye vifa hivyo, Serikali iwe na bili yake ili kuepuka lile neno la kuwa wanalipishwa, kwa sababu wakienda wakichukua vifaa wakitibiwa itakuwa bado Serikali inawalipisha.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, hatuwezi kufanya hivyo kwa sababu wale wote wenye maduka ya madawa wanapitia taratibu zote za kuomba leseni na vibali vya kuuza dawa zile, sasa hatuwezi kusema maduka haya tunayatambua maduka haya hatuyatambui, maduka yote yaliyopo Zanzibar ambayo wanauza dawa ama vifaa vya afya au matibabu ya aina yoyote maduka yale yamepewa vibali maalum kwa ajili ya kufanya kazi hiyo. Na kuna sheria imepitishwa hapa kwamba hata famasi inatakiwa kuwa na *pharmacist* angalau mmoja awepo pale.

Kwa hivyo kwa kusema duka hili tuna-*refer* hili hatu-*refer* kwa wale wote itakuwa sio sahihi. Na la pili Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara ni huria anayetaka kuingia kwenye biashara hiyo ameamua kuingia kwenye biashara hiyo na ni biashara huria, kwa hivyo hatuwezi kuanza kusema kwamba duka hili sisi Wizara ya Afya tunalitambua duka hili hatulitambui ni mgonjwa mwenyewe anaamua pale ambapo kifaa kile ama dawa zile hazipo hospitali , kwa sababu *special drugs* sisi ni jukumu letu tunahakikisha madawa yote muhimu yanaletwa na yapo pale wakati wote. Lakini kwa vile vidonge vyengine ambavyo havipo ni mgonjwa anaamua mwenyewe wapi pa kwenda. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Nam. 48

Utafiti wa Kupata Mbegu Zinazoendana na Hali ya Hewa

(Mheshimiwa Mjumbe aliyeuliza swali hili aliliondoa)

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Zanzibar ya Mwaka 2014

(Kusomwa kwa mara ya Pili)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea lakini kabla ya kuendelea majadiliano hayo nataka muiangalie Ibara ya 59 ya Kanuni zetu.

Ibara 59(i) Kila Mjumbe atalisema lile jambo ambalo liko katika mjadala tu na hatarudia rudia kwa namna yoyote ile maneno yake au yale yaliyokwisha kusemwa na Wajumbe wengine.

Ibara ya 84(10) Mjadala wakati wa Mswada kusomwa kwa mara ya pili utahusu ubora na misingi ya mswada huo tu, lakini Mjumbe yeyote anaweza wakati wa mjadala huo kumuomba Waziri au Mjumbe anayehusika afanye mabadiliko katika Mswada huo ambao ataainisha.

Waheshimiwa Wajumbe katika mjadala wa jana tumetoka nje ya mstari, kanuni yetu inatueleza wazi namna ya mijadala yetu inavyotakiwa kuendeshwa, sasa ningeomba sana wale ambao wataendelea kwa michango ya mswada huu, tunapokwenda nje ya mswada huu tunajikuta kwamba hatuufanyii kazi huu mswada badala yake tunazungumzia mambo ambayo hata Waziri atashindwa kuyajibu. Sasa ningeomba Waheshimiwa Wajumbe twende kwenye Mswada kuna mifano ambayo inaweza kutolewa lakini tusikiuke kanuni ambazo tumezitunga wenyewe.

Nakumbuka mchangiaji wa mwisho ambaye alikuwa hajapata dakika zake zote ni Mheshimiwa Hija Hassan Hija, kwa hivyo nitakupa dakika nyengine kumi kumalizia, dakika kumi na tano jana ulitumia. Mheshimiwa Hija karibu.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na nazingatia sana muongozo wako wa kanuni na nakuomba uturuhusu kutoa mifano pale ambapo inahitajika ili sheria hii iwe nzuri.

Kwanza kabla ya kuendelea mchango wa leo nioneshe kwamba viongozi wetu wengi na sisi wenyewe wengi hatuheshimu maadili ya kazi, jana nilipoondoka hapa usiku nilipigiwa simu na yule ambaye jana nilimtaja hapa kwamba amechukua kule Mwambe, ninachoomba kusema kwamba mtu ajibu hoja ikiwa hoja ya uongo basi nafasi ya utaratibu wa kanuni na Sheria upo basi aweze kuchukua fursa ya kujibu hoja kwa mujibu wa sheria.

Habari ya kutoka hapa tukapigiana masimu huko mitaani ikiwa mtu amekaa na mkewe au mumewe haifai, kwa hivyo naomba mtu ajibu hoja, ikiwa ameongopewa basi ajibu hoja, lakini mimi kama Mwakilishi wa Kiwani na nimeajiriwa na watu wa Kiwani nitaendelea kusimamia uadilifu na haki kwa wananchi wa Jimbo la Kiwani.

Mhe. Mwenyekiti, nilifikia jana kifungu cha 16 (1)g naomba niende kifungu cha 16(2) naomba ninukuu "Waziri atakuwa na uwezo wa kuongeza au kupunguza juu ya mali zinazopaswa kutangazwa". Mhe. Mwenyekiti namshauri Mhe. Waziri kwamba neno kupunguza liondoshwe na badala yake lisomeke kama ifuatavyo.

"Waziri atakuwa na uwezo wa kubakisha au kuongeza juu ya mali zinazopaswa kutangazwa". Yaani haya ambayo sasa yameandikwa tusiyapunguze badala yake tuyabakishe ama tuongeze kwa yale ambayo yanahitajika kusimamiwa na mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 18 kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii kiongozi wa umma anatakiwa kuzingatia miiko ya kijamii na kujibu sheria zifuatazo.

Kifungu cha (i) kimesema ulevi wa kupindukia, naendelea kusisitiza kwamba neno kupindukia liondoke na badala yake kubakie ulevi ili ulevi uwe ulevi tu, jana nilisema hapa kwamba wengine hulewa chupa moja wengine chupa tano wengine mpaka ishirini, sasa ni yupi aliyepindukia, kwa hivyo ningeshauri kwamba kupindukia liondoke libakie ulevi kwa maana ya ulevi.

Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia mswada huu kifungu cha 18 kuna mambo yametajwa kutoka moja mpaka kumi na moja, na Mswada huu umzungumzia mambo mengi yakiwemo wizi, uongo na dharau naomba tuongeze maneno haya matatu ya wizi, uongo na dharau ili kuweza kusimamia vizuri mswada huu, nasema dharau kwa sababu Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi tumekuwa tukimsikia Mheshimiwa Rais akitamka maelekezo kwa mujibu wa sheria lakini bado watendaji wa Serikali wamekuwa na dharau hawatekelezi. Kwa hivyo mimi binafsi huona kwamba tamko la Rais ni amri, sasa ikitokezea mtendaji anakaidi tu tamko la Rais nadhani mswada huu pia uangalie dharau ili kama kiongozi ataagiza, Waziri ataagiza au Rais ataagiza au Makao Makuu yataagiza, basi tamko hili liwe ni tamko la kiongozi lazima lilindwe kwa mujibu wa sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti kifungu chengine ambacho nataka nikichangie ni kifungu cha 18(3) kuhusu kiongozi wa umma anatakiwa kuepuka kauli za ubaguzi. Mimi naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kweli wale waliozoea kubaguliwa watapumua, wananchi wengi wamekuwa wakibaguliwa kwa misingi ya Upemba na Unguja, wamekuwa wakibaguliwa kwa misingi ya rangi zao, wamekuwa wakibaguliwa kwa misingi ya dini zao. Sasa sisi ambao tumezoea kubaguliwa nadhani kwa sheria hii itatupa fursa kubwa ya kujitetea na kuweza kulalamika mbele ya Tume ili suala hili la ubaguzi liweze kukomeshwa.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine kifungu cha 19(1) kwa masharti ya sheria hii Rais anaweza kuchukua hatua zinazoleta mabadiliko katika maadili. Mimi naomba heshima kubwa nimpe Mhe. Waziri neno anaweza liondoke na badala yake liwe Rais atachukua, ili kuweza Mhe. Rais kumpa nguvu zaidi kwamba achukue kwa sababu anaweza ni ridhaa yake anaweza akaacha na anaweza akatenda. Sasa ili kulinda maadili ya viongozi wa umma hili neno anaweza tuliondoshe na badala yake libakie kuchukua.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu kingine ni kifungu cha 31 na 32 adhabu iliyowekwa ni kubwa zaidi kuliko 32 nashauri kwamba 31 adhabu yake ilingane au iwe kubwa zaidi kuliko 32, kwa sababu 32 inamzungumzia mtu ambaye atadanganya ile mali aliyonayo sasa hiyo kudanganya adhabu yake imekuwa ndogo zaidi kuliko ile ya kumzuia afisa kufanya kazi yake, sasa nashauri adhabu 32 basi tuongeze ukubwa wake ili itofautiane na ile adhabu ya 31.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 39 kinga ya jumla. Mheshimiwa Waziri nakuomba hii uiangalie vizuri kwa sababu imesema juu ya Mwenyekiti au Afisi ya Tume kwamba inaweza kuwa na kinga kama atakataa kufanya jambo, kuna jambo nadhani kwa kibinadamu tuiweke vizuri ili tusije tukawafanya viongozi wetu hawa na watendaji wetu wakubwa waka-*delay* na wakajisahau.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu mswada huu umezungumzia masuala mazima ya matumizi ya ofisi na mimi naomba niseme tu kwamba kwa kweli mfano ambao nautoa Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri awe makini inakuwa kuwaje Serikali imetumia fedha za umma imeandikisha wananchi kwa kadi za uraia yaani ID imetumia fedha za umma, imetumia muda na imetumia asasi nyengine za serikali lakini kwa makusudi matumizi mabaya ya ofisi yanakiuka utaratibu wa sheria. Nimefanya utafiti jimboni kwangu na ninazo nyaraka za kopi za

vipande vya Zan ID karibu mia tatu (300), mumeandikisha wenyewe wala hamkulazimishwa, mmechambua, mmebagua hawa wanafaa, hawa hafai, hawa mliosema wanafaa mmewapa wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, lakini tangu mwaka 2013 mwezi wa 4 mnawapiga danadana mnasema kwamba Ofisi haina wino, ofisi haina nini. Hizi ni kopi ambazo mmezifanya wenyewe. Sasa wale ambao hamuwataki tayari mmewabagua, lakini wale mliosema wenyewe kwamba wana sifa mnashindwa kuwapa. Kwa hivyo kuna ushahidi kwamba serikali inatumia, viongozi wetu wanatumia Ofisi kwa maslahi yao binafsi. Mhe. Waziri hili naomba uliweke sawa na mswada huu sasa uwe ni chanzo cha kuweka haki kwa wananchi kwa yale mambo ya sheria yanakabiliana nayo.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 41, "Waziri anaweza kutunga Kanuni". Naomba neno anaweza liondoke nahisi mimi iandikwe kwamba "Waziri atatunga Kanuni". Kwa sababu ukisema anaweza ...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hija Hassan Hija, naomba hivyo vielelezo ambavyo umevionesha baadae umpe muhudumu aviwasilishe kwangu.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana na naomba hata sasa aje achukue.

Mhe. Mwenyekiti: Pamoja na vya jana ambavyo umetoa maelezo yake.

Mhe. Hija Hassan Hija: Lakini naomba Mwenyekiti, kwa heshima yako kwa sababu ni ushahidi naomba atoe kopi halafu anipe mwenyewe au nitoe kopi halafu nimpe.

Mhe. Mwenyekiti: Watafanya hiyo kazi wahudumu.

Mhe. Hija Hassan Hija: Naomba muhudumu utoe kopi unipe mwenyewe baadae.

Mhe. Mwenyekiti: Endelea.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, naomba kifungu 41, Waziri neno "anaweza" basi liondoke na iwe atatunga. Kwa sababu sheria hii ili iende vizuri basi lazima iwe na Kanuni. Kwa hivyo neno "anaweza" liondoke na badala yake liwe "atatunga".

Mhe. Mwenyekiti, ushahidi mwengine ni kwamba mnatumia Ofisi vibaya. Mwezi wa Januari na Machi, mwaka 2014, Baraza hili liliunda Kamati Maalum ya kuchunguza kadhia ya wananchi wa Nyanjale Kiomba Mvua, dhidi ya Muwekezaji wa mchezo wa gofu.

Kamati hii Mwenyekiti, mkaipa fedha na mimi nilikuwemo, mlitulipa na tukafanya kazi. Hadi hii leo ripoti haijaletwa ndani ya Baraza hili lakini tayari mmetoa maamuzi kupitia serikali na barua hii hapa.

Mhe. Mwenyekiti, haya ni maadili mabovu sana, kwamba Muhimili wa Dola unafanya kazi, kazi haijamalizika mnatoa maamuzi nje ya utaratibu wa sheria. Viongozi hawa ambao wanakiuka utaratibu wa Mihimili ya Dola nadhani wachukuliwe hatua kabla ya Sheria hii kuwa tayari. Baraza limeunda Kamati na Kamati imekwenda na maamuzi bado hayajaletwa, baadae yanatokezea watu wanachukua hatua nje ya utaratibu wa Dola. Kwa kweli inasikitisha. Mswada huu kwa kweli utalinda hadhi ya Muhimili ya Dola kwa maana ya Mahakama, Baraza la Wawakilishi na Serikali. Haiwezekani kwamba watu wanatumia madaraka yao kinyume na utaratibu ambao hauelekezi sheria.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelekezo hayo naomba niseme hoja yangu ya mwisho naomba nirejee kwenye kifungu cha 1 nitoe wasi wasi wangu Mhe. Waziri unisaidie. Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Zanzibar ya Mwaka 2014 na itaanza kutumika katika tarehe ambayo Waziri atatangaza katika Gazeti Rasmi la Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, jana nilisema kwamba nchi hii tayari imetafunwa sana. Watu wengi ambao sio waaminifu wamejilimbikizia mali nje ya utaratibu wa sheria. Sasa sheria hii ikitumika kuanzia sasa maana yake nini. Maana yake kwamba tunapiga mstari mwekundu kwamba yale ya nyuma yote ambayo watu wameipora serikali basi

yanasamehewa. Na nadhani Mhe. Waziri sisemi kwamba tufufue makaburi, lakini lazima yale ya nyuma ambayo ni makubwa yametia hasara serikali na umma, lazima yatafutwe yaoneshwe na ikiwezekana yarejeshwe serikalini.

Mhe. Mwenyekiti, hatuoni kwamba nchi hii watu wajinufaishe kinyume cha sheria halafu tukasema kwamba tuwasamehe halafu tuanze ukurasa mpya, hapana. Yale ya kibinaadamu lazima tutayasamehe lakini yale ya makusudi hasa ya kuhujumu uchumi lazima yasimamiwe na yarejee serikalini. Tukifanya hivyo serikali hii itakuwa na uwezo na wananchi watajenga imani juu ya serikali yao.

Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri akinipa ufafanuzi wa hoja muhimu nitaunga mkono Mswada huu, nakushukuru.

Mhe. Mwenyekiti: Nakushukuru sana Mhe. Hija Hassan Hija, naomba tu hizo *documents* ulizokuwa ukizitolea mifano uwapatie wahudumu waende wakatoleshe *photocopy* na ziwasilishwe hapa mezani. Mchangiaji anayefuata ni Mhe. Ismail Jussa baada ya hapo ni Mhe. Fatma Mbarouk Said. Ajitayarishe Mhe. Asaa Othman Hamad.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu (S.W) kwa kutujaalia kuamka tukiwa hai na wazima na tukaendelea na shughuli zetu hapa katika chombo hiki cha wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, pili nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia Mswada huu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Kuanzisha Tume ya Maadili ya Viongozi na Mambo Yanayohusiana na Hayo.

Mhe. Mwenyekiti, jana alipokuwa akitoa maoni yake binafsi Mwenyekiti wa Kamati ya Baraza lako inayosimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Mhe. Hamza Hassan Juma, alikuomba kwamba kwa uzito wa Mswada huu basi uwape Wajumbe wa Baraza hili nafasi pana ya kuchangia ili kuhakikisha kwamba sheria itakayotokana na Mswada huu itakuwa nzuri na ambayo kwa kadiri ya uwezo wa kibinaadamu tujitahidi kwamba isiwe na mapungufu ambayo yanaweza kuja kuleta athari hapo baadae. Kwa hivyo nadhani Mhe. Mwenyekiti, utalizingatia hilo na mimi nikuombe utupe nafasi Wajumbe tuchangie vya kutosha kwa sababu mswada huu ni muhimu sana.

Mhe. Mwenyekiti, Baraza hili kwa hakika jana na leo linaandika historia katika Zanzibar kwa kujadili Mswada huu. Kwa kuiangalia historia ya Zanzibar na misukosuko iliyopitia si rahisi mtu kudhani kwamba tungefika pahala serikali yenyewe ikaleta Mswada kama huu. Kwa hivyo katika hili mimi naipongeza sana serikali kwa hatua ya kuleta Mswada huu yenyewe bila ya shindikizo la mtu yeyote.

Mhe. Mwenyekiti, suala la maadili kwa viongozi ni suala la msingi sana. Nadhani mara nyingi tunapenda kunukuu wanafalsafa, wanasiasa na viongozi wa nje hasa wa nchi za Kimagharibi, lakini nadhani tusende mbali sana katika hili Mheshimiwa mfano karibu upo kwa mbora wa viumbe Mtume wetu Muhammad (SAW), huyu ni Kiongozi wetu Waislamu. Moja katika mambo aliyoyasisitiza sana ni maadili kwa viongozi. Hata ukisoma khutuba yake ya mwisho ya kuaga alisisitiza sana juu ya dhamana ya viongozi kwa wanaowaongoza kwamba hii ni amana kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Ndio maana tunaposomeshwa historia ya Uislamu tunatajiwa visa vingi sana, vya kiasi gani kwamba kiongozi wetu huyu alifanikiwa kuwafanya watu pamoja na wale waliokuwa wakimchukia wakasilimu kwa sababu tu ya kuongoza kwa mifano na maadili mema.

Mhe. Mwenyekiti, nasema hili ni jambo zuri tunalolijadili leo. Maadili Mhe. Mwenyekiti hasa kwa viongozi ni jambo la msingi, kwa sababu viongozi wanapewa madaraka. Madaraka yana kawaida ya kufisidi *Lord Acton* moja katika Majaji wanaoheshimika sana Uingereza alisema, "*power corrupts and absolute power corrupts absolutely"*. Madaraka hufisidi na madaraka yasiyo na kikomo hufisidi bila ya ukomo. Kwa hivyo kuwa na Sheria hii kaweka ukomo katika masuala ya uongozi ni jambo zuri sana.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile moja katika maraisi mashuhuri sana Marekani Abraham Lincoln alisema naomba nimnukuu kuhusiana na madaraka: "*nearly all men can stand adversity, but if you want to test man's character, give him power"*. Kwa maana binaadamu yeyote anaweza kukabiliana na akasimama kwenye ushindani, lakini ukitaka kujua tabia, mwenendo wa binaadamu mpe madaraka.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, nafurahi kwamba leo tunajadili kitu kama hichi kwa sababu kinatuwekea vikomo, vizingiti fulani katika utekelezaji wa madaraka ambayo tumepewa. Kama walivyosema waliochangia jana niseme

nafurahi kwamba leo tunajadili Mswada ambao unatuhusu viongozi, maana mara nyingi tunaleta Miswada ambayo utaikuta imeelekezwa kwa wananchi na sio niseme wananchi, lakini mara nyingi kwa sababu ya kuwa hatuna misingi ya maadili kama hii, huwa tunatafuta njia za kukwepa sheria kama zile. Mifano imetolewa mingi sana jana. Kwa hivyo nafurahi kwamba sheria hii inatuhusu sisi Viongozi.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi kabla ya kuingia katika maudhui ya Mswada, niseme kwamba niulize kama walivyouliza wenzangu. Lakini kwanza nitangulie kusema kwamba mimi nauunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja. Na mimi nasema wenzangu najua wamesema kwa uchungu sana kwamba wengine wameupinga kwa sababu ya kusema kwamba hatupo tayari. Mimi nasema inawezekana kwamba tuna machungu mengi kutokana na sheria zetu kutoheshimiwa na ubaguzi na mifano mingi imetolewa tangu jana na kukiuka maadili, lakini ninachosema isiwe sababu ya kuukataa Mswada huu, Mswada huu ni mzuri na unajenga misingi mizuri sana katika nchi yetu.

Mimi katika hili nasema Mhe. Waziri Dokta Mwinyihaji Makame amepata heshimiwa ya kuja kuwasilisha Mswada huu na naomba heshima hii aitunze. Kwa sababu kiongozi mzuri anapimwa pia anapotembea juu ya maneno yake. Tusiwe tunaweka historia za kuanzisha Miswada kama hii halafu vitendo vyetu haviambatani na maneno yetu.

Mhe. Mwenyekiti, lakini nataka nimtahadharishe na kuuliza kwamba tuko tayari? Wenzetu upande wa Tanganyika jirani zetu, wanayo Sheria kama hii. Kwa jinsi vyombo vyao vilivyokuwa vinasonga mbele katika kusimamia uwajibikaji, tumeshuhudia mara kadhaa Bunge likiwajibisha serikali.

Mhe. Mwenyekiti, karibuni kulikuwa na mjadala mzito kuhusiana na suala la kashfa ya *Tegeta Escrow Account,* pamoja na maneno mengi yaliyotolewa na viongozi wakubwa akiwemo Mhe. Rais Kikwete, kusema kwamba hakuna ukiukwaji hapa akaeleza maelezo mengi, lakini hatimaye matakwa ya wananchi kupitia kwa Wawakilishi wao Wabunge yamesimama.

Mhe. Mwenyekiti, lakini si hayo tu, jana gazeti la serikali la Habari Leo la Serikali ya Jamhuri ya Muungano, limeandika "Chenge, Tibaijuka kuwekwa kiti moto, ni katika Tume ya Maadili ya Viongozi, ni miongoni mwa watuhumiwa tisa wa Escrow, pia wamo Ngeleja, Majaji watatu na Katibu Mkuu". Hoja yangu ni kwamba huu Mswada tunaoujadili leo tukiupitisha tunaelekea huko. Kwa hiyo ndio maana nikasema tujitayarishe na ndio nikauliza hilo swali kwamba tuko tayari?

Mhe. Mwenyekiti, kama sio matukio yaliyotokea Dar-es-Salaam juzi ya kudhalilishwa Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Wananchi CUF, Profesa Lipumba, ilikuwa jana Kamati ya Kusimamia Hesabu za Serikali ya Bunge la Jamhuri ya Muungano (PAC) iwasilishe ripoti yake, lakini Mwenyekiti wake akakataa kusoma ripoti kwa sababu ya kutoridhika na hatua zilizofanyika.

Lakini yaliyokuwemo yaliripotiwa katika Gazeti la Mwananchi la juzi Jumanne tarehe 27 Januari, 2015 lilisema "Ufisadi Mpya Kutikisa Bunge, PAC kusoma ripoti ya kashfa tatu kubwa kesho Dodoma, Jengo la Watu Mashuhuri Uwanja wa Ndege ni balaa, Misamaha ya Kodi, Nyumba ya Mbunge Kutawala Vikao". Sasa Mheshimiwa nimeona niyataje haya kwa mifano kwa kusema kwamba tunapojadili na hatimaye tukaupitisha Mswada huo tunaelekea huko. Mhe. Mwenyekiti maana yake nini? Maana yake ni kwamba tujiandae.

Mhe. Mwenyekiti, hapa Zanzibar haya yaliyoripotiwa katika magazeti ambayo yalikuwa yajadiliwe na yawasilishwe katika Bunge la Jamhuri ya Muungano, Zanzibar yaliibuka hapa. Tumeshuhudia wingi wa kashfa katika Baraza hili hili, hasa Baraza hili katika miaka minne iliyopita. Nyengine zimeundiwa Kamati Teule, Kamati teule zimewasilisha ripoti zake hapa, lakini mpaka leo ukitizama nini hatua za maana zimefanywa au zimetekelezwa kutokana na ripoti za Kamati Teule Mheshimiwa inatia uchungu sana.

Mhe. Mwenyekiti, kama kuna mfano hai wa ukiukwaji mkubwa wa maadili kutumia nafasi zetu kujitajirisha, imeoneshwa katika ripoti ya Ardhi chini ya Kamati Teule iliyoongozwa na Mhe. Ali Mzee Ali. Tunajiuliza mpaka leo Serikali imefanya nini? Hakuna jawabu lolote mbele ya Baraza la Wawakilishi, hakuna ripoti yoyote mbele ya Baraza la Wawakilishi kuonesha utekelezaji wa ripoti ile. Kwa hivyo nasema viongozi wengi wametajwa mle. Sasa najiuliza tunapoleta Mswada huu tupo tayari, narejea tena swali lile lile, tuko tayari?

Mhe. Mwenyekiti, jana Mhe. Hamza alinifurahisha kwa mengi, moja alisema kwamba wananchi wa Zanzibar wa leo sio wananchi wa Zanzibar wa miaka mitano, kumi, au ishirini au hamsini iliyopita. Dunia inabadilika kwa kasi, njia za mawasiliano zimeendelea sana. Watu wanapeana taarifa kwa mwendo kuliko wa umeme. Linatokea tukio sasa hivi utafungua simu yako utapata taarifa ndani yake. Kwa hivyo watu wanayajua mengi, wanatujua kuliko tunavyojijua. Sasa ninachosema kwamba tunapoyatizama haya na sisi wenyewe tujitizame tuko tayari?

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba sasa niende katika Mswada. Mhe. Mwenyekiti, yapo mengi katika Mswada huu na hata kama ningeamua kutumia dakika zangu zote kuuchambua nina hakika nisingeyamaliza. Kwa hivyo naweza kutumia utaratibu baadaye wa kuwasilisha baadhi ya mambo kwa maandishi, lakini kuna baadhi ya maeneo ambayo ningeomba niyagusie hapa.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nilikuwa nataka nitahadharishe jambo moja la jumla hilo. Miswada yetu inajadiliwa kwa Kiswahili hapa, lakini tunaletewa na Miswada ya Kiingereza na unaokwenda kukaa katika vitabu vya Sheria za nchi kwa maana *statue books* ni ule wa Kiingereza. Sasa nimwambie tu Mhe. Waziri, Mswada wa Kiswahili una majadweli mengi, lakini Mswada wa Kiingereza una majadweli mawili.
Kuna jadweli la kwanza ambalo linaelezea ile misingi ya maadili na baadaye kuna jadweli la pili ambalo lina orodha ya viongozi. Zile fomu nyengine zote zile haziko katika lugha ya Kiingereza kama ambavyo ziko katika lugha ya Kiswahili, hizi baadaye ndizo zinakwenda kukaa katika sheria.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, hili nikuombe mapema kabisa yeyote ikiwa wewe mwenyewe au atakayekaa katika kiti hicho, wakati wa kupitisha vifungu nadhani itakuwa si haki kwa Mswada huu namna ulivyo ikiwa tutachukuliwa kwamba tunapitisha vile vifungu vya mwanzo tu na majadweli yatachukuliwa kuwa yamepitishwa kwa sababu yametajwa ndani ya kifungu fulani cha Mswada.

Nadhani kwa uzito wa majadweli yale hasa ya jadueli la kwanza ambalo ndio linaloweka ile misingi ya maadili, tukishalipitisha kijumla jumla tu pengine utawanyima wajumbe wa Baraza hili fursa ya kutoa mawazo katika vifungu mbali mbali. Kwa hivyo nadhani Baraza lifikirie utaratibu gani wa kusaidia katika mjadala ili tupate kupitia kwa kina.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, niende katika vifungu na naomba nianze na suala la kwanza kabisa ambalo linahusu kifungu cha 4. Kifungu cha 4 Mhe. Mwenyekiti, kinaanzisha Tume, Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma Zanzibar ambayo inatajwa kwamba itakuwa ni wakala wa Serikali. Hoja yangu katika kifungu hiki Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba Tume hii ukiangalia kifungu cha 12(1)(g) na (h) na ukiangalia kifungu cha 26 na kifungu cha 27 vinaweka utaratibu ambao unakifanya chombo hiki kuwa ni kama *first judicial*. Kwa maana kwamba kimepewa madaraka ya kusikiliza malalamiko na tuhuma na baadae kutoa maamuzi.

Sasa tatizo nililoliona katika mswada Mhe. Mwenyekiti, na ningemuomba Mhe. Waziri katika hili akubali tufanye marekebisho, ni kwamba mswada hautoi fursa kwa mlalamikiwa baada ya kutolewa maamuzi ya Tume kuweza kukata rufaa au kupata kitulizo chengine chochote kama Katiba yetu ya Zanzibar inavyotaka. Mhe. Mwenyekiti, Katiba ya Zanzibar kifungu cha 12(6)(a) kinasema:

"Kwa madhumuni ya kuhakikisha usawa mbele ya sheria serikali itaweka taratibu zinazofaa na zitakazozingatia misingi kwamba;

(a) wakati haki na wajibu wa mtu yoyote vinahitaji kufanyiwa uamuzi wa mahkama au chombo kinginecho kinachohusika, basi mtu huyo atakuwa na haki ya kupewa fursa ya kusikilizwa na pia haki ya kukata rufaa au ya kupata kitulizo kinginecho cha kisheria kutokana na maamuzi ya mahkama au chombo hicho kinginecho kinachohusika".

Naomba Mhe. Mwenyekiti, tujikite katika maneno au chombo hicho chengine kinachohusika. Chombo hiki ni chombo gani kisiokuwa mahkama, ni vyombo kama Tume hii ambayo vimepewa madaraka ya kusikiliza na kuamua juu ya masuala ambayo yanafanana fanana na masuala ya kisheria. Kwa hivyo ukiangalia mswada mzima hautoi nafasi ya mlalamikiwa anapotolewa hukumu na Tume ama kukata rufaa kwa kitu chengine au kupata kitulizo chengine.

Kwa lugha nyengine hakuna *remedy* ya aina yoyote sio *appeal* wala hata *judicial review*. Sasa Mhe. Mwenyekiti, taratibu zetu za Jumuiya ya Madola nyingi zinaonesha kwamba unapounda chombo kama hiki ukakipa madaraka kama haya kwamba ni *quasi-judicial* basi lazima uweke utaratibu wa ama kuwa na *remedy* kupitia rufaa au *judicial review* au utaratibu mwengine wowote ambao utawekwa. Kwa hivyo nilikuwa naomba Mhe. Mwenyekiti, hilo Mhe. Waziri alizingatie na Serikali ikubali kufanya marekebisho kwa kuweka utaratibu huo ambao umetajwa ndani ya Katiba yetu katika kifungu cha 12(6)(a).

La pili Mhe. Mwenyekiti, ni kifungu cha 27(1) cha mswada; hiki kinazungumzia kwamba baada ya Tume kusikiliza madai au malalamiko na ushahidi uliotolewa, Tume itatoa maamuzi ama kiongozi kavunja maadili au hakuvunja na kupeleka taarifa kwa mamlaka inayohusika kwa hatua zaidi. Hii mamlaka inayohusika imetafsiriwa katika tafsiri ya maneno huko mwanzo na inataja mamlaka inayohusika maana yake ni Rais, Spika wa Baraza la Wawakilishi, Jaji Mkuu wa Zanzibar, Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi na taasisi nyengine yoyote ya umma ambayo kiongozi wa umma anawajibika kwayo.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu hapa ni kwamba ukenda katika kifungu cha 30 kumetajwa orodha ya hatua ambazo hii mamlaka inayohusika inaweza kuchukua, nazo ni pamoja na onyo na tahadhari, kushushwa cheo, kusimamishwa kazi, kufukuzwa kazi, kuondolewa madarakani, kushauriwa kustaafu au kukatwa mshahara.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, ambacho kimenisikitisha ni kwamba sheria au mswada haukutoa fursa kwa mlalamikiwa anapopelekwa mbele ya mamlaka inayohusika kupewa nafasi ya kusikilizwa kabla ya kuchukuliwa hatua hizo zilizotajwa katika kifungu cha 30. Sote tunajua kwamba kuna misingi ya haki za kimaumbile, yaani *principle of natural justice* mojawapo ni kwamba huwezi kuhukumiwa kabla kupewa haki ya kusikilizwa.

Sasa Tume yenyewe imetajwa ukisoma katika kifungu cha 6 na 8 kuna sehemu ambayo inazungumzia kwamba mbele ya Tume kutakuwa na haki ya kusikilizwa ni kifungu cha 23(3) Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu cha 23(3) kinasema. "Mwenyekiti baada ya kupokea maelezo kwa maandishi atapanga siku ya kusikiliza malalamiko au madai yaliyowasilishwa kwa kuzingatia haki za asili na haki ya kusikilizwa". Sasa hili limetolewa kwa Tume lakini kwa huyu anayepelekewa mamlaka inayohusika, yeye hakupangiwa utaratibu wa kumsikiliza yule mtu kabla ya kumchukulia hatua. Nilikuwa nadhani na hilo si haki kumchukulia mtu hatua bila ya kwanza kumpa nafasi ya kumsikiliza.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, mimi kidogo nimepata mkanganyiko na naomba Mhe. Waziri akija anisaidie kwamba mswada unaanzisha Tume ya Maadili ya Viongozi, lakini ukivisoma vifungu vyake vile sitaki kukisoma kimoja kimoja. Vifungu vyake vingi mamlaka yote kapewa Mwenyekiti. Sasa najiuliza kwamba anayesikiliza haya malalamiko na kutoa maamuzi ni Tume au ni Mwenyekiti. Kwa sababu Tume ukisoma kifungu cha 5 cha mswada imesema "Tume itamjumuisha Mwenyekiti na Kamishna wawili" na hao Makamishna wawili wametajwa katika kifungu cha 8 kama anateuliwa na Rais lakini baada ya kutajwa kwenye kifungu cha 8 huoni sehemu nyengine yoyote ambapo kazi zao zimetajwa.

Kila pahala palipohusu kazi za Tume mara nyingi katajwa Mwenyekiti, au ikitajwa Tume inaonekana kama vile ni Mwenyekiti na maafisa wake lakini hawa Makamishna wapo wapo tu. Sasa nilitaka kujua kwamba mamlaka tangu ya kupokea, ya kusikiliza na kutoa maamuzi ni ya Tume kwa maana ya Tume na Mwenyekiti na Makamishna wawili au ni ya Tume kwa maana ya Mwenyekiti tu, nilikuwa naomba hiyo tuwekewe wazi. Kwa sababu tutafautishe baina ya Taasisi na Kiongozi mmoja tu wa Taasisi.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, ambalo nataka kusema hili naona umetafuta njia ya kujikinga na mimi silikubali kabisa Mhe. Mwenyekiti, ni kifungu cha 21 ambacho pia kinaonekana kwenye jaduweli lakini kwa sababu ya muda sitokwenda katika jaduweli nitakisema hapa katika vifungu, nitakuja kuchangia mpaka katika jaduweli ikiwa Waziri atakuwa bado hakuridhika na maelezo yangu.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 21 kinasema mtu kupewa zawadi itakuwa si kuvunja maadili na naomba hili lifahamike Mhe. Mwenyekiti, nikisome kinasema:

"Bila ya kuathiri masharti ya kifungu cha 20 haitozingatiwa kwamba kiongozi wa umma amevunja maadili kwa kukubali au kupokea;

(1) maslahi madogo ikiwa ni pamoja na takrima, zawadi za kawaida au zawadi ndogo.

(2) zawadi kutoka kwa rafiki au jamaa wa karibu iwapo kiongozi huyo hayupo katika kutekeleza majukumu yake ya umma.

(3) zawadi kutoka kwa mtu yeyote ama wa ndani au nje ya nchi ikiwa zawadi hiyo ameitolea taarifa kwa Mkuu wake wa kazi pamoja na thamani yake.

(4) uhaulishaji unaotokana na haki ya kumiliki mali kwa kiongozi wa umma unaotokana na mkataba ambao thamani yake kamili ameitangaza na kuwasilisha taarifa kwa Mkuu wake wa kazi au;

(5) kafanya jambo lolote kwa nia njema kwa kadri Tume itakavyojiridhisha".

Sasa Mhe. Mwenyekiti, nasema tukisema hivi naogopa ya *Prof*. Anna Tibaijuka na rafiki yake Rugamalira. Mhe. Mwenyekiti, *Prof.* Tibaijuka katwambia yeye kaingiziwa bilioni 1.6 na swahib yake Rugamalira na hazikuwa na matatizo yoyote, kaombea msaada skuli. Lakini baadae wengi wametilia mashaka suala hilo na kwamba unawezaje kupewa kiongozi wa umma zawadi kubwa kiasi hiki dola milioni moja.

Sasa hapa kwetu sisi hili tumelifunika funika la kupewa zawadi. Lakini Mhe. Mwenyekiti, kuna nchi katika dunia hii na sisi tunafuata mfumo wa Jumuiya ya Madola kwa mfano Uingereza, kiongozi wa umma kawekewa kiwango kuna zawadi ikifika thamani fulani kwa lugha nyengine kwamba *prescribed nominal value* ikifika thamani hiyo anatakiwa aitangaze na aikabidhi serikalini kwamba haiwezi kuwa yake binafsi.

Kinachokimbiwa nini Mwenyekiti hapa, ni mtu kupewa zawadi baadae zawadi ile ikawa ni sababu ya kununua fedha upendeleo fulani katika kufanya maamuzi na nani anaweza kuthitibitisha kwamba zawadi aliyopewa haikukusudiwa hivyo.

Sasa mfano hai upo hapa wa *Prof*. Tibaijuka na rafiki yake Rugamalira, kwa hivyo nasema mimi hili la kwamba tumeliweka hivi siliwafiki na ninamuomba Mhe. Waziri atukubalie kwamba tuliondoshe hili, kwamba zawadi ile ndogo kama ilivyosema pale na pengine katika *shedulle* isemwe thamani, lakini kuna zawadi ikifika kiwango fulani lazima ikabidhiwe na ziko nchi nyingi Mheshimiwa kwamba ukipewa zawadi ikifika thamani fulani si yako tena ni ya nchi, wewe umeipokea kwa sababu ya wadhifa wako si kwa sababu wewe ni Ismail Jussa au wewe ni mtu mwengine yoyote.

Pia Mhe. Mwenyekiti, nadhani 21(5) kimetoa mamlaka makubwa sana, hii kwamba kafanya jambo lolote kwa nia njema kwa kadri Tume itakavyojiridhisha kwamba leo pia si kuvunja maadili. Hii nia njema anae-*determine* nani *good faith,* sheria iko kimya. Kwa hivyo nasema na kijifungu hiki nacho Waziri akitizame tena kwamba kinaonekana kimetoa mamlaka mapana sana.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika kifungu cha 22, hapa ndio nimepata homa kabisa, msingi mzima wa kuleta sheria hii ni kutunza maadili na kuimarisha uajibikaji wa viongozi wa umma kwa wananchi wao. Lakini kifungu cha 22 kinachoanzisha daftari la kumbukumbu za mali la maslahi linatajwa kuwa litakuwa ni la siri. Sasa ninajiuliza mimi kwamba ikiwa lengo ni wananchi kuwatambua viongozi wao ambao wanatakiwa kutaja mali zao, kwa nini daftari liwe la siri na tena utaratibu wake wa kuliona ni mpaka kwa ruhusa ya waziri au amri ya mahkama. Lakini sheria hiyo hiyo au msaada huu haukuweka utaratibu wa huyo Waziri atatoa ruhusa hiyo kwa utaratibu upi, kwa faida ipi, lakini vile vile hata Mahkama yenyewe haikuwekewa utaratibu.

Sasa najiuliza kwamba kama tunagharimika kuanzisha chombo kama hiki na chombo hiki kitakuwa na gharama kubwa sana Mhe. Mwenyekiti, kwa maumbile yake, halafu daftari lenyewe liwe siri, mimi sikiungi mkono, ninamuomba Mhe. Waziri akija hili aliondoe, daftari hili liwe ni *public document*. Kama tumeamua kwamba tunataka kuwajibika kwa wananchi, wananchi waweze kuwa na *access* katika kifungu hiki.

Mhe. Mwenyekiti, naomba pia nichangie kwa ufupi mengine kama nilivyosema naweza kuyaandikia nikayawasilisha kwa Mhe. Waziri kwa sababu ya muda, lakini katika masharti yaliyokuwemo katika jaduweli la kwanza kuna kitu kimenitanza sana, kila pahala humu imetajwa Mahkama maalum na pahala pamoja ikitajwa kama

ni Mahkama maalum ya viongozi. Sasa nilikuwa ninajiuliza hii Mahkama hii ni ipi kwenye mfano kifungu cha 5 cha jaduweli la kwanza, panatajwa Mahkama maalum ya viongozi na mahkama maalum na imerejewa rejewa katika baadhi ya vifungu.

Mimi sikuona pahala popote mahkama hii imeanzishwa wapi na muundo wake ni upi na mimi siwafiki Mheshimiwa kuwa na mahkama maalum. Katika kingereza imetajwa *leadership tribe union* mimi nadhani tuekewe wazi chombo hiki ili tujiridhishe na kama hatujiridhishi Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hili tutakuwa hatuwezi kuliunga mkono kwa sababu linaweka kama kuna hadhi maalum kwa baadhi ya viongozi na wananchi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jussa umebakisha dakika tatu kumaliza.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Nitajitahidi nimalizie Mhe. Mwenyekiti, haya masuala mengine nitayawasilisha kwa maandishi.

La mwisho kabisa Mhe. Mwenyekiti, basi kwa kutumia hizo dakika tatu ambazo umeniambia nnazo, naomba niende katika jaduweli la pili.

Mhe. Mwenyekiti, kuna watu au viongozi ambao nilidhani walipaswa kuorodheshwa katika orodha hii siwaoni hapa. Moja ninajiuliza tumetaja meya, tumetaja Katibu wa Halmashauri za Wilaya lakini madiwani hawatajwi, Mwenyekiti wa Halmashauri hatajwi ambao kihadhi hawa wanafanana, kwa hivyo nilikuwa nadhani hawa waingie.

Zaidi Mhe. Mwenyekiti naomba kwamba katika jaduweli la pili masheha waingizwe. Sheha tumemfanya mtu mkubwa sana katika nchi hii, anapeperusha bendera ya nchi lakini ukenda katika jaduweli la kwanza ambalo linahusu hayo maadili yenyewe mengi yanahusu utoaji huduma kwa wananchi. Na sehemu kubwa ya huduma kwa wananchi katika ngazi waliko wanapewa na masheha. Na tumeona mara nyingi humu masheha kiasi gani wanatumia nafasi zao kujilimbikizia mali na kutumia vibaya madaraka yao.

Masheha wana ardhi, wanajikatia katika maeneo yao, sasa sheria kama hii imetajwa viongozi wengi lakini huyu ambaye ndie anayemuhudumia mwananchi na haya masharti jaduweli la kwanza mengi yanahusu katika utoaji huduma kusiwe na upendeleo, kusiwe na ubadhirifu, kusiwe na rushwa, kusiwe na mtu kuingilia maslahi binafsi na maslahi yake.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nadhani kwamba hayo hayawezi kukubalika kwa hivyo nilikuwa naomba kwamba hawa masheha vile vile nao waongezwe.

Mhe. Mwenyekiti, katika majaduweli haya kuna kifungu kimoja kimenivutia sana na ni imani yangu kwamba ili kuepusha nchi yetu isiingie katika matatizo, basi tutakiheshimu sana nacho ni kifungu cha 3 cha jaduweli la kwanza kimesema:

"Umoja wa Kitaifa, utawala wa sheria na kuheshimu watu wote" nianze kifungu cha pili kinasema:

"Taratibu za kitasisi na za kidemokrasia zinaakisi mazingira ya kitaifa na ya ndani ya nchi hivyo zinapaswa kukuzwa".

Tatu, taratibu za Taasisi hizo ni pamoja na:

a) Kwamba taratibu za kubadilishana madaraka zinapaswa kufanyika kwa amani kupitia uchaguzi ulio huru na wa haki na uwazi;
b) Utawala wa sheria na haki za binaadamu;
c) Uhuru wa Mahkama;
d) Serikali sikivu na yenye kuzingatia haki;
e) Umoja wa Kitaifa na;
f) Haki za raia, maadili, mila na desturi.

Hii inamaanisha kwamba hifadhi yoyote ya kikatiba na taasisi yenye kulinda maslahi na haki za binaadamu na kiraia zinapaswa kuheshimiwa na kutafsiriwa kwa upana zaidi kwa kuzingatia maslahi ya wananchi na mambo mengine kama hayo.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, ninafurahi kwamba haya sasa tunayatambua kama ni maadili ya viongozi na kwa sababu nchi hii mara nyingi imekumbana na misuko suko katika masuala ya uchaguzi, ninaamini kifungu hiki kitatupelekea kwamba sasa tuheshimu maamuzi ya wananchi katika chaguzi na tubadilishane madaraka kwa njia za amani mwaka huu kama ilivyosemwa katika kifungu hiki.

Baada ya kwisha kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, ninashukuru na kama nilivyosema yako ambayo nitawasilisha kwa maandishi na ninafikiria hata katika baadhi ya vifungu nilivyovitolea maoni kuandika *shedulle amendment* ambayo nitaiwasilisha kwa Mhe. Waziri na kupitia Ofisi yako. Ninakushukuru Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema tena naunga mkono mswada huu mia kwa mia.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa hii kuuchangia mswada huu wa kuanzishwa kwa sheria ya maadili ya viongozi wa umma na kuanzishwa Tume ya Maadili ya Viongozi na mambo yanayohusiana na haya.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimepata faraja kidogo kuwasikia wenzangu kwamba mswada huu wameunga mkono na niseme kwamba waliounga mkono wengi ni wazoefu na watungaji wa sheria na niseme ni wanasheria, sijui kama ni wanasheria wadogo au ni wakubwa lakini najua kwamba wanafanya kazi hizo za uanasheria. Kwa sababu ulipowasilishwa mswada huu baadae Mwenyekiti mwenyewe alisema huu mswada ni mgumu sana kwa upande wetu sisi hasa viongozi.

Hii niseme hivyo kutangaza mali inakuwa ni jambo gumu kwa kiongozi, kuheshimu wadhifa alionao, kuacha uasharati, uropokwaji, kwa kweli mimi nilikuwa napata mashaka kwanza kwenye sheria hii kuambiwa kwamba ni ngumu.

Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba mswada huu ni mzuri na wenzangu tuupitishe mswada huu kwa kupitia vifungu. Mhe. Mwenyekiti, leo umewahi mapema sana kutwambia kwamba twende na vifungu, kwa sababu kila mmoja alikuwa na lake labda la kusema kutokana na historia mbali mbali zilizojitokeza, kila mmoja ameathirika kiupande wake.

Mhe. Mwenyekiti, niende na mswada huu kuanzia sehemu ya pili, kifungu cha 7 sifa ya mwenyekiti anasema kwamba: Mtu atakayekuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Mwenyekiti sifa zake ikiwa Mzanzibari na mwenye sifa za kuwa Jaji wa Mahakama Kuu.

Kwenye kifungu hiki nikienda na kifungu cha 37 (1) kinasema kwamba, naona kama kinakinzana na kifungu kile, kinasema kwamba; "Mwenyekiti atatayarisha ripoti ya mwaka kwa kila mwaka wa fedha na kuwasilisha kwa waziri ndani ya kipindi cha miezi mitatu baada ya mwisho wa mwaka wa fedha husika". Lakini huku sifa ya Mwenyekiti ni kwamba awe Mzanzibari, mwenye sifa za kuwa Jaji wa Mahakama Kuu au sijui kama sijafahamu tu, lakini waziri atakapokuja naomba anifahamishe, kwa sababu mambo ya fedha yanataka uwezo wa kihasibu.

Kwa hivyo, hapa naomba Mhe. Waziri atakapokuja katika sifa hizi au pengine kwa kutofahamu kwangu inaweza kuwa ikawa sikufahamu.

Mhe. Mwenyekiti, nikienda ukurasa wa 60 ambao ni sehemu ya tatu ya maadili yatakayotumika kwa kiongozi wa umma.

Kifungu cha 18 kinasema, kuzingatia miiko ya kijamii. Kwa kuzingatia masharti ya sheria hii kiongozi wa umma atatakiwa kuzingatia miiko ya kijamii na kujiepusha na tabia zifuatazo.

Ulevi kupindukia, uasharati, uropokwaji, utoaji wa siri, uzembe na kutojali matatizo ya wananchi, kushindwa kutunza familia na wazee wake, kushirikiana na watu wenye mienendo isiyokubalika, kushindwa kulipa madeni, kutumia kauli na lugha isiyofaa, ugovi, unyanyasi wa kijinsia. Yote haya Mhe. Mwenyekiti kama viongozi tunatakiwa haya ni lazima tusiwe nayo.

Ukimuona kiongozi ni mtoaji wa siri huyo hajakamilika na hana maadili, uzembe na kutojali matatizo ya wananchi vile vile hayo sio maadili, mtu mgomvi ikiwa mtu mgovi ujue anahatarisha maisha ya watu, unyanyasi wa kijinsia vile vile. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti sioni tatizo la sheria hii tukasema kwamba ni ngumu, tukatia yetu lakini haya ndio maadili ya kiongozi yeyote anavyotakiwa.

Mhe. Mwenyekiti, nikienda sehemu hiyo hiyo ya tatu kifungu kidogo cha (2) kiongozi wa umma hatakiwi kujihusisha na vitendo vya jinai ikiwa ni pamoja na utapeli, wizi na ubakaji. Mheshimiwa bado naona hakuna tatizo la sheria hii kwa nini tusiipitishe na mambo yako wazi kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, kuna maandishi ya pembeni, hii inasema Rais kukuza maadili katika ofisi ya umma, kifungu cha 19, kifungu kidogo (1);

"Kwa masharti ya sheria hii, Rais anaweza kuchukua hatua zitakazoleta maadili ili kuweka misingi ya kuimarisha imani ya wananchi juu ya uaminifu wa kiongozi wa umma na taratibu za kutoa maamuzi serikali na katika sekta ya umma jumla"

Mhe. Mwenyekiti, Rais ukisema anaweza akafanya au asifanye, basi ningeomba hapa badala ya anaweza "Rais atachukua hatua zitakazoleta mabadiliko ya maadili ili kwenda kuweka misingi ya kuimarisha imani ya wananchi".

Mhe. Mwenyekiti, tunaendelea na vifungu, kifungu kidogo cha (2) katika kuchukua hatua za kufanya mabadiliko ya maadili kwa mujibu wa sheria hii Rais atazingatia mambo yafuatayo. Kwamba kiongozi wa umma hatojilimbikizia mali kinyume na sheria.

Mhe. Mwenyekiti, nasikitika sana kwamba sheria hii nitasema bado ni nzuri, kama kiongozi atajilimbikizia mali ambazo ni kinyume cha sheria na wala tusiogope waheshimiwa humu ndani, kwani kuna njia nyingi tu za kupatia mali za kihalali, kwa nini tuogope kuzielezea mali zetu. Wala Katibu Mkuu sidhambi kuwa na nini kwa sababu unapokuwa katika dunia tunaambiwa kwamba ujenge dunia yako kama utaishi miaka mingi, lakini vile vile utizame na akhera yako kama utakufa kesho.

Kwa hivyo, haya ni mambo ya msingi kabisa usiogope kutaja mali zako, kwa nini uogope kuna njia chungunzima watu wanachukua mikopo Makatibu na wanao uwezo huo. Kwa nini tuogope kutaja mali zetu Mhe. Mwenyekiti, mimi naona bado tuna uwezo wa kufanya hivyo bila ya woga.

Mhe. Mwenyekiti, nikienda kifungu cha 20 kinasema kwamba, "kiongozi wa umma atachukuliwa kwamba amevunja maadili ikiwa kwa makusudi amefanya yafuatayo.

(a) " Kutumia visivyo au kujinufaisha kutokana na taarifa anazozipata kutokana na utekelezaji wa majukumu yake ambazo hazijatolewa kwa matumizi ya umma".

Huo ni uvunjaji wa maadili. Lakini vile vile kuna kifungu;

(c) "kutumia ushawishi katika uteuzi, upandaji vyeo, kutoa adhabu au kumuondoa kazini mtumishi wa umma".

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli kama ni uvunjaji wa maadili kwa sababu kama kiongozi mimi nina watu ambao nawaongoza tabia zao nazijua, namjua huyu ana tatizo hili, huyu ana tatizo hili, huyu ana sifa hii, yule ana sifa ile. Kwa nini niwe navunja maadili kwamba mimi nikashawishi kuwa fulani aajiriwe, kwa nini nimevunja maadili, kwa nini iwe mimi nimevunja maadili kama ni kiongozi. Naomba Mhe. Waziri tutizame vifungu kama hivi.

(d) "ni dhambi kutumia mali ya serikali kwa matumizi binafsi au matumizi yasiyoidhinishwa kwa njia ya kujipatia maslahi ya kiuchumi".

Mhe. Mwenyekiti, wenzangu wamesema hapa kwenye kifungu hiki cha sehemu ya tano kinasema makosa na adhabu. Mimi nasikitika sana kamati hapa kuna kamati zinaundwa, kuna Kamati Teule, kuna Kamati zetu za kudumu za Baraza, kuna maeneo mengi tunapita na kuona mambo mengi na hasa zile Kamati Teule.

Nasikitika sana kwamba ripoti moja hapa ya Baraza la Manispaa ilikuja na kusomwa mbele ya Baraza lakini bado muhusika mkuu siwezi kusema sana, kwa sababu watu wanasema lako halikutapishi isipokuwa linakueneza moyo, lakini mtu huyu kapanda cheo badala ya kushuka cheo, mimi nasema kwamba kapanda cheo. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti tusione haya tunapozifanya sheria hizi lazima tuzitekeleze. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti sheria hii bado nasema kwamba ni sheria nzuri lazima yale yaliyokuwemo humu basi tuyafanyie kazi na sheria hizi zitumike ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kifungu cha 37 hiki kidogo, hii sifa za Mwenyekiti na kazi zake ambazo anazifanya kidogo na vile vile niseme kama taasisi hii kutakuwa na fedha ambazo zinapitishwa na Baraza hili la Wawakilishi, basi vile vile tusisahau kwamba hesabu hizi zikaguliwe na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, na vile vile kuwe na mahesabu yale kabla ya kuanza mahesabu ya mwaka mwengine. Basi vile vile kupelekwe hesabu zile mpaka tarehe 30 Septemba, ziwe zishafika kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.
Kwa sababu taasisi zetu nyingi zinakuwa tunajisahau baada ya kufunga mahesabu, basi mahesabu yale ni lazima yapelekwe kwa Mdhibiti na Makaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, sehemu ya saba inasema masharti mengineyo, kwenye masharti mengineyo kifungu cha 41 Waziri anaweza kutunga kanuni kwa utekelezaji mzuri wa sheria hii, sio anaweza. Waziri atatunga kanuni kwa utekelezaji mzuri wa sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, nikienda kwenye jadweli la kwanza maadili ya viongozi (chini ya kifungu cha 40) kinachosema, maadili ya viongozi.

Mhe. Mwenyekiti, hii inatokana na umoja wa kitaifa, utawala wa sheria, *heading* yake ni hiyo. Kuheshimu watu wote. Mhe. Mwenyekiti, lakini vile vile sisi ni viongozi na siku zote lazima utoe haki kwa mwenzako. Hapa sijaona kwa sababu na sisi kama viongozi vile vile tukilinda maadili ya wenzetu lakini na wao vile vile watuheshimu kama sisi viongozi.

Sasa hivi viongozi wanakuwa hakuna maadili ya kwamba na wale tunaowalinda na wao au tunaowaongoza lazima na yule aliyekuongoza na wewe umuheshimu, na tumeambiwa tumuheshimu baba na mama, basi na hata viongozi vile vile tuwaheshimu. Lakini sasa hivi imekuwa ni tabia ya kwamba sisi hususan viongozi wa wawakilishi na wabunge unakuwa mara nyingi ile haki yako haipo. Anaweza akaja mtoto mdogo akakuvunjia heshima, kwa sababu hakuna maadili na kwenye sheria hii basi ilikuwa lazima kuwepo na maadili kama hayo, vile vile ya wananchi wawaheshimu viongozi wao.

Mhe. Mwenyekiti, nasema kwenye kifungu kidogo cha (5) kwenye hii umoja wa kitaifa, utawala bora wa sheria na kuheshimu watu wote, inasema kwamba;

> "kila kiongozi wa umma anapaswa aheshimu sheria za nchi, aheshimu, asaidie na atekeleze maamuzi ya Mahkama maalum ikiwa ni pamoja na Mahkama maalum ya viongozi".

Hapa Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli sijaona ndani zaidi na wala sina hoja, lakini nimesoma kwa kujua kwamba kila kiongozi wa umma anapaswa aheshimu sheria za nchi.

Mhe. Mwenyekiti, serikali itakuwa na jukumu la msingi kifungu kidogo cha (7) katika hiyo hiyo maadili, kinasema;

> "serikali itakuwa na jukumu la msingi kuheshimu na kutekeleza maadhimio ya vyombo vya kutunga sheria".

Serikali naiomba sana, serikali yangu inayoongozwa na chama changu kuheshimu kamati zetu za Baraza zinazofanyakazi kubwa. Naomba kama serikali imekubali hili na sheria hii, basi tusioneane haya, kwani tutakuwa hatufiki mbali. Kwa sababu lengo na madhumuni yote ni kupata ufanisi wa kazi zetu na serikali yetu ambayo kila siku tunasema kwamba ni changa, lakini kuna mambo mengi ambayo yanaturudisha nyuma.

Mambo mengi sana yanaturudisha nyuma na mbali ya kwamba serikali tunasema kupitia Wizara ya Ardhi, kwamba kuna Shirika lile la Nyumba ambalo tumelianzisha. Mimi nafikiri lingefanya kazi vizuri, kulikuwa hakuna haja kwa

sababu mambo mengi yanayosababisha viongozi kuchukua fedha nyingi mara nyingi zinakuwa zinaenda kwenye mambo ya kuekeza kwenye majumba. Lakini serikali ilikuwa yote inalenga kwenye nyumba zile, karibuni majenzi yote yawe chini ya serikali.

Naamini kwamba kama Hayati Karume angekuwepo mpaka leo Baba wa Taifa letu hili, nchi yetu hii ya Zanzibar naamini basi kungekuwa na uadilifu mkubwa, kwa sababu kitu kinachotufanya kwamba tusifate maadili watu wengi ni kujilimbilikizia mali kupitia njia hiyo. Kwa hivyo, kungekuwa na sheria hii kwamba nyumba zote zinamilikiwa na au maakazi yote yanakuwa yanamilikiwa na serikali yenyewe, basi nafikiria kungekuwa na upungufu mkubwa sana wa kupoteza pesa za umma.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa umebakiza dakika tatu malizia.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Mhe. Mwenyekiti, vile vile nikienda kwenye ukurasa huu 69 kusema kwamba viongozi wa kisiasa, kimaadili wana jukumu kuandaa sera madhubuti zenye kutekelezeka. Lakini Mhe. Mwenyekiti naona kiongozi yeyote yule ambaye anaongoza kwa nini kusiwe na kifungu cha viongozi wa kidini wawe na jukumu la kimaadili ya ushekhe wasiwe na uchochezi, kwa sababu na hili pia Mhe. Mwenyekiti, naliona kwamba ni kikwazo kikubwa kwa kupitia viongozi wetu hawa.

Kwa hivyo, kwenye maadili haya nayo pia viongozi hawa kuwa na kifungu makusudi. Siku moja Mwenyekiti mimi nitakwambia, ilikuwa kabla sijaja humu muumini wa dini ya Kikiristo lakini alipendezewa sana na mawaidha na zile daawa anazozitoa Sheikh Othman Maalum, ni muumini kabisa wa Kikristo, lakini anasema mimi katika Sheikh mmoja ninayempenda basi ni Othman Maalim. Kwa nini, sababu namna anavyotoa hotuba zake, anavyowaidhi watu wa dini yake, anasema kwa kweli ninampenda. Kwa hivyo na hili ningeomba viongozi wa kidini na wao wawe na maadili ya Kisheikh.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa na mengi ya kusema lakini kwa sababu umeshaniambia kwamba kuna dakika tatu basi nishukuru na nasema mswada huu ni mzuri niuunge mkono. Kwa sababu hakuna sababu ya kwamba nisiupitishe mswada huu mzuri ambao utaweka maadili ya viongozi wetu, tukiachana na mambo haya nchi yetu itang'ara.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo naunga mkono kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Amani kwa asilimia mia moja.

Mhe. Asaa Othman Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima na nikushukuru pia kwa kunipa fursa hii kuwa miongoni mwa wachangiaji wa mswada huu muhimu sana kwa nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, wala sitaki nitofautiane na wale waliotangulia walioukubali mswada huu, kwamba ni mzuri, unafaa na umekuja wakati muwafaka. Nimpongeze sana Mhe. Waziri na timu yake kwa kuliona hili na kuleta mswada huu kwenye Baraza lako tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na wasiwasi nilionao lakini nitamke kwamba na mimi nauunga mkono. Napata wasiwasi kwa uzoefu wa utekelezwaji wa mambo kama hayo. Kuna usemi kwamba, "Mazowea yana tabu tabia zikilingana". Kwa mazowea yetu mambo muhimu kama haya mazuri, yenye faida kwa wananchi utashangaa yanavyowekwa pembeni kana kwamba sheria haipo ama haijulikani. Lakini ni basi tu ndio yale tunayosema ni mazowea yetu tunapanga mambo mazuri, muhimu, lakini sijui niseme huwa tunaiga tu na sisi tutajwe tu kwamba na sisi tumo hatujaachwa nyuma. Wala mimi sitaki niseme kwamba tunaoneana haya siamini hata kidogo. Kwa sababu kwa nini kama ni neno la kuona aibu, kuoneana vibaya yawe upande mmoja, upande wa pili usilione hilo. Lakini ni kwa sababu ndivyo tulivyojijenga.

Mhe. Mwenyekiti, mswada huu kama baada ya kupitishwa na Baraza lako tukufu na kwa mara ya kwanza ukaanza kuvunja hii miiko ninayoisema kwamba sasa iwe basi, utatupa heshima kubwa kwanza Baraza hili. Wenzangu wametaja tumeshayapitisha mengi, makubwa, muhimu, wananchi wanakaa kuyasubiri matokeo yake hadi leo hayapo.

Mhe. Mwenyekiti, jana tulipoondoka hapa naweka gari mahali nikaingia msikitini mwananchi mmoja akaniuliza Mheshimiwa hongereni mswada mwema ule lakini si hayo? Sasa haya maneno siyasemi mimi ni maneno ambayo

ndivyo yalivyozoeleka, labda sasa serikali iondoe miiko kwa kujitathmini viongozi wenyewe kwanza, tujitathmini na mimi natajwa kwenye sheria hii kwanza tuwe wasafi.

Kuna vifungu kwenye jaduweli la kwanza, jaduweli hili mimi limenirudisha nyuma kuona kwanza ipo kazi ya sisi viongozi labda kama ni kuingia mahali hivi kujisafisha tukatoka weupe.

Ukurasa wa 67 pale kwenye maneno "Umoja wa kitaifa, utawala wa sheria na kuheshimu watu wote". Haya ni mambo makubwa mno na ni muhimu sana leo na huko tunakoelekea.

Namba 3 inasema utaratibu na taasisi hizo ni pamoja..., nakwenda na muda Mheshimiwa, kwamba taratibu za kubadilishana madaraka zinapaswa kufanyika kwa amani kupitia uchaguzi ulio huru na wa haki na uwazi. Tulikubaliana kwamba tutabadilishana madaraka ya nchi hii kwa kura moja mtu mmoja, tumeshuhudia vituko na vitimbwi waliozowea hayo wajitathmini na sheria hii ni angalizo tu kwangu, wajitathmini na sheria.

Mhe. Mwenyekiti, nazungumza kilichoandikwa ndani ya mswada huu, wajitathmini yaliyopita sisemi yamepita lakini sasa tunapitisha sheria. Wako duniani wengi tu waliyafanya waliyoyafanya sasa hivi sheria walizozisaini wenyewe zimewashika.

Mhe. Mwenyekiti, nina kumbukumbu si Baraza hili lakini ni chombo hiki hiki *Zan ID* baada ya kuletwa mswada wake wengine tulishituka kutokana na hili ninalolisema, kwamba tuna wasi wasi tu mambo yakiletwa ama yamelengwa mahali jambo ambalo ni baya sana kumtungia mtu sheria baada ya kutungia watu. Tukasema kwamba *Zan ID* hii huko mbele twendako itatumika vibaya tukakataliwa kwa nguvu kubwa na wenzetu na wengine bado tuko na Mwenyezi Mungu atujaalie twende nao. Awamu tofauti kila mmoja aliyekuwa chini ya wizara hiyo akakataa kwa nguvu zake zote kwamba haitotumika huko, *Zan ID* hiyo leo tunashuhudia *story*.

Mhe. Mwenyekiti, maana yangu nini? Maana yangu niko hapa hapa kwenye ukurasa wa 67 kwa kiongozi wa umma na sifa anazotakiwa kuwa nazo.

Mhe. Mwenyekiti, Mswada kwenye ukurasa wa 64 Sehemu ya Saba, Masharti Mengineyo. Kinga ya jumla naomba niinukuu.

Kifungu cha 39 kinasema kwamba:

> "Hakuna kitendo au kitu chochote kitakachofanywa au kuachwa kufanywa na Mwenyekiti au ofisa yeyote wa Tume, kama kutenda huko au kuacha kutenda huko kumefanywa au kuachwa kufanywa kwa nia njema katika kutekeleza majukumu yake chini ya sheria hii, kutampelekea kuwa ni mkosa".

Mhe. Mwenyekiti, kwa nia njema , nimekaa nayo sana hii kujiuliza nia njema hii tutaipimaje? Ni vipi tutaweza kujua kwamba hapa alikuwa na nia njema ama hapa hakuwa na nia njema ni kipi kitakachotufanya sisi tuamini kwamba ni moja katika mawili hayo.

Mhe. Waziri nitakuomba uje utumie muda wako utukonge nyoyo zetu kwamba hapa kifungu hiki hakitatumika vibaya, kinatupa mashaka. Wengine jibu litakuja tu kirahisi alikuwa na nia njema Mwenyekiti na akishasema akiwa na nia njema basi ndio imepita na Mwenyekiti huyu kapewa madaraka makubwa na mengi mno. Tume ipo lakini Mwenyekiti ndiye yeye kila kitu.

Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 58 uwezo wa Mwenyekiti pale nambari 13(a), kumuagiza ofisa yeyote wa Tume kufanya uchunguzi au upelelezi wa tuhuma yoyote au uvunjwaji wa sheria hii. Suala la uchunguzi ni fani, kusema ofisa yeyote nadhani haiko sawa; aagizwe ofisa mwenye dhamana hii au mwenye fani hii ya upelelezi asiwe yeyote tu, yeyote tu hatutotendea haki kwa huyo anayechunguzwa.

Mhe. Mwenyekiti, kuanzishwa kwa Tume, sifa za Mwenyekiti nambari 7(2), zimetajwa sifa za Mwenyekiti ikiwa pamoja na uweledi, uaminifu, uadilifu. Mhe Mwenyekiti, uadilifu, uaminifu ni sifa nzito kwa mwanadamu. Mimi bado tu natoa kama tahadhari kwa Waheshimiwa Viongozi waliotajwa na sheria hii kuna mengi mazito, makubwa tu, ambayo yanawaondolea sifa hizi. Sifa ya uadilifu, sifa ya uaminifu ni muhimu sana.

Mhe. Mwenyekiti, leo nchini kwetu hapa imani iliyojengeka kwa wananchi haki haipatikani bila ya rushwa, ubaguzi umekithiri, uonevu ndio mazowea sasa na ubaguzi upo tu, tunautia kwenye kisiasa, sehemu anayotoka mtu, masuala ya dini wala hayapo hapa kwetu, nyanja kuu zipo kwenye siasa na eneo gani analotoka. Sasa ningewaomba sana Waheshimiwa hawa wenye dhamana hizi haki za watu, dhulma na dhulma Mwenyezi Mungu anaisema katu haidumu na inapodumu huwa ni nakama, wasije wakatuletea nakama Mwenyezi Mungu atakwenda kuwanakamisha peke yao huko. Wanachokichuma kila mtu atalipwa.

Kuna adhabu zinaletwa na Mwenyezi Mungu anapokasirika hazitafuti kwanza, zinawachukua watu wote baadae huko ndio uchambuzi. Kwa hiyo kuna watu hawahusiani na haya, tungewaomba iwe basi na hii sheria ifanyiwe kazi.

Mhe. Mwenyekiti, jengine hizi nafasi za mwenyekiti na wakurugenzi. Mara nyingi tunasema nafasi kama hizi hasa kwa sheria hii, sheria ambayo ina uzito wa aina yake na umuhimu tunampa Rais jukumu la kuteuwa watu hawa. Sifa za watu tunaowahitaji kwenye sheria hii ziko wazi kwa nini zisitangazwe watu wakaomba wenye sifa wapo. Sifa hizi walionazo watajaza waombe lakini bado tunazirudisha kwa Rais, Rais ni binadamu ana shemegi, ana wajomba, ana wakwe, ana marafiki.

Tumemaliza mimi na kamanda Hamza Hassan chuo kimoja, tumechukua shahada moja lakini tunapishana uwezo, mmoja hapa ni rafiki wa Rais kumbe uwezo wake ni mdogo kuliko mwenzake, yapo hayo. Rais anapelekewa watu sio kwamba kila mtu anamjua yeye, wanapendekezwa hawa watu anapelekewa Mheshimiwa ni hawa na watu walio karibu yake watatafuta na wao waliokaribu yao kumbe ni wale waliwooza. Ndio tukasema ingefaa sana kumuondolea mzigo huu Rais nafasi hizi zikatangazwa Mhe. Waziri.

Haya tunayarudia, tukiyarudia siku hadi siku bado msimamo ni ule ule kwa sababu tunatafutana mjomba, shangazi wa nani na nani, nani ni yupi, huyu hafai anatoka wapi, hilo ndilo liliopo, nitasema hivyo Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu kwa nini hatusikilizwi na serikali ya nchi hii. Hivi kuna ubaya gani hizi nafasi zisitangazwe. Watu waliopo watajitokeza.
Lakini bado hapa si bure ndio nikasema tusifanye mambo tusitafute sheria kwa kukimbilia kwamba labda kuna nchi fulani wao wameshafika hapa sio bado tutaonekana nyuma, kama hatujakuwa tayari bora tuchelewe. Tuchelewe lakini tukienda twende na wenzetu wanavyokwenda. Nasema hivi Mhe. Mwenyekiti, kwa mifano kadhaa tu na masheria mpaka Waheshimiwa hawa humu wengine wameshazisahau, mpaka umshitue atakwambia kweli tumepitisha hajaisikia kutumika pahali, tena jengine zinatusema mno.

Mhe. Mwenyekiti, tumepitisha sheria hapa kutokuvuta sigara hadharani jambo ambalo linasababisha matatizo makubwa hasara ya serikali, afya ya wananchi inakwenda, unapanda gari watoto wachanga wamo mle mtu anapanda na sigara mdomoni. Hakuna chochote mwenzangu jana kataja *helmet* na mengineyo mengi. Sasa tusifanye tu kwamba labda tukishapitisha ndio hivyo, hapana lazima zisimamiwe na zitekelezwe na zifatiliwe.

Mhe. Mwenyekiti, mie Mwakilishi wa Jimbo la Wete naukubali mswada huu kwa maana kama si leo itakuwa kesho kama si kesho itakuwa keshokutwa, kama si keshokutwa ni mtundogoo. Lakini ikishapitishwa itakuwa ipo na wale wenzangu watajitayarisha waliozoea kuyafanya wayafanyayo wakijua kwamba sheria ipo.

Jana Mhe. Hija Hassan Hija alikuwa na lake linalomgusa ndani ya Jimbo lake kuhusiana na uadilifu huu wa viongozi hawa wa umma. Mimi nataka nitoe tahadhari litakuwa langu la mwisho kwa leo.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar ni nchi, ni Taifa ambalo Mwenyezi Mungu katujaalia rasilimali yetu kubwa ni bahari ndio mgodi wa matumaini yetu na maisha yetu. Wenzetu waliopewa dhamana kubwa za kutuongoza na wasaidizi wao lazima wazisimamie rasilimali hizi kwa faida na maslahi ya nchi hii. Kuna tetesi kuhusiana na usajili wetu wa meli na *agent* wetu tuliekuwa nae Dubai, kuna wenzetu mikono imeshaingia huko. Serikali ilikuwa inapata....

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa umebakiza dakika tatu malizia.

Mhe. Asaa Othman Hamad: Zinatosha kumalizia hizo.

Serikali hii ilikuwa inapata fedha za kusaidia maendeleo ya watu wake. Watu kwa sababu zao bahati nzuri yamefanyika sheria hatujaipitisha sijui ikishapitishwa itakuwaje, tutaiuliza kuwa na sheria. *Agent* aliyepewa sasa kunyanganywa yule alietangulia mwanzo hajaleta, hajasajili hata Mtumbwi wala Ngalawa wala senti tano haijaja nchini. Badala yake serikali ndio imetoa dola zetu kumpelekea *agent* huyu angalau alipe mshahara. Kuna mtihani sifa za mswada huu na viongozi hao.

Mwenzangu mmoja alieko huko aliyeshuhudia maana nina mpaka picha walipokuwa wanasaini mkataba huu, anasema watu safi kabisa Zanzibar Dr. Ali Moh'd Shein mwenyewe na Makamu wake wawili, walibaki tafuteni sana muwape nafasi kama hizi. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kupata nafasi kutoa mchache sana kuhusu mswada huu muhimu na adhimu unaohusu maadili ya viongozi na sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ikiwa tumo katika orodha ya viongozi hao.

Pengine nitumie ule msemo wa kiswahili kuwa "Mtoto akichezea wembe mpe" Kwa hivyo, sisi tunachezea wembe, sisi ndio tunaotunga sheria na kama utafuatwa upande huu kuna baadhi ya watu utawachinja. La kama itakuwa kama atakakotoka mtu kafanya hapa akaondolewa hapa kama mchezo wa bao la kete ndio ile ile inaweka kishimo hichi unaitia kishimo chengine, ndio huko nyuma tunakotoka watu wanafanya majanga adabu yao ni kuhamishwa hapa wakawekwa pale, ni kama mchezo wa bao tu. Lakini nadhani sheria hii huwenda ikafuta huu mchezo wa bao.

Mhe. Mwenyekiti, watu waliomo katika orodha hii ni wengi kidogo kaanziwa Mhe. Rais na tumemalizia kwenye wateule wa Rais na Mawaziri. Sasa wale ambao watakwenda kinyume na sheria hii baada ya kuwa sheria watachukuliwa hatua za kinidhamu na za kisheria. Lakini Mhe. Mwenyekiti, niulize swali katika Katiba ya nchi hii Rais anachukuliwa hatua? Kama anachukuliwa sawa kama hachukuliwi kwa nini akaingizwa hapa, sisemi aondolewe. Lakini kwa Katiba na Sheria za nchi hii hivyo ni kweli Rais anachukuliwa hatua?

Halafu Mhe. Mwenyekiti, hii Tume iliyoanzishwa au utakayoanzisha ndio itakayoshughulika kutafuta hayo ambayo yanataka kutafutwa. Lakini wajumbe wake na wao ni miongoni walimo katika orodha hii wao watachunguzwa na nani? Huyu Mwenyekiti na Kamishna wake wawili kwa sababu hawa walioteuliwa na Rais na huku katika orodha hii wanaingia je, wao nani atakawachunguza.

Mhe. Mwenyekiti, Mswada huu wa maadili ya viongozi kama ulivyo miswada mengine una uzuri wake na una ubaya wake. Kwa kuwa watu ndio hawa hawa waliokwisha zoea hivyo tulivyozowea; tumezoa rushwa, tumezoa ubaguzi, tumezoa kutofuata sheria. Sheria hii nayo hofu yangu isije ikawa kama hizo zilizopita. Lakini hata kama tutaidharau iko siku kwa sababu ipo, iko siku itatumika hata kama hatuko tena sisi katika madaraka, itatuandama kwa sababu tunaitunga kwa kuanzia hapo inapotungwa kuendelea tunakokwenda. Itakujabainika kuwa kiongozi fulani katika wakati alifanya hivi na hivi na sheria hiyo ipo kwa hivyo itamuandana.

Mhe. Mwenyekiti, ufisadi uliopo katika nchi hii na watu walivyojilimbikia mali kinyume na sheria kama mapesa hayo yangekusanywa yakarudishwa, basi huu umasikini tunaouhubiri kuwa tuondoe umasikini fedha hizo ambazo wanazo watu pengine kwa njia walizozipata wanazozijua wao, zingeweza kutosha kuondoa umasikini kwa Wanzazibaari. Lakini hazirudi wala hazitorudi Mhe. Mwenyekiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwenyekiti kapewa uwezo mkubwa sana hata wale Makamishna wake ni kuwa anawaagiza. Mhe. Mwenyekiti, ningependekeza kuwa wale Makamishna wake ashauriane nao katika maamuzi ya mambo hapa yeye tu wale wote ni kama watoto nyumbani niletee maji, nifanyie hivi, lete vile. Hasa Makamishna wa hii Tume si chochote mtendaji na aliepewa mamlaka ya kutenda na kufanya kila kitu ni Mwenyekiti peke yake kwa nini?

Basi ilikuwa kusiwe na Tume kuwe na Mwenyekiti tu. Kwa sababu kama ni Tume basi ni lazima kuwe na watendaji wa kazi kwa pamoja.

Mhe. Mwenyekiti, hizi sifa mbali mbali zilizotajwa kwa viongozi takribani asiwe mlevi wa kupindikia, kwani ulevi wa kupindikia ni upi kwa sababu kila mtu anakiasi chake kwa kila kitu. Tukisema mtu asile akashiba sana shibe yangu mimi ya kula sana iko kiasi kadhaa, lakini shibe ya mtu mwengine ya kula sana pengine ni yangu mimi mara sita, ndiyo kala sana. Kwa hivyo, tukisema asiwe mlevi kupindukia bado hatujaweka masharti ni kuwa asiwe mlevi, asiwe mropokwaji, kuropokwa ni nini? Ni kweli kiongozi aliekuwa na dhamana kama anakaa anaropokwa hiyo dhamana aliyopewa anaijua na anaithamini?

Mhe. Mwenyekiti, mswada huu umetaja mambo mengi ambayo yamo katika *practice*. Tunasema kuwa tutizame katika kifungu kidogo cha 67

> "Taratibu za Taasisi hizi ni pamoja na kwamba taratibu za kubadilishana madaraka zinapaswa kufanyika kwa amani kupitia uchaguzi ulio huru wa haki na uwazi"

Hivyo Mhe. Mwenyekiti, ni nzuri na inahitaji wale ambao tunasimamia tunaingia katika uchaguzi tuione vizuri sentesi hii. Uwe wa haki, wa huru na amani na tuondoe ile dhana kwa serikali hii kwa kuwa ilikuwa ni ya Mapinduzi haitopatikana kwa vikaratasi, anaesema hivyo itakuwa hii anaikataa. Kweli na Mapinduzi lakini sasa tumechagua utaratibu wa kubadilishana, kwa hivyo vikaratasi ambavyo vinakataliwa kwenye Baraza hili kuwa kisa ni vikaratasi. Lakini sentensi hii inatuelekeza kuwa serikali hii itapatikana kwa uchaguzi.

Kwa hivyo, sisi ambao hatujui kuwa uchaguzi ni haki na wa halali tuelimishwe, tuache zile kauli za kusema kuwa serikali hii haikupatikana kwa vikaratasi. Mhe. Mwenyekiti, sentensi hii ni nzuri ni kubwa, yenye maana pana, sina hakika kama itatekelezwa na sina hakika huyu mwenyekiti ambaye ndie atakaesimamia maadili hayo pindipo ikienda vyenginevyo kuwa ataweza kuchukuwa hatua yoyote dhidi ya aliekwenda kinyume na hii sentesi ilivyo. Kwa sababu tunatafuta utawala gani, Utawala wa Sheria na haki za binaadamu. Sasa Utawala wa Sheria ni ule unaotokana na Uchaguzi na ridhaa za wapiga kura.

Mhe. Mwenyekiti, ili mswada huu uweze kufanyakazi barabara lazima sisi viongozi tuliotajwa humu tujielewe, tujifahamu, tujichunguze na tujirekebishe. Kwa sababu ni sisi ndio wenye madaraka na wale wenye dhamana pengine za kuajiri wanatumia rushwa mara nyengine za aina tofauti. Wengine wanataka rushwa ya pesa matumizi, wengine wanataka rushwa ya aina nyengine, kama unataka nafasi hii usiku njoo pahala fulani; nayo hii ni rushwa na iko na wengine wanaitumia na kama hujatoa rushwa hiyo ajira hupati, inasemekana hivyo.

Sasa tujijue sisi tuliokuwa tuna dhamana kuwa hayo sasa yamepitwa na wakati, pindipo mswada huu utakapokuwa sheria Mhe. Rais akasaini na kuanza kutumika.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sitaki niseme sana wala sitaki niseme mengi, kwa sababu Mswada huu upo wazi sana, umefafanuliwa vya kutosha na unatuhusu sisi wazungumzaji na wenzetu wengine ambao hapa hawapo, lakini wamo katika orodha ya wanaohusika ili wembe usituchinje wenyewe. Kila mmoja ajichunguze, ajipeleleze na ajirekebishe, ili Mswada huu utakapokuwa sheria yeye usimkumbe. Vyenginevyo itakuwa tumegeuka pweza tunajiparia makaa sisi wenyewe kwa sababu Mswada huu hauwendi chini kwa watu wa kawaida, unakuja kwa hawa tuliotajwa tu.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi nitafurahi kama Mswada huu kwa sababu mara nyengine unatokezea uteuzi wa Mhe Rais, mtu katajwa leo lakini anaambiwa uteuzi wake unaanza tarehe kadhaa, tarehe ya nyuma. Kwa hivyo na Mswada huu ukishasainiwa ni bora uanze kutumika kwa miaka mitatu minne au mitano iliyopita nyuma.

Mhe. Mwenyekiti, Mswada huu unachunguza mtu na mali zake. Je, ni kiwango gani cha mali ambacho kitaonekana kuwa hiki aah! Kiwe kimepita mpaka na hiki kinafaa awe nacho.

Kuna kipimo gani cha kuona kuwa mali hii ni nyingi, kapataje na kama imezidi, kuna vigezo gani kuona kuwa hii ni *size* ya mtu huyu kuwa na mali hii. Kwa sababu tutapeleka au tutajaza mali tulizonazo, nyumba 12, gari tisa, mashamba matano. Sasa katika mali zote nitakazozitaja, Tume hii kuna kiwango kitaonekana kuwa hiki kimezidi ninyang'anywe au tunatangaza ajulikane tu kuwa mheshimiwa fulani ana mali kiasi fulani, na kama kujulikana

kuwa ana kiasi fulani, kitasaidia nini. Kama kuna kiwango ambacho anamiliki chengine anyang'anywa kitaenda wapi, kitarudi Serikalini.

Je, sheria hii itakuwa na uwezo wa kumchukulia mtu mali yake kama kuirudisha Serikalini. Mhe. Mwenyekiti, ningependa kujua kwa sababu kuna uchunguzi wa mali, kujulikana tu kuwa kipo hivi. Mimi ninahisi haitoshi hatua zifuate na pia baada ya hatua hizo mali iliyozidi kiwango kilichokubalika kichukuliwe na ashitakiwe. Lakini ikiwa huyu hashitakiwi ndiyo iliyofanya ikawa wakubwa tunafanya tutakavyo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi sitaki niseme mengi nimalizie hapo, niseme kuwa Mswada huu, Miswada mingi mimi siungi mkono lakini huu nitaunga mkono kwa asilimia karibu 90.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Mohamed Haji Khalid, sasa ni zamu ya Mhe. Hassan Hamad Omar ninatarajia atatumia muda wake vizuri ili na Mhe. Ashura Sharif Ali aweze kuchangia.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Mwenyekiti, na mimi ninakushukuru sana kunipa nafasi hii kutoa maoni yangu katika Mswada huu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma na kuanzisha Tume ya Maadili ya Viongozi na mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijaalia kuwa katika uhai, uzima na afya, niseme *alhadulillah* kwa neema aliyotupa Mwenyezi Mungu.

Mhe. Mwenyekiti, tukizungumza neno maadili ni jambo jema. Maadili lina upana wake, unaweza ukawa na maadili mema au ukawa na maadili mabaya, lakini kwa mujibu wa Mswada huu tunatakiwa tuwe na maadili mema wote, tuliotajwa katika Mswada huu na hata wale waliokuwa hawamo katika Mswada huu, lakini hana madhumuni ya kuwa na maadili mema ili kuwatendea haki wananchi wetu na kuifanyia mambo mazuri nchi yetu ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, wengi wameusifia Mswada huu, hata mimi ninausifia kama ni Mswada mzuri ambao pia utawakomboa wanyonge ambao walikuwa wanaogopa lakini kwa mujibu wa Mswada huu watakuwa na uwezo wa kusema, kwa sababu na wananchi nao wametajwa hapa kutoa taarifa na kuzipeleka kwenye Tume.

Mhe. Mwenyekiti, katika mambo haya ya maadili kwanza ni kufuata utaratibu wa haki za binadamu, kuwa na utawala bora, ndiyo haya yanayotupelekea mpaka tukawa na Mswada huu. Lakini wenzangu wengi wamesema na sipendi kurudia rudia lakini ni tatizo, kwamba sheria zetu ni nzuri lakini usimamizi wake siyo mzuri, ndiyo maana tunafikia mahali sipo. Lakini *inshaallah* kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu, sheria hii tunayoichangia na baadae ikapita hapa Baraza la Wawakilishi na Mhe. Rais akaitia saini basi tunaomba wote wanaohusika na usimamizi waisimamie vizuri na ifanye kazi zake ili kuinusuru nchi.

Mhe. Mwenyekiti, nikenda katika sehemu ya Mswada huu katika kifungu cha 12 (b), naomba ninukuu, "Kupokea tuhuma za taarifa za uvunjwadi wa maadili kutoka kwa wananchi". Naomba niongezee maneno haya yafuatayo, "Kupokea tuhuma na taarifa za uvunjwaji wa maadili kutoka kwa wananchi zinazomuhusu kiongozi wa umma", iongezwe maneno hayo.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu katika kifungu cha 18 (3) kumetajwa mambo mengi pale. Lakini hapa nitazungumzia uropokaji. Naomba vile vile liongezwe neno, "Uropokaji na matusi". Tumeshuhudia mambo mengi ya uropokaji hapa na hata viongozi kudhalilishwa kwa matusi makubwa na hakuna hatua zozote mtu anazochukuliwa. Mtu ana wadhifa mkubwa Serikalini lakini anatukanwa na watoto wadogo, hakuna hatua zozote zinazochukuliwa, haya ni maporomoko ya maadili. Hatuwezi tukaropokwa na tukatukana. Wengine wanaropokwa kwa kutaja mambo mazuri tu lakini atakayeropokwa kwa matusi, naomba hili neno niongezee.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu katika Mswada huu katika kifungu hicho hicho cha 1(11), kimezungumzia unyanyasaji wa kijinsia. Maana unyanyasaji wa kijinsia huu ambao wengi tumeshuhudia, mambo mengi watu wananyanyaswa na kukosa haki zao za kimsingi. Mhe. Mwenyekiti, naomba uniruhusu nitoe mfano ulio hai katika Mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, kama kuna mnyanyasaji mkuu basi mimi niseme anayenyanyasa watu kijinsia ni Sheha wa Shehia ya Kiungoni. Kwa kutumia mfano wa neno hili hapa. Mhe. Mwenyekiti, Katiba yetu inazungumza mtu yeyote mwenye kutimia umri wa miaka 18 na akatimiza masharti yaliyotajwa pale ana haki ya kupata *Zan ID*. Mhe. Sheha huyu wa Kiungoni na naomba nimtaje jina lake hasa wanisikie, anaitwa Omar Khamis ni Sheha ya Kiungoni huyu, huyu katika kunyanyasa watu amevuka mipaka.

Mhe. Mwenyekiti, huyu ni mtoa huduma kama watu wengine wanavyotoa huduma za Serikali, lakini huyu alifika watu kwenda kutaka fomu tu za kuweza kupata *Zan ID*, akawaambia wananchi siku ya tarehe 17 ili mupate fomu hizi basi kwanza mujitolee mukachukue udongo, wananchi wakaridhika wakenda kuchukua udongo, ni wananchi wasiopungua 37 wakapeleka kwenye *nursery* wakajaza na sasa hivi tayari *nursery* hiyo imeshakuwa nzuri, lakini *wallahi,* haki ya Mungu hata mtu mmoja hakumpatia fomu ya kwenda kuchukua *Zan ID*.

Mhe. Mwenyekiti, sasa mambo haya ya unyanyasaji huu utatokezea mwengine, watu wana haki zao za msingi na pia umewapa agizo wakachukue jambo fulani wamefanya na wewe mpaka leo hujatoa fomu, halafu munazungumza kama maadili ya viongozi, yapo wapi? Basi kama sheria hii ikipita huyu mtu ni wa kuchukuliwa hatua, si mtu wa kumnyamazia kimya.

Mimi nimpongeze Mhe. Mwinyihaji Makame wakati alipokuwa Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tulizungumza naye katika bajeti moja hapa, kwa kweli alitufuata na akenda akazungumza na watu wote wahusika, akiwemo yeye mwenyewe Waziri, Mkurugenzi wa vitambulisho, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wabunge, Wawakilishi, Madiwani na Masheha wote pale Benjamin Mkapa. Na akazungumza kama kuna tofauti ziondolewe lakini *wallahi* kwa kutojali au kwa mikakati ya makusudi, basi mpaka leo hii dhuluma inaendelea. Halafu munaweka maadili ya viongozi, utayapata wapi!

Mhe. Mwenyekiti, hii ninampongeza sana kwa sababu alitimiza ile ahadi na akatuita. Na aliyekuwa Mkuu wa Mkoa Mhe. Dadi alizungumza pale Sheha yeyote atakayethubutu kumdai mwananchi cheti cha kuzaliwa basi Sheha huyo tutapambana naye. Lakini *wallahi* baada ya wiki tu mambo yalijirejea pale pale. Mimi nimwambie Mheshimiwa wangu aliyeshika wadhifa Mhe. Haji Omar Kheir naye alitupa ahadi katika bajeti iliyopata kama yale tuliyozungumza na tukayatolea ushahidi humu, atakwenda kuyaona mpaka leo ahadi ile haijatimiza basi atekeleze ahadi.

Tumeambiwa moja wapo katika maadili ya viongozi ni kutekeleza ahadi. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, na huyu atekeleze ahadi, akione hiki kwamba jamani mtu mzima akisema jambo au ukisikia mtu mzima analia basi pana jambo, usifikiri tunazungumza kwa utashi tu mambo haya yapo. Na kama yapo isiwe tunatwanga maji kwenye kinu ikawa hayakai, lazima yafuatiliwe na yafanyiwe kazi.

Mhe. Mwenyekiti, hata mule tumezungumza tena mukiyafanyia kazi utasifiwa lakini kama hamuyafanyii kazi tutayasema kila siku. Ni haki yetu na hapa ndipo mwahala mwa kusemea, hatuna pengine pa kusemea, lazima tuyaseme.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mwakilishi haki yako kusema lakini tunajadili Mswada. Kwa hivyo ujadili ndani ya Mswada usitoke nje ya Mswada, haki ya kusema unayo na kila kipindi cha Baraza la Wawakilishi inatoa nafasi ya kuzungumza. Kwa hivyo haki ya kusema unayo lakini bado uende kwenye Mswada, ndiyo ninachosisitiza.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru lakini mimi katika Mswada sijaenda *against* na hilo, nimezungumzia unyanyasaji na nimetoa mfano wa unyanyasaji. Na ninasema tena mnyanyasaji yule achukuliwe hatua.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na hayo kuna mambo mengi tu ya Mswada huu yamezungumzwa na mimi sina budi kuunga mkono kwa asilimia mia juu ya mia. Lakini haya tunayozungumza yatiliwe maanani.

Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana mheshimiwa, sasa nimpishe Mhe. Ashura Sharif Ali na kama muda utatosha basi tutampa Mhe. Omar Ali Shehe.

Mhe. Ashura Sharif Ali: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, mwingi wa rehma aliyetujaalia uhai lakini pia akatupa na uzima na akatuwezesha kuwepo hapa kutekeleza majukumu yetu kwa maslahi ya taifa letu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kumshukuru *Allah Subuna Wataallah*, nikushukuru na wewe kunipatia fursa hii ya kutoa alau mchango wangu mdogo ijapokuwa nilikuwa ni Mjumbe wa Kamati, mambo yangu mengi niliyakamilisha huko kwenye Kamati.

Mhe. Mwenyekiti, nichukue fursa hii tena kuipongeza Serikali kwa maamuzi yake ya kuleta Mswada huu mbele ya Baraza lako hili tukufu. Mhe. Mwenyekiti, ninadhani kuna mengi ambayo tulikumbuka katika historia ya Zanzibar iliyokuwepo kale na zama ya Chama chetu cha *Afro Shirazi Party* kilipokuwepo, kilikuwa kina miiko ya uongozi.*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, leo tunarudi tena kusema kuna maadili ya kiongozi wa umma. Yeyote ambaye anafahamu tulikotoka, anajua kwamba historia ya Chama chetu cha Afro Shirazi kwa wakati ule kulikuwa na miiko ya kiongozi. Leo tumeongeza tumeleta tena wa umma, ndiyo Afro Shirazi tu. Ninadhani kama laiti tungelikuwa tumeyachukulia yale ambayo tulikuwa nayo kule nyuma, hivi leo tungehitaji kuziba viraka kwa yale ambayo kwa wakati huu yamepitwa na wakati tu. Tusingekuwa tunahitaji kuileta hii sheria, hii sheria ingekuwa ni endelevu kwa historia hiyo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ninaamini kwamba Serikali nia yake kwa sasa ijapokuwa yenyewe ina vidonda vingi lakini nina imani kuna siku kwamba haya kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu yatatekelezeka. Nina imani kwamba taifa letu limefika pahala likaona wenyewe kwa misingi na taratibu zinazoendeshwa sekta za umma pamoja na viongozi mbali mbali wa kisiasa, hali haipo shwari kwa maslahi ya taifa juu ya wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, uchumi wa taifa unahengahenga kwa maslahi ya wananchi, ukusanyaji wa kodi, huduma za kijamii zimepoteza uwezo kwa sababu ya kumomonyoka maadili ya viongozi wa Zanzibar. Imani yangu Mhe. Mwenyekiti, sheria hii Rais atakapoitia saini, tutakuwa na kipindi cha mpito, maana hii sheria ina kipindi cha mpito cha kujitathmin tulikotoka, tulipo na tunakoelekea na taifa lenye viongozi mahiri linapotengeneza vitu hivi lazima lijiwekee mipango ya utekelezaji wa sheria yenyewe.

Sheria hii ni msumeno, unakata mbele na unakata nyuma. Tena haikuchagua, haikubagua; imetaja orodha ya viongozi wengi ambao kwa kweli kwa njia moja au nyengine ndiyo watendaji wakuu wa shughuli za wananchi.

Mhe.Mwenyekiti, mswada una malengo makubwa ambayo wananchi wanaotusikiliza wakati huu wanajiuliza, masuala, hivi hichi kinachosemwa kweli kitatekelezeka au ndio hayo hayo, niambie serikali itakuwa aibu kubwa kusimama ukasema mwenyewe halafu usitekeleze. Mwenyezi Mungu *Subhanah* wataala ametaka muda huu sheria hii iingie.

Kuna wengi walikuwa hawataki, lakini muda alioupanga Mwenyezi Mungu kwa sheria hii iingie ni sasa hivi kwamba wanyonge wengi wanapika kelele dhidi yetu sisi viongozi tunaowaongoza katika Taifa lao. Wamekosa sauti za kusemea, Baraza hili ndio chombo chao cha kusemea, akitoka hapa akifika, huku kule yeye ndie muhisika mkuu wa kunyanyasa mnyonge.

Mhe. Mwenyekiti, kuna kifungu cha kwanza hapa kinasema kwamba maadili ya viongozi wa umma yatalenga kwa kadiri inavyowezekana kuweka na kukuza misingi ifuatayo kulingana na matendo ya kiongozi mwenyewe, kuhusiana na viwango vya maadili kwamba viongozi watafanya kazi kwa uaminifu na ukarimu, umakini na kutosheka na kukuza maadili kwa kiwango cha juu ili imani ya wananchi katika utendaji wa serikali bila ya upendeleo iimarike.

Hichi ni kipengele kinachoonesha wazi wazi kwamba patakapotumika uwadilifu na huruma ikaingia ndani yake, maana yake yale mambo ambayo kwa sasa imekuwa serikali nzima inanuka uvundo kwa sababu ya kuweza kushindwa kusimamia wale ambao wanakiuka maadili ya uongozi.

Mhe. Mwenyekiti, nayasema haya nikiwa nina ushahidi huu katika mkono wangu, hii ni barua iliyoandikwa na kikao rasmi cha wananchi wa Nyanjale mwaka 2011. Waliitahadharisha serikali na taasisi kabisa, jamani mnanunua huku lakini eneo letu Bandari yetu, njia zetu, mambo yetu haya sisi hatutokubali.

Mhe. Mwenyekiti, leo wanawake wapatao 150 wamefukuzwa kwa kutumia nguvu za dola katika eneo lao la kutafutia riziki, hawana pakwenda huu mwezi wa bamvua wao huwa wanapika na kupata riziki zao, wana watoto mayatima wana watoto wao wanaosoma wengine ni wasichana mashuleni, mwezi huu hawakufanya hilo, amepewa muwekezaji ikitumika nguvu ya serikali ya kupitia viongozi mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, kwa huzuni kubwa niombe serikali kwamba kwa sababu tunakwenda kwenye utaratibu huu wa maadili ya viongozi, ichukuwe fursa ya makusudi watu wale warudi katika maeneo yao na waweze kufanya shughuli zao za kiuchumi. Wanawake wapatao 150 serikali haina ajira, inasema jiajirini, viongozi waadilifu, waaminifu, wenye kutenda haki kwa raia hao, wanawaondoa maeneo yao na kuwatupilia mbali na kwa kutia sura za ubaguzi ndani yake, inasikitisha.

Imani yangu chombo hichi kama ndio kauli ya wananchi. Spika wa Baraza hili aliteuwa Kamati Teule ya Kisekta, ndio uadilifu. Kamati ikatumia fedha za walipa kodi ikaenda kuona huko kuna nini. Kamati haijasomwa Barazani haijatoa majibu, serikali imetoa maamuzi, tuko wapi, tunakwenda wapi, tunataka nini, ni mtihani.

Nayasema haya nikiwa na ushahidi wa (a-z), nina *documents* zinazoonesha kwamba wananchi walikataa wenyewe, muhuri wa Sheha wa eneo husika imo. Kwamba kikao chao wanakataa, lakini bado serikali inangangania mpaka uharibifu wa mazingira unaafanyika...

Mhe. Mwenyekiti: Utaziwasilisha hizo *documents* kwangu wape wahudumu.

Mhe. Ashura Sharif Ali: Ahsante zitafika hizo *documents,* nakushukuru Mhe. Mwenyekiti.

Lakini pia, nna *documents* nyengine ambazo watu wa mazingira walifanya uchunguzi wa miradi ya serikali ya kimazingira katika mahoteli mbali mbali, basi wamekutana na mkasa huu. Kuna hoteli unaambiwa hizo za vigogo, hazikufanyiwa tathmini ya kimazingira, lakini pia hata *ZIPA* yenyewe hawaijui miradi hiyo ni vitu vya ajabu katika Taifa letu kutokea vitu kama hivyo.

Sheria hii itakuwa muarubaini wa matatizo yaliyojitokeza kwa muda mrefu. Umefika wakati nasema kwamba haya ameyapanga Mwenyezi Mungu kama kuna wengine walikuwa hawaitaki sheria hii, lakini tujiulize jamani hivi Mwenyezi Mungu hakuna wengine anaoweza kuwachagua wakawa viongozi tuwe mimi na nyinyi.

Tujue kwamba Mwenyezi Mungu ametaka kutujaribu tutawaongoza vipi wenzetu, viongozi wa leo ndio tutakaokuwa raia huko kesho na sisi tukapata viongozi wengine wakatuongoza. Hivi haya tunayoyafanya au tunayoyatenda tunadhani na sisi tunaweza tukaridhia hayo. Migogoro ya ardhi tumeunda Kamati Teule hapa zaidi ya 3, migogoro ya ardhi imekithiri mno na ardhi hizi ukitaka kujua wenyewe ni vigogo, ndio lugha inayotumika, ni aibu.

Yalisemwa hayo *Afro*-Shirazi ni miko mtu kujikusanyia mamali, hatutaki upebari, miko hiyo ya kiongozi wakati ule wa *Afro*-Shirazi yetu. Leo tumerudi tena tunaogopa kukagua, nasema tena; mali zitangazwe Mhe. Rais saini hii uitie, wale ambao watakiuka haya wenyewe wamejiingiza hatiani hakuna huruma. Mimi nina imani kwamba tutafika huko, hatuwaza hivyo.

Nije tena katika hichi kifungu ambacho kinasema hapa Umoja wa Kitaifa, Utawala wa Sheria na kuwaheshimu watu wote. Kifungu cha pili kisema vipi hapa;

"Taratibu za kitaasisi na za kidemokrasia zitahakikisha kukidhi mazingira ya kitaifa ya ndani ya nchi, hivyo zinapaswa kukuzwa".

Mhe. Mwenyekiti, hichi ni kifungu kitamu sana, maana sisi wote ni Wazanzibari na tukijiangalia aliyekuwa hakumuao ndugu yake, kamuoa dada yake, hata Baraza limezoea humu ndani kuitana shemegi na mjomba na dada yangu na ndugu yangu. Hii inaonesha wazi kwamba wote Wazanzibari mara nyingi tumekuwa ni kitu kimoja na tumeungana kwa njia moja au nyengine.

Serikali ya Umoja wa Kitaifa sura yake na taswira yake inaoneshwa msingi wake huko juu tu, ndio ukweli. Ukienda kwenye Wakuu wa Mikoa tizameni nyie wenyewe, je, ile umoja wetu tunaotoka wa Serikali ya Taifa tutafikia katika msingi huu wa kujenga Umoja na Sura ya Kitaifa, tuangalie Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya nao pia wanavunja taratibu unawakuwa wamevaa sare za vyama vyao, tujiulize hayo ndiyo maadili. Hivi wewe ukivaa vile na mwengine akivaa vile, huo utendaji utakuwepo na huo Umoja wa Kitaifa utakuwepo.

Nataka niwaambie kitu kabla *Afro*-Shirazi leo niko huko nimehamia huko kwa sababu ndio msingi mkuu, kulikuwa na vyama vingi; vilikuwepo huko vingi *ZPP,* sijui, hebu nitajie kidogo nikumbushe, ndio najua mnavijua sana. Yuko mwana *Afro*-Shirazi mwana kindakindaki mwezangu hapa, vilikuwepo. Lakini vikaja vikaondoka vile vyama ikaja *Afro*-Shirazi.

Afro-Shirazi imeondoka lakini Wazanzibari ndio wale wale waliotoka pale wakenda kwenye CCM, wakatoka tena CCM, ikazaliwa tena Vyama Vingi na waliozaa vyama vingi hawa ni wale wale Wazanzibari, si wengine. Tuna nini tunafika pahala ya kukaa pamoja, tukaendesha siasa za kistaarabu hatimae tumebalika mifumo na tumesahaliana. Tunakwenda sehemau ambazo hazigusani na mambo yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kama hivi ndivyo tunavyokusudia kwamba Utawala utakuwa wa Sheria na Misingi ya Haki za Binaadamu, basi miongoni mwao ni kusema kwamba jamani tujaribuni sana kuiangalia Katiba ya nchi. Katiba yetu iko wazi kabisa kila mtu ana haki na uhuru wa kuabudi dini aitakayo, leo mtihani ukitaka kufanya muhadhara utaambiwa ukaombe polisi, aibu, ndio ukweli huo.

Ukaombe kwanza kwa sababu itakuwa, hivi jamani kila mtu ana haki ya kuabudu dini aitakayo, Katiba hivyo! Kwa msingi ule wa Katiba unauvunja na Katiba ndio Sheria mama katika Taifa, unabonyengwa huko na unaambiwa sasa kila unachokitaka ukaombe tutaomba mangapi jamani na Mwenyezi Mungu hakuta hilo, yeye alitaka na akasema wote tuko sawa. Katuumba tofauti na rangi tafauti na makabila tafauti ili tujuane tu, tunazuiliwa hadi hali hiyo.

Tujitafakari na tujiulizeni jamani kama kweli tuna maadili, basi tuna dini zetu na uislamu unaujua unatupendekeza na umoja ndani yake, hali tuliyonayo ya Zanzibar haiko shuwari ndio ukweli. Wananchi wamepoteza hamu ya kuweza kusikia mambo yote, aah! ndio hao hao bwana wanajuana wenyewe hao, kila kitu masikini wamekuwa wamejikunja. Mheshimiwa "kizuri kinajiuza".

Kama serikali ingeliweka mifumo na akitandika hasa mifumo ya Demokrasia na Utawala Bora hasa, haki za wanyonge ikawa zinapatikana wala isingekuwa mashaka. Huu mswada wala usingekuwa unampa mashaka na wasi wasi. Lakini mswada huu unatoa mashaka na wasi wasi, mimi naomba utiwe saini kesho kama unapitishwa kesho hapa, Rais autie kesho kabisa wala sina wasi wasi, najua tutajifunza lakini tutafika.

Tubadilishe *mindset* zetu, tuone sasa tuko wapi na tunaelekea wapi ili tuweze kufika na Taifa hili tuliondolee migogoro, migogoro ya Taifa hili haileti mtu mwengine. Maadili ya viongozi yakivunjwa, maana yake wale unaowaongoza unawasababishia mambo ya ajabu ajabu.

Mhe. Mwenyekiti, kuna ukurasa wa 70, kuna kitu kinasemwa hapa kuwaheshimu watu, viongozi lazima waelewe kwamba tabia na mienendo yao inapaswa kuiana na taratibu zifuatazo;

> "Watu wote wanapaswa kuwa sawa kwa mujibu wa sheria".

Mhe. Mwenyekiti, kwa wakati huu tulionao hili halipo, mwenye nguvu na madaraka ndiye mwenye sheria na haya yanaoneshwa wazi wazi haya niliyoyasema sasa hivi, kwamba Nyanjale leo mwezi huu watashindwa kulipa ada za shule, watoto wao wamefaulu watashindwa kuwatafutia *uniform* na madaftari ya kuendelea kusomea kwa sababu mwezi huu wakupika dagaa wao, kwa sababu tu ya watu fulani wana *interest* zao, hapa maana yake tukufanya hivi tukitengeneza bustani, kumekorogwa korogwa, maana yake mazingira yameharibiwa huko hakuna kunachosemwa.

Mkurugenzi anasema mimi niliuzuia lakini ndio wakubwa maana yake unajua hili tatizo lako lina wakubwa hili. Ni mtihani mkubwa ni nani jamani!

Nafurahi kwamba mswada huu sasa umemtambua mpaka Rais.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, una dakika tatu malizia tunataka kuakhirisha mapema leo.

Mhe. Ashura Sharif Ali: Mhe. Mheshimiwa, zinatosha sana kabisa, nakushukuru, yaani zinanitosha kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, niwaombe wenzangu sisi wawakilishi kwa wakati huu tuko katika kipindi cha lala salama, lakini naamini kwamba wale watakaokuja kuingia hapa na wale ambao wamefanya matendo makubwa, sheria ifuate mkondo wake, mali za umma kama *Escrow* wenzetu huko tumeyaona sisi Kamati Teule tatu na nne na fedha za umma zimetumika, lakini hakuna kilichopo wameendelea mawizarani na maidarani na sisi wenyewe tunaendelea kushadidia.

Hii ni aibu kwa Taifa letu, serikali na viongozi ambao wanajali maadili na kuwatakia kheri wananchi wake.

Mhe. Mwenyekiti, niombe viongozi hisia tulizonazo katika vichwa vyetu kwa wakati huu na mawazo yale tuliyonayo tuliyotokana nayo huko, tubadilishe *mindset* zetu kuona kwamba haya mambo yanawezekana na yakifuatiliwa, Zanzibar hii itarudi ile tuliyokuwanayo mwanzo huko. Kiongozi mwema anapokuwa anaongoza katika misingi ya haki, usawa na uhuru kwa wananchi, basi neema hupatikana.

Zamani kulikuwa na mananasi mwitu leo hayapo, kulikuwa na kila kitu kinapatikana wazi wazi, tukaisema sisi wenyewe Zanzibar ni njema atakae aje, leo njoo uone tumetengeneza sheria mpya hapa kwa sababu sasa hivi hali haikuwa shuwari, ulinzi na mengineyo, hatukuwa na uwekezaji, hatukuwa na uvuvi wa bahari kuu, hatukuwa na mafuta na gesi, lakini Wazanzibari waliishi katika maisha ya salama na vizuri kabisa.

Imani yangu Mhe. Rais, atakapoitia saini sheria hii na sisi tukabadilisha *mindset* zetu, naamini kwamba yale tuliyoyazowea tukayatoa kwenye vichwa vyetu na tukayaingiza tena namna ya kufuata mswada huu, imani yangu Taifa letu litafikia pale hasa alipokusudia mwenyewe hayati Mzee Abeid Amani Karume. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, kama mnakumbuka jana kulikuwa na tangazo la kwamba leo tutakuwa na shughuli ya ufunguzi wa msikiti wetu ambayo itaanza saa 6:40. Kwa hiyo, nichukue fursa hii Waheshimiwa Wajumbe, nimuombe Waziri katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, aweze kutengua Kanuni ya muda ili tuakhirishe kikao hadi jioni.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa muda wa asubuhi bado umebaki nusu saa na kwa kuwa tuna shughuli makhsusi ya kufanya katika muda huu ili tuweze kuifanya shughuli hiyo.

Naomba kutoa hoja uliakhirishe Baraza lako kwa muda huu uliobaki ili twende tukafanye hiyo shughuli makhsusi iliyopangwa na baadae Baraza lako lirudie tena kama kawaida yake saa 11:00 jioni hii ya leo. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Wanaounga mkono hoja, wanaokataa, wanaounga mkono hoja ni wengi zaidi.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Waheshimiwa, kwa hiyo, tunaakhirisha kikao hadi jioni saa 11:00, nawashukuru sana.

(Saa 6:40 Kikao kiliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11.00 Jioni Baraza lilirudia)

Mhe. Mwenyekiti: Naangalia idadi ya Wajumbe waliokuwepo labda tusubiri kama Kanuni zetu zinavyosema tusubiri dakika tano Wajumbe wengine waweze kufika ili tuanze kikao chetu, kwa hivyo, naakhirisha kikao mpaka baada ya dakika tano.

(Saa. 11.05 Baraza liliakhirishwa kwa dakika tano)

(Saa 11.15 Baraza lilirudia)

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma wa Zanzibar wa Mwaka 2014

(Kusomwa kwa mara ya Pili)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Omar Ali Shehe: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii jioni hii nikiwa mchangiaji wa kwanza, baada ya kukushukuru nianze kwa kuipongeza Serikali kwa maamuzi yake ya kuleta Mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, ukweli ni kwamba mswaada huu ulikuwa na kazi kubwa hadi kufikia hatua hii kwa sababu haukuanza leo, mchakato wake ulikuwa ni mkubwa. Kwa hivyo, niipongeze Serikali kwa hatua hiyo kwa kuamini kwamba Mswada huu umekuja katika wakati muafaka sana, umekuja wakati ambao nchi yetu inahitaji kuwa na sheria hii. Katika miaka ya 1970 au kuanzia miaka 1960 na miaka ya 1970 mpaka 1980, maadui wa Taifa walitangazwa kuwa ni maadui wanne, kwamba kulikuwa na adui ugonjwa, njaa, maradhi na umasikini.

Lakini kwa miaka ya karibuni miaka ya 1990 amejitokeza adui mwengine ambaye ni adui wa viongozi kukosa maadili na hali hii tunashuhudia kwamba katika kipindi chote hicho cha miaka ya 1990, amekuwa ni adui mkubwa sana anayehatarisha uchumi wetu na anayeua na anayenyonya wananchi wanyonge katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali ya kawaida unaweza ukadhani nini msingi hasa wa kuporomoka kwa maadili ya viongozi, kama nilivyosema katika historia utaona kwamba jawabu rahisi inaweza ikawa kwamba ni kutokana na kuondoshwa kwa Azimio la Arusha. Azimio la Arusha ambalo liliweka misingi ya namna gani viongozi watakuwa katika utendaji wao, namna gani viongozi watasimamia uchumi wa nchi.

Lakini katika miaka ya hivi karibuni kuondolewa kwa Azimio la Arusha na Azimio lile la Zanzibar ndio unaweza ukadhani kwamba ndilo lililopelekea viongozi wengi wa umma kuondokana na maadili, lakini unapofikiri hivyo ukigeuka upande wa pili unaweza ukafikiria ni kwa nini zile nchi ambazo bado zinaendelea na siasa za kibepari, nchi ambazo hazikuwa na Azimio la Arusha, kwa nini viongozi wake wana maadili makubwa, hapo ndio utaona kwamba tatizo si hoja kuwe na Azimio la Arusha au kuondoka kwa Azimio la Arusha, hoya ya msingi ni kuweko kwa Sheria, sheria madhubuti, lakini vile vile na viongozi kuwa na nia njema ya kuwatumikia wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa msingi huo baada ya kuipongeza Serikali kwa kuleta mswada huu, nataka nitangulie kuunga mkono kwa asilimia mia moja Mswada huu. Sasa baada ya dibaji yangu hiyo nataka nijielekeze kwenye Mswada na kwanza katika kifungu hichi cha tatu, katika tafasiri wa ufafanuzi wa maneno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika neno "mali" ambapo imeelezwa katika mswada kwamba mali maana yake ni kitu chochote kinachomilikiwa na kiongozi wa umma ambacho kina thamani na kinaweza kuuzwa au kutumika kulipia deni, ni tafsiri nzuri. Lakini ukichukua hii ndio tafsiri ya neno "mali" na kwa kuwa imeelezewa katika neno tafsiri, ningelipendekeza hili kwamba isije tafsiri likagongana na maana ya vifungu.

Naomba tafsiri hii iongezewe neno kwamba mali maana yake ni kitu chochote kinachomilikiwa na kiongozi wa umma ambacho kina thamani na kinaweza kuuzwa au kutumika kulipia deni, naomba liingizwe neno kwamba "kwa mujibu wa sheria hii" neno hilo liongezwe hapo au inakiliwe hapa kwamba kama inavyoelezwa katika kifungu cha kumi na sita, kwa sababu kifungu cha 16 ndipo zilipotajwa hizo orodha za mali ambazo zinahusika na sheria hii. Kwa hivyo, pendekezo langu tafasiri iwachwe kama ilivyo, lakini iongezewe neno kwa mujibu wa sheria hii au iambatanishwe na kifungu ambacho kinahusika na sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, sheria hii ni muhimu sana na kwa sababu sheria hii ni muhimu ukiangalia jaduweli la pili, viongozi walioonyeshwa katika jaduweli la pili ina orodha ndefu sana ya viongozi ambapo imeanza na Rais wa Zanzibar na kumalizia na viongozi wengine, yaani kumalizia uteule wa Rais, idadi yao ni kama 79.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa sheria hii inaguza viongozi muhimu kuanzia Rais mwenyewe napendekeza, Mwenyekiti wa Tume hii atakayechaguliwa ni muhimu sana awekewe kinga, itakuwaje mtu huyo asiwekewe kinga tuliona udhoefu hata katika Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutokana na umuhimu wake juu ya jukumu lake analolifanya la kukagua mahisabu ya Serikali, ndio Katiba yetu ikatambua na hiyo yote imetokana na maazimio ya Kimataifa ambayo na sisi Zanzibar tumeridhia, sijui kama tuliridhia au vipi, lakini kwa vyovyote vile kwamba ni maazimio kutoka kwenye *size,* yaani *Supreme Audit Conferences* zao zilizofanyika duniani huko, baada ya kutoa Azimio lile la *LIMA* na sisi tukakubali kuridhia Azimio lile na ndio maana na sisi *GAG* wetu tukamuwekea kuwa na kinga ya Kikatiba, kwa sababu ndio maazimio ya kimataifa.

Mhe. Mwenyekiti, sasa kutokana na uzito wa Mwenyekiti na majukumu yake kwamba atapaswa kumuangalia Rais mpaka mtendaji mwengine wa kawaida, si vyema kumuacha Mwenyekiti akawa hana kinga, ni vyema tumjengee mazingira ya kuwa na kinga ili aweze kufanyakazi zake kwa umuhimu na kwa kujiamini.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 16(2), kimesema kuwa *marginal note* kuna mali zinazopangwa kutangazwa na *marginal note* 2 inasema; "Waziri atakuwa na uwezo wa kuongeza au kupunguza juu ya mali zinazopaswa kutangaza".

Mhe. Mwenyekiti, sheria hii imetangaza mali, yaani imetaja mali, sasa kama ikiwa waziri kapewa fursa hii kwamba aweze kuongeza au aweze kupunguza, mimi nadhani mlango mmoja tumfungulie na mlango mmoja tuufunge. Hizi mali zilizotangazwa zibakie kwamba ndio hizi zilizotangazwa na kama kutakuwa kuna fursa nyengine ya Mhe.Waziri kuongezwa basi apewe fursa hiyo, lakini asipewe fursa ya Mhe. Waziri kuweza kupunguza mali.

Mhe. Mwenyekiti, majukumu haya ni majukumu mazito kumpa Mhe.Waziri ambaye na yeye ni sehemu ya watumishi Mhe. Mwenyekiti, hilo litakuwa ni kosa kubwa, kwa sababu kama nilivyosema mambo haya yana miiko yake kama vile ambavyo mdhibiti kwa jukumu lake zito alilopewa, hapaswi tu Mhe. Waziri kumuingilia ingilia kirahisi majukumu ya mdhibiti, ndivyo navyo hivi kwa kweli Mhe. Waziri ambaye nae ni sehemu ya watumishi waliotangazwa na sheria hii, si vyema hata kidogo na si busara hata kidogo kumpa fursa ya kupunguza ama kuongeza, tumpe tu ile fursa ya kuongeza, lakini tusimpe fursa ya kupunguza kwa sababu na yeye ni sehemu ya watumishi ambao wametangazwa ndani ya sheria hii.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 18, kimeelezea kuzingatia miiko ya kijamii ambayo yametajwa hapa, mambo ambayo yatakuwa ni miiko ya kijamii kwa kiongozi wa umma kuweza kuyafanya ni kama yalivyotajwa hayo mambo kumi na moja, sina tatizo na hayo, lakini kuna jambo la msingi sana kwamba hayo ukiangalia yanahusu zaidi mambo ya kijamii kama yalivyoelezwa, lakini naomba niongeze neno kwamba kuwekwe na nyongeza la kiongozi anayekiuka kusimamia sheria. Kumekuwa kuna tatizo la viongozi wetu wa kutozisimamia sheria au kuzikiuka sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, naomba na hilo liingizwe liwe nyongeza katika kifungu cha 18.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 22(4) ambao msingi wake ni daftari la kumbukumbu za mali na maslahi, ambacho kinaeleza kwamba;

"Kutakuwa na daftari la kumbukumbu litakalotumika kuweka taarifa za tamko la mali".

Kifungu cha nne, kinaelezea;

"Daftari la kumbukumbu litakuwa ni siri na halitoruhusiwa kuonekana na mtu asiyehusika, bila ya ruhusa ya Waziri au kwa amri ya Mahakama".

Mhe. Mwenyekiti, nirejee tena kwamba Mhe. Waziri ambae naye ni sehemu ya kiongozi aliyetajwa, inawezakana kuwa ni kiongozi mmoja ambaye nae kahusika na makosa yaliyotajwa humu, sasa unapompa jukumu hilo, kwa kweli nadhani tutakuwa hatufanyi haki, nadhani Mhe. Waziri asipewe mamlaka haya, kwa sababu akipewa mamlaka haya huenda akaitumia mamlaka yake ndivyo sivyo kwa lile jambo ambalo litamuhusu yeye binafsi.
Sasa mimi nadhani tungelitafuta mtu mwengine ambaye kidogo kwa kiasi fulani huenda akawa hana utashi wa kulionyesha buku hili kwa mtu ambaye anayehusika. Kwa hivyo, nadhani ningeliomba Mhe. Waziri asipewe dhamana hii kwa sababu hiyo ambayo nimeitaja.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 29, kinahusu ripoti ya mwaka ya kazi za tume ambapo Waziri atatayarisha ripoti ya mwaka na kuiwasilisha kwa Rais ndani ya kipindi cha miezi mitatu baada ya mwisho wa mwaka wa fedha. Sasa ninavyofahamu kwamba kwa mujibu wa sheria hii Mwenyekiti wa Tume ambaye ni Mwenyekiti Mtendaji, huyu ndiye atakuwa *accounting officer,* kwa sababu imeelezwa katika sheria hii hii, kwamba huyu Mwenyekiti Mtendaji na kwa vyovyote vile Tume kwa mujibu wa sheria hii itakuwa ina *vote,* ina fungu la fedha,

Kwa hivyo, suala la kusema kwamba Waziri atatayarisha ripoti, nadhani si sahihi kwamba Waziri atatayarisha ripoti ya mwaka na kuiwasilisha kwa Rais ndani ya kipindi cha miezi mitatu baada ya mwisho wa mwaka wa fedha na ripoti hiyo, kifungu cha tatu kinaeleza kwamba;

"Baada ya kupokea ripoti hiyo kifungu hichi Rais atamtaka Waziri kuiwasilisha ripoti hiyo mbele ya Baraza".

Mhe. Mwenyekiti, nadhani ni mfumo ule ule kama mfumo wa *GAG* kwamba Mwenyekiti yeye ndiye atakayekuwa kiongozi wa tume, kwa hivyo, Mwenyekiti ndio awe na mamlaka ya kuandaa ripoti, kama ilivyo kwa Mdhibiri na Mkaguzi Mkuu kwamba yeye ndio mwenye mamlaka, Mwenyekiti huyu aandae ripotim Mwenyekiti mwenyewe ampelekee Mhe. Rais na Mhe. Rais ampe Mhe.Waziri kwa ajili ya kuileta katika Baraza hili.

Lakini kusema kwamba kule kuna Mwenyekiti, Mhe. Waziri yeye ndio aandae ripoti, mimi nadhani Mwenyekiti, hapa panahitaji mabadiliko na mabadiliko yawe kama hivyo ninavyopendekeza kwamba Mwenyekiti, kwa sababu yeye ndio mkuu wa Tume, ndiye mtendaji wa Tume, yeye awe na Mamlaka ya kuandaa ripoti, Mwenyekiti awe na mamlaka ya kumpelekea Rais na Rais katika muhtadha wa kuileta katika Baraza hili, ndio ampe Waziri wake kwa ajili ya kuja kuiwasilisha katika Baraza hili.

Nadhani Mhe. Mwenyekiti, naomba nishauri hivyo katika kuleta ule uwajibikaji mzuri na usio na mashaka kwa tume na taasisi nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 34(1), kinaeleza kwamba;
"Tume itakuwa na fungu lake la bajeti...",

Mhe. Mwenyekiti, ndio hilo nililokuwa nazungumzia, kwamba Tume hii ina fungu lake la bajeti ina *vote,* sasa kwa vile ina *vote* maana yake kwamba kifungu cha pili kimesema kwamba mlipaji mkuu wa Serikali atateua Afisa Mhasibu atakayesimamia fungu la bajeti la Tume na Mhasibu Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa sheria hii.

Sasa uzoefu uliopo au tunaokwenda nao hivi sasa ni kwamba *PMG* ambaye ni *Pay Master General* katika Wizara za kawaida huwateua Makatibu Wakuu kama ma-*accounting officers* au wale wakuu wa Idara kwa zile idara ambazo zinajitegemea kuwa wo ndio ma-*accounting officers. S*ina shaka kwamba kifungu hichi kimekusudia kwamba *PMG,* sina shaka ingawa hakutajwa hapa, lakini kwa vyovyote vile itakavyokuwa kwamba *PMG* atamteua

Mwenyekiti, kwa saabu yeye ndio mtendaji kuwa ndio *accounting officer,* hilo sina tatizo nalo, kwa sababu ndio uzoefu unavyoonyesha katika Taasisi za umma zinavyokwenda.

Mhe. Mwenyekiti, na kama hivyo ndivyo basi, kifungu cha 37, naomba hicho kifungu cha 34 nihamishe hoja yangu katika kifungu cha 37 ambapo inasema ripoti ya mwaka, sheria inasema;

"Mwenyekiti atatayarisha ripoti ya mwaka...".

Mhe. Mwenyekiti, na ndio tunakubaliana kwamba Mwenyekiti atatayarisha ripoti ya mwaka kwamba ni huyu ambaye tayari kateuliwa na *PMG* kuwa ndio *accounting officer*, kwa sababu hawa kawaida ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha ndio anayewateua, sina tatizo na hilo na ndio maana kifungu cha 37 kikasema kuwa Mwenyekiti ataitayarisha ripoti ya mwaka, hamna tatizo ni kwamba;

"Mwenyekiti atatayarisha ripoti ya mwaka kwa kila mwaka wa fedha na kuiwasilisha kwa Waziri ndani ya kipindi cha miezi mitatu bada ya mwisho wa mwaka wa fedha".

Mhe. Mwenyekiti, mimi hapa nina *problem* kwa sababu hii itakuwa ni taasisi ambayo ina fungu, kwa mujibu wa sheria ya fedha, huu utakuwa ni ufungaji wa mahisabu ya mwisho wa mwaka, kitendo hichi tafsiri yake itakuwa ni ufungaji wa hisabu za mwisho wa mwaka ambapo sheria imetaka baada ya mwisho wa mwaka, kila Idara na taasisi za umma zina miezi mitatu ya kufunga hisabu zake. Tatizo langu liko katika maelezo kwamba Mwenyekiti ataiwasilisha kwa Mhe.Waziri ndani ya kipindi cha miezi mitatu baada ya mwisho wa mwaka wa fedha.

Mhe. Mwenyekiti, hili nadhani ni tatizo kwamba *accounting officer* yeyote kwa mujibu wa sheria ya fedha hufunga mahesabu na kuyawasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hisabu za Serikali, hapaswi tena huyu kwenda kumpa Mhe. Waziri katika kuomba bajeti kwa sababu hichi ni kitengo ambacho kimo ndani ya Wizara, sina tatizo kwa sababu mwisho wa siku bajeti ya taasisi hii atapaswa Mhe. Waziri aiwasilishe hapa, hilo halina tatizo na ndio tunavyokwenda.

Lakini kwa suala la ufungaji wa mahisabu inatakiwa kila taasisi yenye fungu ifunge mahesabu na kuwasilishwa kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, sasa isije *contradiction* kama inavyoonekana kuna *contradiction* siku hizi, kwa sababu hata ukifungua ripoti za mdhibiti nyingi utakuta taasisi fulani haiwasilishi mahesabu, lakini ukweli ni huo, ukweli unapokwenda wakati mwengine kwenye taasisi unakuta zinafunga mahesabu, tatizo linalojitokeza badala ya kumpelekea mdhibiti kama sheria inavyotaka, wao huzichukua hesabu zile za kuzipeleka wizarani na wakizipeleka wizarani hukwama kule, ndio mdhibiti akaandika hoja.

Sasa nataka nieleze hivi katika kutahadharisha kwamba hichi kifungu kwanza kinapingana na sheria ya fedha, kwa sababu sheria ya fedha inasema kwamba;

"Kila *accounting officer* atafunga mahesabu ya kila mwisho wa mwaka na kuyawasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na sio Waziri anayehusika".

Mhe. Mwenyekiti, mwisho naomba niseme kwamba katika jadueli wametajwa viongozi hapa, kuna orodha kubwa ya viongozi kama nilivyotaja awali kwamba kuna viongozi 79, lakini kuna mtu mmoja hapa simuoni kiongozi mmoja muhimu sana masheha wetu. Masheha hatuzungumzi suala la mshahara tunachozungumza ni suala la mamlaka ya mtu katika kuwatumia watu. Ikiwa hivi ndivyo kwamba tunazungumzia kiongozi mwenye ku-*deal* na watu kushughulika na watu kutoa huduma kwa watu, maana yake na masheha nao pia nao wanaohusika na hili.

Mhe. Mwenayekiti, sheria tulizozipitisha juzi masheha hawa ndio walioko kwenye watu na ndio wanaotoa huduma kwa watu mara nyingi. Sasa kwa yale mambo ambayo yanahusiana suala la ukosefu wa maadili, naomba sana umuingize sheha hapa kwa sababu huduma nyingi kwa wananchi zinatolewa na Mhe. Sheha na yeye ni kiongozi muhimu na ni kiongozi mkubwa kwa watu wetu huko katika vijiji. Kwa hivyo, naomba naye kwa sababu ya dhamana hiyo aliyonayo kwa wananchi naomba tumuingize katika orodha hii ili nawe awe ni sehemu ya viongozi ambao sheria hizi zitakuwa naye zinamuhusu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimalizie kwamba niipongeze tena Serikali kwa kuleta mswada huu, lakini naomba nikumbushe suala la kupitisha sheria na kuwa na sheria ni kitu kimoja na suala la kutekeleza sheria ni suala jengine. Tunaweza hapa tukaipitisha sheria hii kwa mbwembwe kubwa, lakini *application* yake isionekane.

Na isionekane kwa sababu ni uzoefu wetu kwamba tunaunda sheria na tunaunda Taasisi, lakini ukweli ni kwamba miaka inakatika hukuti matayarisho wala hukuti kuwa na utekelezaji wa aina yoyote. Tumeunda na Tume ya Rushwa, leo tukiuliza Tume ya Rushwa iko wapi inafanya shughuli gani, kazi zake ziko wapi, sidhani kama kutakuwa na Mhe. Mwakilishi yeyote aliyekuwa na *reference*.

Mhe. Mwenyekiti, tuna mabodi huko chungunzima tumeyaunda lakini hatuoni utekelezaji wake.

Sasa naomba sana kwa umuhimu wa sheria hii kama walivyosema wenzangu nami naomba niwaunge mkono kwamba kuna haja ingawa sheria hii ina nia njema na sisi viongozi wote tunapaswa sasa tubadilike kwa mujibu wa ujio wa sheria hii kwa sababu ukiisoma hii sheria yenyewe ilivyo, basi kila mmoja kama hana roho ya kijasiri anaweza akaikataa.

Kwa sababu kwa kweli ni mwanzo mpya ambao wa kufunga milango ya demokrasia na milango ya haki katika nchi yetu, kwa hivyo, msisitizo wangu katika sheria hii ni kwamba Serikali ijitahidi sana katika utekelezaji wake kwani itakapotekelezwa ipasavyo, kutakuwa lile suala na kilio cha wananchi kwa muda cha kwamba viongozi kujifanya waungu watu nadhani huu ndio muarubaini watu.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu, ingawa mchango wangu utakuwa mdogo sana kwa sababu ya afya na pia kwa maidha yako uliyonipa baada ya kuahirisha kikao cha asubuhi. Mhe. Mwenyekiti, na ingelikuwa ulikuwa hujalitaja jina langu basi ningekuandikia kimemo kutokana na mawaidha mazito niliyopata ya kuachia wenzangu waendelee kuchangia.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze mchango wangu katika ukurasa wa 56, kifungu cha 5(1), kifungu hiki kinaeleza muundo wa Tume na hapa tumeambiwa kwamba Tume itakuwa na Mwenyekiti na Kamishna wawili. Sasa naomba nipate ufafanuzi naona huu muundo ni mdogo sana na hofu yangu hapatakuwa na ufanisi, je, hii ndio kawaida ya Tume za aina hii zinavyokuwa. Lakini vile vile, naomba niende katika kifungu cha 7 (2), hapa pametajwa mtu asiye na tabia au mwenendo wenye kutiliwa shaka na jamii.

Naomba niipongeze sana Kamati kwa kukiona kifungu hiki kwa sababu kwa jamii yetu tuliyonayo kila mtu, kila kundi la watu lina mtazamo wake, kwa hivyo, hiki kifungu kingeliwachwa hivi, nadhani tusingelipata Mwenyekiti. Kwa sababu kutiliana shaka imekuwa ni jambao la kawaida.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, naomba niende katika kifungu cha 9, kifungu hiki kimeeleza sifa ya Kamishna wa Tume. Naomba nikinukuu hiki kifungu, kinasema;

"Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Kamishna ikiwa ana sifa zilizotajwa katika kifungu cha 7, isipokuwa kifungu cha 7(1)(b)".

Mhe. Mwenyekiti, ikiwa Kamishna atakuwa na sifa zilizotajwa kifungu cha 7, isipokuwa kifungu cha 7(1)(b), ni vyema kifungu cha 9 kitaje sifa ya elimu ya Kamishna ili Mwenyekiti apate watu wenye uzoefu na maarifa ya kumsaidia. Lakini vile vile, katika kifungu cha 18(1) kimetaja kiongozi wa umma ajiepushe miongoni mwao na ulevi wa kupindukia.

Mhe. Mwenyekiti, pia, hapa napenda niipongeza Kamati kwa kukiona kifungu hiki, kwa sababu tungelikwenda na ile ile kama kiongozi wa umma ajiepushe na ulevi wa kupindukia ina maana kiongozi angeliruhusiwa kuwa mlevi. Na sheria hii tungeliona imekopiwa kwenye jamii ambapo ulevi ni jambo la kawaida.

Mhe. Mwenyekiti, wazanzibari ulevi ni ila, sio sifa njema. Kwa hivyo, naipongeza sana Kamati kwa kuliona hilo.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, katika kifungu cha 18(3) kimetaja kiongozi wa umma atatakiwa kuepuka kauli za kibaguzi. Mimi hapa naona sio kauli tu za kibaguzi, bali kiongozi wa umma aepuke kauli za kibaguzi na vitendo vya kibaguzi. Kwa sababu anaweza akawa mtu asiwe na kauli za kibaguzi, lakini vitendo vyake vikawa ni vya kibaguzi. Na kwa kweli vitendo hivyo vikaleta athari sana kwa jamii na hii hata hapa petu wananchi wengi wanalalamikia vitendo vya kibaguzi kwa mfano kwenye ajira, *Zan ID*, vitambulisho vya kura na nafasi za masomo.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, kifungu hiki nashauri iwe kiongozi wa umma aepuke kauli za kibaguzi na vitendo vya kibaguzi. Kwa kusema kauli za kibaguzi tu ni kuwa watu watajificha kusema lakini vitendo wataendeleza, kwa hivyo, mimi nashauri hapo pawe hivyo.

Lakini vile vile, naomba nimalizie kwa kuuliza, je, Serikali iko tayari na sheria hii? Na vile vile, je, Serikali yenyewe na hasa viongozi wa Ofisi za Serikali wameshajitathmini kauli zao na vitendo vyao?

Mhe. Mwenyekiti, jem viongozi wa Serikali wameshausoma huu mswada na kuuelewa na jem viongozi wote tuko tayari kwa matokeo ya utekelezaji wake?

Mhe. Mwenyekiti, mimi ushauri wangu kama kweli sheria itakayotokana na mswada huu tunataka kuisimamia, hatuna budi kwanza kuelimishana juu ya sheria hii jambo ambalo halijafanyika na hasa ukizingatia wadau wa sheria hii ni wananchi wote. Kwa hivyo, ni vizuri hapa pakatolewa elimu juu ya sheria hii. Ikiwa hapajatolewa elimu kwa kweli kutakuwa hakuna litakalokuwa na itakuwa ni ile ile hali ya kawaida tuliyoizoea.

Mhe. Mwenyekiti, la pili, tunapaswa tuondokane na muhali jambo ambalo hapa kwetu ndio nguo yetu. Lakini la tatu, la kumalizia utekelezaji na usimamizi wa sheria hii usiangalie kwa miwani yenye jicho la itikadi ya kisiasa jambo ambalo ndio ugonjwa wetu.

Mhe. Mwenyekiti, sidhani kwamba tuko tayari. Tunahitaji kuelimishana na kwa pamoja tushirikiane katika usimamizi wake.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi nashukuru kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi nizungumze machache katika mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa niende katika madhumuni na sababu ya mswada huu. Naomba ninukuu madhumuni na mswada na sababu ya mswada huu ni "Kupendekeza kutungwa kwa sheria ya maadili ya viongozi wa umma kuanzishwa Tume ya Maadili ya uongozi, baada ya kutungwa kwa sheria ya rushwa na uhujumu uchumi, Serikali imeamua kuwasilisha mswada huu ambao utasimamia maadili ya viongozi wote hapa Zanzibar waliotajwa kwenye jadueli la mswada huu".

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilete shukurani kwa Mhe. Waziri na watendaji wake wote ambao wamekaa na kufikiri kwa muda mrefu wakaona watuletee mswada huu, kwa kweli ni mswada wenye maana kubwa sana kwetu.

Mhe. Mwenyekiti, nimeyasema madhumuni na sababu hii kutaka kujua kwamba kama madhumuni umekusudia viongozi basi na viongozi wenyewe wakatajwa katika hii orodha, basi hatuna sababu ya viongozi sisi kuwanyooshea vidole labda viongozi wenzetu wengine, tukijua sisi wenyewe wote humu ndani ni viongozi, vile vidole vilivyobaki vinatuelekea na sisi.

Mhe. Mwenyekiti, tumekuwa tukisema sana hapa labda tunainyooshea kidogo Serikali kwamba labda inafanya sivyo au inafanya mambo yake kinyume, lakini tusijisahau na sisi viongozi tuliomo humu ndani kwa kuwa sheria hii imeletwa basi niseme imekuja kuturekebisha wote.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, sheria hii tutakapoifata na kuzingatia yale yote ambayo yameletwa hapa mbele yetu nahisi wajumbe wenzangu waliotangulia walisema kama kisiwa chetu kitaweza kupiga hatua moja nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, mswada huu umeeleza kila kitu na umeeleza mambo mazuri juu yetu, isipokuwa Mwenyezi Mungu atupe nguvu, hekima na busara ili tuweze kuifata sheria hii tupate mafanikio mema. Na haya yote yatakuwa

tunakwenda kama wenyewe tunavyojisifia kama asilimia 99 ni waislamu na katika uislamu hakukubakishwa kitu. Mwenyezi Mungu alitwambia katika kitabu chake kitukufu kwanza tumtii yeye, tumtii na Mtume (*S.A.W*) wake, lakini tuwatii na wale viongozi wakaopata nafasi miongoni mwetu.

Kwa hivyo, sasa Mhe. Mwenyekiti, tukianza kujiheshimu sisi wenyewe, lazima tutaweza kuheshimu na wengineo. Lakini tukiona sisi wenyewe tunajivunjia heshima basi tuelewe kutakuwa hakuna mwengine wa kutuheshimu. Kwa hivyo, mimi nisisitize ukitaka kusema aibu ya mwenzako basi unatakiwa uiseme aibu yako wewe mwenyewe kwanza.

Mhe. Mwenyekiti, sisi wenyewe tujiangalie kama Wawakilishi ikesha kuwa tumepata hizi fursa na kinga basi pia huwa tunazitumia vibaya. Mhe. Mwenyekiti, tunajenga kiburi hata hizo sheria tunafikia kuzivunja na sisi. Kwa hivyo, basi tusiwaone wenzetu tu tukawaelekea vidole wenzetu, kwa hivyo, tujuwe na sisi miongoni mwetu tunayatenda makosa hayo. Kwa kuletetwa sheria hii sasa tunatakiwa wote tujirekebishe ili tuweze kwenda sambamba na mswada huu.

Mhe. Mwenyekiti, sisi ni viongozi na viongozi tuna jukumu kubwa kwa wale ambao tunawaongoza. Tuna jukumu kubwa kwa mwenyewe Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataala* vile tutakavyokwenda kinyume na utaratibu ambao yeye ametupangia na sisi ni viongozi lazima tuelewe wajibu, majukumu na mipaka yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kiongozi hupaswa kabisa kutumia chombo hiki ukatia lugha za uchochezi, yaani kuwachochea watu, kutamka maneno ambayo yataashiria kichocheo cha kuleta athari katika nchi yetu. Tunapaswa sisi tutumie vizuri kauli zetu kwa sababu tunasikilizwa na wengi. Kwa hivyo, tunapaswa tunapozungumza kauli zetu Mwenyezi Mungu atujaalie tuweze kuzichunga ili tuepukane na hayo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilitaka nichangie katika haya majadueli, kuna jadueli hili la pili ambalo kwa mujibu wa sheria ya kifungu cha Katiba cha 36 cha Katiba yetu ya Zanzibar ya mwaka 1984, Rais hatashtakiwa akiwa madarakani na katika jadueli la pili sheria inamtaka Rais atangaze mali zake na asipofanya hivyo, atakuwa ametenda kosa kwa mujibu wa sheria hii. Je, Tume itakuwa na mamlaka gani ya kumshtaji Rais endapo atashindwa kutekeleza masharti ya sheria hii wakati Katiba ya Zanzibar inamlinda Rais dhidi ya mashtaka yoyote.

Mhe. Mwenyekiti, pia, niende katika kifungu cha 42, kifungu hiki cha mswada wa maadili kinamtaka waziri baada ya kushauriana na Tume kufanya marekebisho katika jadueli lolote la sheria hii. Mimi napendekeza pia kuwepo na kifungu chengine ambacho kitaipa mamlaka Tume baada ya kushauriana na Rais kumwita mtumishi watakaemuhitaji ambaye hayupo katika jadueli la pili kutoa taarifa za mali yake.

Mhe. Mwenyekiti, pia, niutoe tu ushauri wangu wa kuona ni Tume nyingi tumeshaziundwa na tukapitisha hapa kupitia Baraza lako hili, lakini maandalizi yanakuwa hayapo. Niombe sasa kupitia Baraza lako hili tukufu kwamba Tume hii ambayo inakusudiwa kuundwa basi lazima iwe na mahala pake pazuri pakufanyia kazi kwa sababu hiki nacho ni chombo kikubwa.

Mhe. Mwenyekiti, si vyema Tume hii ikaja ikatanga tanga na ikawa haina maeneo muhimu ya kufanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, pia, nikenda katika kifungu cha 18(2), hapa pia mimi ningeshauri penye maneno yanayosema naomba ninukuu;

"Kiongozi wa umma hatakiwi kujihusisha na vitendo vya jinai ikiwa pamoja na utapeli, wizi na ubakaji".

Mhe. Mwenyekiti, mimi ningeomba haya maneno mengine tuyafute ili haya maneno utapeli, wizi na ubakaji basi tuweze kuyaonesha katika hivi vifungu vyengine ambavyo vipo juu hapa ili yaweze kuonekana na tusiwe tumeyaficha kama hivi yalivyo. Tungefuta ili haya maneno utapeli, wizi na ubakaji tukaweza kuingiza katika hapa ikaonekana *specific* kwamba haya nayo yanaonekana ni mambo muhimu mtu hatakiwi awe nayo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sina mchango mkubwa sana, sina hasa maana yake hizo *points* zimeshazungumzwa na wengi, mengi ambayo nilitaka kuyazungumza naona wenzangu wengi wameyazungumza. Isipokuwa niungane na wenzangu katika kuunga mkono mswada huu kwa asilimia mia kwa mia na niombe wajumbe wenzangu tuweze kuunga mkono mswada huu tukijua kwamba viongozi tunatakiwa kuchunga miiko na maadili ya uongozi wetu.

Kwa hiyo, huo mswada utakuwa ni mmoja ambao unatuchunga chungam ni kama vile unapotaka kuswali na kutia udhu, kila ukijua udhu umetoka basi unakimbilia kuweka udhu mwengine.

Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekitim hii itatusaidia sana na *Inshaallah* tuwaombe viongozi wetu hili sasa liweze kutekelezeka kwa sababu mara nyingi mambo yanakwama katika utekelezaji. Hili tulitekeleze ili kwa manufaa yetu sisi ambayo yatatuweka viongozi kuwa katika maadili mazuri na ndivyo Mwenyezi Mungu anavyopenda tufanye kazi kwa uadilifu kama alivyotuagiza, basi *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atujalie viongozi wetu Mwenyezi Mungu awape hekima na busara tuweze kuyatekeleza haya kwa mafanikio yetu na wananchi wetu kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru. (*Makofi*)

Mhe. Ali Mzee Ali: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nakushukuru sana kunipa nafasi hii na hasa kwa kuwa ndio nitafunga dimba hili. Leo ni siku ya Alhamis, Baraza la Wawakilishi lilianzishwa tarehe 14 Januari, 1980, wakiwepo wajumbe 109, Baraza la mwanzo lilianza na wajumbe 109. Kwa bahati nzuri katika wajumbe 109 ni mjumbe mmoja tu ambaye alikuwepo siku hiyo na leo yupo ni ndugu yetu, mwenzetu Mhe. Ramadhan Abdallah Shaaban, anastahiki kila sifa kwa kuwa ni mzee wa Baraza hili. (*Makofi*)

Lakini leo tena baada ya tangu mwaka 1980 leo Baraza la Wawakilishi limefungua msikiti, nayo hiyo ni historia kubwa kwa leo Baraza la Wawakilishi limefungua msikiti wake nayo hiyo ni historia ambayo na wewe Mwenyekiti unakuwemo katika historia hiyo kwa sababu unasimamia na hayo unayaweka sawa. Kwa nini nikasema historia na msikiti?

Nakumbuka wakati tuko kule Mnazi Mmoja Mwakilishi Said Ali Mbarouk alikuwa anachangia na anamtaja Hafidh Ali, tulikuwa tunasali nje tu pale na mimi nilikuwa ndiye Mwenyekiti wa Baraza. Hafidh Ali aliichukua ile akasema Mhe. Mwenyekiti, nimemsikia Said Ali Mbarouk wakati mnasali, sala imevunjwa kaja kumjibu, leo haiwezekani kuna msikiti, kuna nini. Kwa hivyo, hayo ni mafanikio.

Mhe. Mwenyekiti, lakini sasa tuje katika maudhui ya mswada huu, Mswada wa Maadili.Kwanza nataka niwapongeze Wawakilishi wote waliochangia wameukubali, wameushauri na namuomba Mhe. Waziri, ayachukue yote na ayafanyie kazi. Wengi waliochangia wameuliza, je, serikali iko tayari, je, sisi tuko tayari? Huo ni wasi wasi, lakini nataka niwatoe wasi wasi. Sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ndio wenye dhamana ya kusimamia maadili kwanza sisi wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, tarehe 8 April, 2006, Makamu wa Rais Ali Mohammed Shein, alikuja kutuhutubia Baraza la Wawakilishi kwenye semina, kwa bahati mbaya wengi waliokuwepo siku ile leo hawapo, yaani wengi ni wapya. Lakini katika semina ile hii hapa hotuba yake alisema; "Nimeelezwa kwamba mafunzo hayo yataanza leo yataendelea kwa muda wa siku tatu na yatahusisha Katiba ya Zanzibar, Katiba ya mwaka 1984, maadili, uwajibikaji wa Wawakilishi na mengineyo".

Sasa mimi nazungumza hii maadili na uwajibikaji wa Wawakilishi. Tulifanya semina hiyo lakini matokeo yake hayajaonekana. Nichukue nafasi hii kumpongeza Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein na serikali yake kwa kuweza kuletwa mswada huu wa maadili kikamilifu na kwa kufanya hivyo ndio anatekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Sasa maadili ni nini? Neno "maadili", neno hili ambalo kwa lugha ya kiingereza linaitwa *ethics* limeelezwa kama ifuatavyo kwenye *Oxford Advanced Leaners Dictionary, Fifth Edition. Moral principles that govern or influence a person's behavior*. Tafsiri ya kiswahili tunaweza kusema ni tabia au mwenendo unaotawala au kushawishi maisha ya mtu, ndio maana ya maadili.

Mwaka 1979, Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1979, kifungu cha 26 kinasema hivi;

"Kila Mjumbe Mwakilishi anayehusika na masharti ya Ibara hii atatakiwa kuwasilisha kwa Spika wa Baraza la Wawakilishi nakala mbili za taarifa rasmi ya maelezo ya mali yake na kadiri itakavyokuwa mali ya mke wake, wake au mume wake. Taarifa hiyo itatolewa kwa kutumia fomu maalum itakayotumika

kwa kazi hiyo kwa mujibu wa Katiba hii. Masharti ya Ibara hii yanatumika kwa kila mjumbe wa wawakilishi isipokuwa Wakuu wa Mikoa".

Hiyo ni mwaka 1979, si jambo jipya hili.

Mhe. Mwenyekiti, lakini Ibara ya 29(5), Spika anatakiwa kuwasilisha kwa Mwenyekiti wa Mapinduzi na Rais wa Zanzibar nakala mbili za taarifa rasmi ya maelezo ya mali ya huyo Spika na kadiri itavyokuwa; mali ya mke wake au mume wake, mfano walimtabiri iko siku watakuwa wanawake na leo uko wewe Mwenyekiti, siku hizo ingebidi upeleke mali ya mumeo.

Kwa ajili hiyo na kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi na atatoa taarifa namna hiyo mara kwa mara. Lakini yote haya yamo ndani ya Katiba, lakini mwaka 1984 katika Baraza lako tukufu kikao cha Machi, 1984 ilisema;

> "Mswada wa Sheria wa Kurebisha Katiba ya Zanzibar".

Kwa hivyo, haya yote yalirekebishwa na yakiwa ndani ya Katiba. Kwa hiyo, Katiba ya Zanzibar sasa hivi haizungumzi maadili.

Mhe. Mwenyekiti, lakini sisi ni Wawakilishi tunayo maadili, ukitizama katika kinga katika kifungu cha 33 kwenye Kanuni utaona "*any member who offer*s" yaani mtu ambaye anatoa na anapokea rushwa yote haya tumekatazwa.

Ukienda katika kifungu cha 49, kinazungumzia. "*A member shall in addition with duties provide under section 88 of the constitution of the following duties and obligations:-*

a) *To guard the integrity of the House and its Committees and not involving himself in willful disobedient act, that would bring the House or its committee into ridicule; and*

b) *To use sitting of the House and committee to defend the rights and interest of the citizens in accordance with the provisions of the Constitution, the Constitution of United Republic of Tanzania 1977 and national ethics".*

Sasa haya yote mambo mazuri, lakini mimi sikumbuki Baraza la Wawakilishi kuita Kamati ya Maadili na kifungu 119 ipo Kamati ya Maadili ya Baraza. Nakumbuka mara moja tu Kamati ya Maadili iliitwa baada ya Mhe. Haji Faki Shaali, mimi kumtaka aombe radhi, atoe ufafanuzi na alikataa akamuandikia Spika kama Mwenyekiti amekwenda kinyume na utaratibu. Kwa hivyo, Kamati ya Maadili ikaitwa na ikafanya kazi yake na hatimae maamuzi yake ikawa Mwenyekiti amekosea.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nawaomba Wajumbe tuipitishe sheria hii yote tuliyoyasema haya, hayafanyiki na hayatendeki kwa sababu hakuna maadili, tupitishe. Kazi ya Baraza ni kupitisha sheria na kusimamia serikali. Sasa tuipitishe sheria hii na mimi namuomba Mhe. Rais, wako watu wake bali mimi si mwanasheria anayasikia, tukiipitisha tu sheria hii Rais ai-*sign* na akishai-*sign,* afanye kila njia aunde hiyo Tume.

Lakini naamini Mhe. Rais hiyo Tume atakayoichagua itakuwa Tume ya watu waadilifu na wenye uzoefu ili iweze kufanya kazi. Yote niliyoyasoma yalikuwa yanahusu Wawakilishi, lakini sheria hii inahusu Wawakilishi, wafanyakazi wa serikali, viongozi wa serikali. Kwa hivyo. itiwe saini itumike na hapo sasa sisi kama Baraza kwa mujibu wa Katiba kifungu cha 88. Baraza la Wawakilishi pamoja na kuongoza shughuli zake kutokana na vifungu vya Katiba hii itafanya kazi kwa mambo yafuatayo:

Kutunga sheria pale ambapo utekelezaji wa jambo linahitaji kuwepo kwa sheria hiyo;

Kujadili shughuli za kila wizara;

Kuuliza masuala; na

Kuidhinisha mipango ya maendeleo ya serikali na kuisimamia serikali. Ni wajibu wetu.

Mhe. Mwenyekiti, Baraza la Wawakilishi lilipoanzisha liliitwa ni ngome, sasa Baraza la Wawakilishi linapewa silaha ndani ya ngome, ngome yenyewe ndio hii sheria ya maadili, lazima tuipitishe na tufanye kazi. Watu wamesema kwenye ardhi, sijui sheria hazifuatwi, sheha, ndugu yangu Hamad Masoud anasema amekwenda yeye na waziri mpaka Pemba na wamefuatilia, lakini sheha hajafanya chochote. Mwengine anasema hivi, yaani kila mtu anasema yake, sasa tupitishe sheria ya maadili ili tuweze kuhoji na tuweze kuuliza. Lakini sheria hii ya maadili inazungumza pasiwe na ubaguzi, hakuna kitu kibaya kama ubaguzi.

Mhe. Mwenyekiti, Sheria Nam. 6 ya mwaka 1964 inasema hivi;

"Kwa kutekeleza uwezo aliopewa na sheria, uweze kutunga sheria 1964, Rais wa Jamhuri ya Zanzibar kwa kushauriana na kukubaliana na Baraza la Mapinduzi ametunga sheria hii, sheria imejuulikana kama Sheria ya Usawa, Maridhiano, Umoja wa watu wa Zanzibar wa 1964. Madhumuni makuu ya Mapinduzi ya Watu wa Zanzibar ni kutokomeza upendeleo wa kiuchumi, kijamii au upendeleo wa kisheria na mapungufu yote yaliyopita yaliyokuwa yanawagawa wananchi na makundi mbali kwa raia kwa njia ya ukabila, jinsia, dini au uasili wa mtu. Na madhumuni hasa ya Mapinduzi ni kukuza usawa, maridhiano, umoja wa watu wa Zanzibar. Kwa msingi huo kila raia wa Zanzibar..." Wakati huo tulikuwa na uraia wetu wa Zanzibar "...anatangazwa kuwa na haki sawa, fursa na hifadhi ya uraia wake kama vile ambavyo anatekeleza majukumu na wajibu wake wa uraia.

"Hakuna haki, fursa au hifadhi inayoweza kufutwa kisheria kwa yeyote kwa kutumia vyombo vya dola au kwa kutumia hatua za mtu binafsi kwa sababu ya misingi ya kisingizio cha ukabila, dini, jinsia, uasili na raia huyo. Hakuna kifungu chochote ndani ya sheria itakayozuia serikali kutunga sheria itakayotoa nafuu maalum au upendeleo kwa kiuchumi, kiutamaduni au kijamii kwa raia aliyekosa haki ya msingi kwa madhumuni ya kutuletea sawa".

Haya ndio madhumuni ya Mapinduzi kwa mujibu wa sheria.

Sasa tunaposema Mapinduzi Daima, haya ndio ya kutekeleza. Sasa haya yanapovunjwa, tutakwenda kwenye maadili na kwenye maadili imezungumza juu ya kuvunja haki za binadamu, haki za ukabila. Kwa hivyo, narudia tena naomba sana ndugu zangu tuupitishe mswada huu kwa moyo wetu.

Vile vile, nataka nimpongeze Dkt. Mwinyihaji amebahatika kwa kuwa leo yeye ni Waziri Ofisi ya Rais, wakati Mhe. Rais anazungumza kwenye Sherehe za Miaka 51 kwa mara ya mwanzo mimi nimesikia Baraza la Wawakilishi linapewa pongezi. Rais anasema nawapongeza; "Baraza la Wawakilishi kwa kupitisha miswada 54", ni mara ya mwanzo nimesikia mimi katika maisha yangu niliyokwenda Sherehe za Mapinduzi. Sasa Baraza la Wawakilishi sisi tunapongezwa, lakini miswada 54 tumeipitisha.

Mhe. Mwenyekiti, juzi hapa anasema waziri sheria ya mwaka 2002 ndio sasa hivi inafanyiwa marekebisho ya Kanuni, haya mambo yasite mara moja. Sasa serikali na mawaziri wahakikishe Kanuni zinazopitishwa wazipitishe ili tuweze kufanya kazi , bila ya Kanuni ni tabu.

Sasa watu wamesema mengi sana, mimi nilitaka nimpongeze Mhe. Hamza Hassan Juma. Mhe. Hamza Hassan ni Mwenyekiti wa Wenyeviti, kwa kweli ameumia sana siku tatu hizi tulikuwa na miswada mitatu kwa Kamati yetu mpaka usiku, lakini Mhe. Hamza Hassan ana nguvu, saa tano usiku asubuhi tayari ripoti, hii tabia ya Mswada wa Dharura, maana ya dharura ni jambo haliepukiki.

Sasa tupunguze dharura kwa sababu tunaona leo watu wengi wanapiga piga *brush brush* tu, kwa sababu muda wa kusoma hasa ulikuwa hamna. Sasa tumejitahidi na tumepitisha na bahati mbaya ningefanya nafasi mchana leo ya kuzungumza ningesema Mhe. Hamza Hassan, Mwenyekiti wa Wenyeviti, aongezewe cheo awe yeye sasa ndiye Imamu Mkuu wa Msikiti wetu kwa ajili ya Wawakilishi tu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa makofi hayo inathibitisha limekubalika, Mhe. Hamza Hassan, vaa joho na koti lako Mwenyekiti wa Wenyeviti, Imamu wa Baraza la Wawakilishi, Baraza la Wawakilishi tu, sio Kwa Mtipura, aa! *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, katika Mswada huu, kifungu cha 43 kuna orodha refu ya watu wametajwa kama; Rais, mawaziri, watu chungunzima wametajwa na waziri ana mamlaka ya kuongeza watu, sio kama mwisho hapa. Kwa hivyo, wale waliotoa mawazo waziri atayapokea akiona ataongeza na ile Mahakama Maalum sisi kama Kamati tumefuta. Lakini, je, hawa watu wa tume wakishaapishwa wao hawajatajwa, wao wanawajibika wapi? Rais anapeleka kwao, kila mtu anapeleka kwao, je, wao?

Wakati binadamu wote wameshatolewa roho, miti ishaundwa kama malaika, Mwenyezi Mungu atamwambia malaika wake bado mmoja, atazunguka asema nishamaliza, anaambiwa bado mmoja, nishamaliza wote, anaambiwa hapana, atabaki yeye na mwisho na yeye itabidi ajimalize. Sasa hawa, je, watakwenda wapi?

Sasa kifungu cha 43, Mhe. Waziri, kifungu cha 41 kinampa waziri mamlaka ya kutuga Kanuni, hiyo mimi sina tatizo nayo, lakini kifungu cha 43, kinasema;

"Waziri ataweka utaratibu utakaowezesha Mwenyekiti na naibu wake kutangaza mali zao".

Kwa hivyo, Rais akishasaini tu, Mhe. Waziri Dr. Mwinyihaji Makame, kitekeleze na naamini bado utakuwa waziri wewe, tekeleza utaratibu kwa hawa jamaa maalum kuwa na wao wanawajibika wapi.

Waheshimiwa kikao cha Machi kitakuwa ni kirefu kidogo, tutakuwa na ripoti za Kamati, naomba Baraza la Wawakilishi kuhusu ripoti za Kamati, kwamba Kamati tatu siku moja, sio sawa kabisa. Tunataka kwenye ripoti za Kamati twende tukaulize tukajue hizi Kanuni zinapitishwa vipi. Nawaomba Wajumbe wa Kamati mbali mbali tufuatilie na Baraza lipange muda wa kutosha, haiwezekani Kamati nne siku moja, siku mbili itakuwa mchezo na sasa hivi Machi/Aprili ndio lala salama. Wananchi wanatusikiliza, wanatungojea na wanatuhukumu.

Mhe. Mwenyekiti, nataka kusema jambo moja tu, kwa sababu mengi yamesemwa. Wakati wa semina ile ilisema hivi;

"Mhe. Spika, uongozi unaozingatia maadili na uajibikaji ni nyezo muhimu katika kukuza demokrasi na utawala bora. Katika nchi yoyote ile mara nyingi wananchi wanatarajia kuwa viongozi wao (Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi) watatetea, watawaletea maendeleo na kuwaondolea umasikini unaowakabili. Wajumbe wakiwa wawakilishi na wananchi kwenye Baraza watumie nafasi zao za uongozi na wajibu wao kwa kushirikiana na serikali kuwaletea wananchi maendeleo yanayotarajiwa. Mjumbe yeyote wa Baraza akumbuke daima kuwa cheo ni dhamana aliyopewa kwa faida ya wananchi na sio vyenginevyo. Maadili hayakatazi Mjumbe kuwa na mali au utajiri, kinachokatazwa ni Mjumbe kutumia vibaya nafasi yake ya ujumbe kwa manufaa yake binafsi au kujilimbikizia mali isiyo halali ambayo ni kinyume na sheria ya nchi".

Waheshimiwa Wajumbe, kwa kutumia nafasi hii, kinachokatazwa hapa ni viongozi kuwa sio wasiwe na mali, kuna Mwakilishi mmoja kasema jana mmoja kuwa viongozi humu ndani wana meli, wengine wana mahoteli, hii haikatazwi, lakini uwe umepata kwa halali, usiwe unavamia.

Mhe. Mwenyekiti, rafiki yangu mmoja yeye anazungumza kule, alikuwa ananambia yeye ni mnadhimu wetu, ana mradi wake anataka kufanya *drop* juu ya mikarafuu, ananambia Mhe. Ali Mzee ndugu yangu nina mradi wangu wa kufanya *drop research,* lakini sina ardhi, pahala na shamba. Sasa hana eka, anasema hata eka moja apewe hana, yule pale. Waziri wa Kilimo na Maliasili mpeni. Sasa kuna watu wana eka 20, 30, sasa yetu Mhe. Salmin Awadh Salmin, anataka eka tatu afanye *research,* hayo ndio mambo yanayokatazwa kujikusanyia, haya huyu Mhe. Waziri ananong'ona anasema yeye hana hata robo.

Sasa tupitishe ili tuweze kuhoji, Waheshimiwa Wajumbe, naomba tuipitishe hii kwa kauli moja, hapa kuna uchafu mwingi unafanywa, kila siku maripoti ya Kamati yanaundwa, lakini inashindikana kwa sababu huna pakwenda.

Leo kasema Mhe. Hamad Masoud Hamad, ana hoja yake kapeleka, amesema haijambo yeye yake ameambiwa labda kikao cha Machi, mwengine ana hili, Mhe. Mbarouk Wadi Mussa, ana hoja yake, sasa kama haijafanywa utaipeleka wapi, lakini kama kuna maadili basi maadili ndio utamaliza ndio dawa, tuunge mkono.

Mhe. Mwenyekiti, maadili sio vitambulisho tu, hapana, wengi wanasema vitambulisho, maadili ina mambo mengi na hivyo vitambulisho vyengine tupitishe mswada huu kwa kauli moja, hata wale wawili, watatu, tuupitishe na tuusimamie na tuone sasa tunafanya kazi ya maadili, tutawajibika hapa, tuwajibike, tuwe mfano na tusivamie vamie tu, si vizuri.

Sasa mimi nasema wakati umefika tujibadilishe, kwenye ile sheria ya kizungu inasema; tuwe na *integrity*, yaani tuwe na watu ambao tuna heshima. Mwakilishi akienda benki, akitaka shilingi milioni mia moja, anachukua barua kwa Katibu wa Baraza, mwananchi anatakiwa apeleke dhamana, kwa nini? Kwa sababu ana *integrity* ile uheshimiwa.

Sasa tuuheshimu uheshimiwa wetu kwa vitendo, tusionee watu, tusidhulumu watu, lakini na sisi wenyewe tusivamie vamie na wale wanaovamia vamia vitu huku na huku waache, tugawane kidogo, kwa sababu Mapinduzi yanasema tugawane kidogo tulichonacho, sio kila kitu uchukue wewe tu.

Mhe. Mwenyekiti, nafikiri nimejaribu kuzungumza kwa sababu ni kama nasaha. Sasa la mwisho kabisa amani na utulivu. Mtu mmoja alikuwa na jahazi yake, jahazi ni yake na kapakia watu, akawa ile jahazi anaitoboa, wale wakamwambia mbona jahazi unalitoboa? Akasema nini, jahazi si yangu, nyinyi ingieni tu, wale wakamwambia lakini hii jahazi ikitoboka wote sisi tutazama japo jahazi ni yako. Kwa hivyo, wale ambao wanadhani wana mamlaka ya kutoboa jahazi, waache kwa sababu hii jahazi ikitoboka, tutauwawa wote na amani hii tuliyonayo.

Juzi nimemsikia Dr. Ali Mohammed Shein, amesema sipendi kusema kizungu, lakini amesema,; "*enough is enough",* aliposema hivyo basi hali imerudi na sasa hivi *Alhamdulillah,* tuna amani na utulivu. Sisi Wajumbe wa Baraza tuna jukumu, nimesikia lugha humundani zilivyotumika, maneno yaliyotumika tuyawache. Kasema Mhe. Haji Omar Kheir, sisi wote humu hakuna mpinzani, sijasema mimi kasema yeye, wote sisi tuko ndani ya mfumo mmoja.

Mhe. Mwenyekiti, tarehe 29 Januari, 2009 Baraza lako tukufu lilipitisha Azimio la Baraza kufikiria kuunda Tume ya watu sita kuelimisha watu na hatimaye tukenda kwenye *referendum* na hatimaye kupata hii Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Sasa tudumishe amani, tunakwenda kwenye ving'ora, tunatukanana wenyewe kwa wenyewe, tunasemana, si tabia nzuri, halafu hapa tunakaa vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, huko kwenye ving'ora unamtukana halafu kwenye supu mnakaa pamoja, mnakunywa supu pale, bahati mbaya wananchi hawatuoni, tuwe na *integrity* ya kweli kweli, tupendane tujenge nchi yetu. Sisi hatujaunganisha vyama, mimi ndiye niliyekuwa Mwenyekiti, nataka niseme leo, mimi ndiye niliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati ile Wajumbe wa CCM ni Mhe. Haji Omar Kheir na Mhe. Ali Abdalla Ali, Wajumbe wa *CUF* ni Mhe. Nassor Ahmed Mazrui na Mhe. Abubakar Khamis Bakary.

Sisi ndio tuliozunguka, lakini hatujaunganisha vyama kila mtu ana chama chake na kila mtu atakwenda katika jukwaa mwaka 2015 kuuza bendera yake, lakini tunataka tufanye mambo yeende kiustaarabu.

Mhe. Rais, amesema tufanye kampeni za kistaarabu, tujenge nchi kistaarabu na mimi naamini katika mpira kila timu inasema itashinda, hakuna timu inayosema mimi sishindi, tukienda mwaka 2015 kila chama kitasema kitashinda na mimi naamini kwa kazi nzuri tunayofanya Chama cha Mapinduzi kitapewa bendera ya kuongeza nchi hii tena mwaka 2015/2020. (*Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa hayo, naunga mkono hoja hii na nawaomba wajumbe wote waunge mkono hoja hii kwa salama na amani. *(Makofi)*

Kwa hayo, sasa namaliza tutakutana kwenye Kamati huko mbele na ndugu zangu tuupitishe mswada huu kwa kauli moja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Ali Mzee Ali na sasa hivi basi tumpishe Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Utawala Bora aje kujibu hoja za Wajumbe.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Ikulu na Utawala Bora: Ilivyokuwa michango ya Waheshimiwa ya jioni hii bado hatujaifanyia kazi vizuri, basi itakuwa vyema ukinipa muda wa jioni hii kwenda kuweka mambo sawa ili asubuhi kesho nije kufanya majumuisho. Kwa hiyo, naomba kutoa hoja ya kusoma majumuisho yangu baada ya masaa sita.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Wajumbe wanaoafiki hilo wanyooshe mikono. Wote wamekubali nawashukuru.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Mwenyekiti: Sasa kwa kuwa muda wetu bado haujamalizika, namuomba Mwanasheria Mkuu aweze kutengua Kanuni ili tumalize muda huu kwa hii leo. Mhe. Mwanasheria Mkuu, karibu.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, naomba kurudia maneno ambayo tayari ameshazungumza na mtoa hoja Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Ikulu na Utawala Bora wa kutenga kando Kanuni ya muda ili apate muda mzuri wa kwenda kujitayarisha na majumuisho. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako hili tukufu liakhirishwe hadi kesho siku ya Ijumaa tarehe 30/O1/2015 saa 3:00 asubuhi. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante, sasa niwaulize tena Wajumbe waliokubali hoja wanyooshe mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, nichukue fursa hii kuwashukuru sana kwa michango yenu mbali mbali ambayo itasaidia sana kwa ajili ya kupitisha mswada huu. Lakini vile vile nichukue fursa kwa wale ambao waliokuwa wakisikiliza kwa utulivu na umakini wao. Kwa hiyo, niseme tu sasa hivi naakhirisha kikao hadi kesho tarehe 30/01/2015 saa 3:00 asubuhi.

(Saa 12:23 kikao kiliakhirishwa hadi tarehe 30/01/2015 saa 3:00 Asubuhi)